# Kiswahili

## Kidato cha

## 2

## Kitabu cha Mwalimu

©2024 Bodi ya Rwanda ya Elimu ya Msingi

Haki zote zimehifadhiwa.

Kitabu hiki ni mali ya Bodi ya Rwanda ya Elimu ya Msingi

Shukrani lazima zitolewe kwa Bodi ya Rwanda ya Elimu ya Msingi

wakati yaliyomo yamenukuliwa.

# Dibaji

Mwalimu mpendwa,

Bodi ya Rwanda ya Elimu ya Msingi inayo heshima kwa kutoa mwongozo wa mwalimu kwa kidato cha pili katika ngazi ya chini ya elimu ya sekondari.

Mwongozo huu ni waraka rasmi utakaoongoza ufundishaji na ujifunzaji kuendana na mtaala uegemeao katika uwezo.

Falsafa ya Elimu Rwanda inalenga kumpatia mlengwa uwezo kwa kila ngazi ya elimu ili kumwezesha kumudu vizuri katika jamii na kumpa fursa ya kujipatia ajira.

Ili kwenda sambamba na juhudi za kuboresha elimu, Serikali ya Rwanda inasisitiza umuhimu wa kufungamanisha ujifunzaji na ufundishaji na zana pamoja na mitaala ili kuwezesha mchakato wa ujifunzaji. Mambo mengi huathiri yale ambayo wanafunzi wanafundishwa, namna nzuri ya kujifunza na uwezo waupatao. Mambo hayo ni pamoja na umuhimu mahususi wa yaliyomo, ubora wa walimu, mbinu za ufundishaji na ujifunzaji, mikakati ya upimaji na vifaa vya kufundishia vilivyopo.

Tumezingatia umuhimu wa mbinu zenye mchakato wa kujifunza ambao unamwezesha mwanafunzi kuendeleza mawazo yake na kufanya ugunduzi mpya wakati wa mazoezi thabiti yawe ya binafsi au katika makundi. Wanafunzi, kwa msaada wa wakufunzi, watapata stadi za lugha zinazofaa zitakazowawezesha kutumia yale waliyojifunza katika miktadha ya maisha halisi. Kwa kufanya hivyo, wataonyesha tofauti siyo tu katika maisha yao binafsi bali pia hata kwa taifa .

Hii inatofautiana na mfumo wa zamani kuhusu nadharia ya ujifunzaji iliyosisitiza mchakato wa kujifunza kama upataji wa maarifa kutoka kwa yule aliyemzidi maarifa na hasa akiwa ni mwalimu.

Katika mtaala uegemeao katika uwezo, ujifunzaji unachukuliwa kama mchakato wa kazi ya kujenga na kuendeleza maarifa na ufahamu, stadi na maadili na mwenendo mwema kutoka kwa mwanafunzi ambapo dhana aghalabu huanzishwa kwa mazoezi, hali na mazingira yanayomsaidia mwanafunzi kujenga maarifa, kuendeleza stadi na upatikanaji chanya wa maadili na mwenendo mwema.

Aidha, kazi ya kujifunza hujishughulisha na wanafunzi kwa kufanya mambo na kufikiri kuhusu yale wanayoyafanya na wanafarijika kuonyesha uzoefu wao halisi na maarifa katika mchakato wa ujifunzaji.

Katika mtazamo huu, ili kutumia kitabu hiki kwa ufanisi, jukumu lako kama mkufunzi litakuwa :

- Kuandaa masomo yako na vifaa vya ufundishaji vinavyofaa,
- Kuandaa majadiliano katika makundi ya ushirikiano ya wanafunzi ukizingatia umuhimu wa ushauri kuwa kujifunza hufanyika kwa ufanisi wakati mwanafunzi afanyapo kazi kwa kushirikiana na watu wanaomzidi maarifa na uzoefu;

- Kushirikisha wanafunzi kwa kupitia kazi za ujifunzaji kama: njia ya uchunguzi, makundi ya mijadala, utafiti, mazoezi ya utafiti na kazi za kibinafsi;
- Kutoa fursa ya usimamizi kwa wanafunzi kwa kuendeleza uwezo wao, kwa kuwapa ushindani tofauti na kutoa majukumu yanayoongeza tafakuri tunduizi, utatuzi wa matatazo, ubunifu na uvumbuzi, mawasiliano na ushirikiano;
- Kutoa msaada na kuwezesha mchakato wa ujifunzaji kwa kutathmini mchango wa wanafunzi katika mazoezi ya darasani;
- Kuwaongoza wanafunzi ili waweze kuoanisha matokeo ya utafiti;
- Kutilia maanani tathmini ya kazi binafsi na kazi za makundi zilizofanyika darasani kwa kutumia mchakato na mbinu za tathmini zinazoegemea katika uwezo wa wanafunzi,
- Kuutumia mwongozo kutakusaidia katika kazi yako ya kufundisha kwani yaliyomo katika mwongozo huu wa mwalimu yanaeleweka kiasi kwamba unaweza kutumiwa kwa urahisi.

Ingawa mwongozo huu wa mwalimu una majibu kwa kila kazi zote zilizotolewa katika kitabu cha mwanafunzi, unaombwa kupitia kila swali na kazi kabla ya kutathmini.

Napenda, kwa moyo wote, kutoa shukrani zangu kwa watu wote walioshiriki kutoa mchango wao wa kuboresha mwongozo huu wa mwalimu, na hasa wafanyakazi wa Bodi ya Rwanda ya Elimu ya Msingi (REB/CTLR) walioandaa mchakato wa kazi hii tokea ilipoanzishwa.

Pongezi maalum ziwaendee walimu wa ngazi tofauti kwa msaada wao wa kuendeleza na kukamilisha zoezi hili.

Maoni au mchango wowote wa mawazo unakaribishwa kwa ajili ya uboreshaji wa kitabu hiki kwa matoleo mengine yatakayofuata baadaye.

**Dkt. MBARUSHIMANA Nelson**

**Mkurugenzi Mkuu, Bodi ya Rwanda ya Elimu ya Msingi**

RWANDA BASIC EDUCATION BOARD (REB)

## Shukrani

Napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wale wote walioshiriki kwa hali na mali katika kukiandaa na kukifanikisha kitabu hiki cha mwongozo wa mkufunzi. Kitabu hiki kisingeliwezekana bila kuwepo wadau mbalimbali walioshiriki; jambo ambalo limenifanya nitoe shukrani zangu za dhati.

Shukrani zangu za kwanza ni kwa wafanyakazi wa Bodi ya Rwanda ya Elimu ya Msingi walioshiriki katika kuandaa na kuandika kitabu hiki. Pia napenda kutoa shukrani kwa walimu wa ngazi zote kwa juhudi zao katika ufanikishaji wa kazi hii ya thamani.

Aidha, natoa shukrani kwa uongozi wa shule mbalimbali nchini Rwanda kwa kuwaruhusu walimu kushiriki katika kukiandaa na hata kukikimilisha kitabu hiki.

**Joan MURUNGI**

**Mkuu wa Idara ya Mitaala, Ufundishaji, Ujifunzaji na Zana ( CTLR)**

# Yaliyomo


**Dibaji** ........ iii

**Shukrani** ........ v

**Utangulizi** ........ vii

Azma ya mwongozo wa mwalimu ........ viii

Wanafunzi wenye mahitaji maalumu ........ viii

Mahitaji na majukumu ya jumla ya mwalimu katika ufundishaji na ujifundishaji ........ x

Vidokezo vya kutumia mwongozo wa mwalimu kwa kurejelea cha Kitabu Mwanafunzi ........ xviii

Ramani ya yaliyomo ........ xix

Andalio la somo ........ xxiv

**Sura ya 1: Mazungumzo na majadiliano** ........ 1

Msamiati na mawasiliano katika shughuli za kilimo na ufugaji ........ 1

**Sura ya 2: Utungaji** ........ 37

Barua kuhusu matembezi, barua za kirafiki, barua za mwaliko, simu, tangazo/ilani ........ 37

**Sura ya 3: Matumizi ya lugha katika mazingira mbalimbali** ........ 57

Rejesta za mpira na burudani ........ 57

**Sura ya 4: Mazungumzo na mawasiliano katika shughuli mbalimbali za kijamii** ........ 95

Msamiati katika kazi za jumuiya ........ 95

**Faharasa** ........ 133

**Vitabu vya rejea** ........ 137

## I) Utangulizi

Kitabu hiki kimeandaliwa ili kikuongoze kuafikia lengo la kila kipindi darasani kwa kumweka mwanafunzi katikati. Mbali na mbinu zilizotumika hapo awali, mbinu za kufunzia na kujifunzia zilizotolewa kwenye mwongozo huu zinampa mwanafunzi kipaumbele katika harakati za ufundishaji na ujifunzaji kama ilivyopendekezwa kwenye silabasi mpya. Kazi yako kama mwalimu itakuwa kuwaongoza wanafunzi wako kuafikia malengo ya mtalaa kwa kuwashirikisha kikamilifu katika kila somo.

Kitabu hiki kinakupa mwongozo kuhusu malengo ya kila kipindi ili ujiandae ipasavyo kabla ya kipindi husika. Mpangilio wa kitabu hiki unakifanya rahisi kutumika hivyo basi kurahisisha kazi yako ya kuafikia matarajio ya silabasi. Hata hivyo, yapo mambo muhimu ambayo sharti uyatilie maanani.

Jambo la kwanza ni kuitalii silabasi na kujua tosha yale unayohitajika kufunza siyo tu katika kidato hiki cha pili bali hata katika vidato vyote unamofunza Kiswahili.

Pili, ni jambo la busara kutayarisha ratiba yako ya mafunzo. Hili halina ugumu wowote kwa kuwa silabasi imejaribu kuonesha ni yapi ya kufunzwa katika kidato gani na kwa muda gani. Utakiwalo kulifanya ni kuyapanga hayo yaliyomo katika silabasi wiki kwa wiki.

Kumbuka hapa kwamba ratiba hii hutegemea uwezo walio nao wanafunzi wako. Utaratibu uliopewa katika silabi haujakufunga. Ingawa ni lazima yafunzwe yote yaliyomo katika silabasi, si lazima yafunzwe kwa kufuata utaratibu uliomo kwenye silabasi.

Ni muhimu kwako kama mwalimu kuandaa utaratibu wa somo ama masomo utakayoyafundisha siku yoyote ile. Mathalan, ikiwa leo utafunza kuhusu Msamiati wa mazao nchini Rwanda, ni sharti uwe na utaratibu wa kufunzia mada hiyo ndogo. Si jambo la kufaa kwako kuingia darasani bila utaratibu wowote wa kufunzia. Hatua za kufunzia pamoja na yote yanayohitajika lazima tayari uwe umeyapangia. Kufikia hapo, utakuwa yu tayari kuingia darasani.

Ni vizuri uwakumbushe wanafunzi kuhusu umuhimu wa Kiswahili hasa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki ili wawe na ari ya kukisoma na kukifahamu vyema. Kiswahili ni lugha ya Afrika inayozungumzwa na watu wengi barani Afrika na ulimwenguni kwa ujumla. Jamii ya Rwanda imezungukwa na nchi ambazo zinazungumza Kiswahili, kwa maana hii ipo haja ya kuwasiliana nao katika nyanja mbalimbali kama kisiasa, kiuchumi, na kijamii kwa sababu ni lugha inayozungumzwa katika nchi wanachama wa Jumuia ya Afrika ya Mashariki ambapo Rwanda ni mwanachama.

Katika harakati ya kufunza na kuwaongoza wanafunzi kujifunza, huenda ukakumbana na wanafunzi wenye uzito wa kuelewa au mahitaji maalumu. Wanafunzi hawa ni sharti wahusishwe kikamilifu katika shughuli zote za ufundishaji na ujifunzaji. Kamwe wasiachwe nyuma kutokana na hali zao. Ni sharti kila wakati wawe pamoja na wenzao kielimu na kwa mambo mengine yote.

## II) Azma ya mwongozo wa mwalimu

Azma ama lengo kuu la mwongozo huu wa mwalimu ni kukupa vidokezo vya mambo muhimu ya kuzingatia katika ufundishaji na ujifunzaji pamoja na hatua mbalimbali unazostahili kufuata unapofunza kila kipindi kutoka mwanzo wa kitabu hadi mwisho wake, ili wanafunzi wafaidike vya kutosha. Kila kipindi kimetoa pendekezo ambalo linalenga kufunza stadi nne za lugha: Kusikiliza na Kuzungumza (kupitia masimulizi mbalimbali, kuuliza maswali na kupata majibu), Kusoma (kusoma vifungu vilivyopo katika Kitabu cha Mwanafunzi kimoyomoyo, kwa sauti na katika vikundi, kusoma sentensi nyepesi zilizoandikwa ubaoni na kujisomea maagizo katika mazoezi mbalimbali), Kuandika (wanapojibu maswali katika mazoezi ya kibinafsi au kikundi na kadhalika). Pia kuna sarufi katika kila sura. Hakikisha kuwa stadi hizi zote zimetiliwa maanani wakati wa ufundishaji na ujifunzaji.

Licha ya kuwepo kwa vidokezo vya namna ya kufunza kila kipindi, ukumbuke kuwa huu ni mwongozo tu. Ni kielelezo kinachokuonesha njia unazoweza kupitia ili kufikia malengo fulani. Kwa kuwa wewe ndiwe unawafahamu vyema wanafunzi wako, upo huru kuongezea mbinu nyinginezo zitakazowasaidia wanafunzi wako kuafikia malengo ya kipindi husika. Usije ukajifunga kwa mwongozo.

Pia, mwongozo huu umetoa vidokezo vya namna ya kuwaandaa wanafunzi kwa minajili ya kazi ya wanafunzi wawili wawili au kikundi. Katika ufundishaji na ujifunzaji, mwongozo huu umetoa vidokezo vya namna ya kuwashughulikia wanafunzi wenye mahitaji maalumu na wale wenye uzito wa kuelewa. Mazoezi ya ziada pamoja na nyongeza ya msamiati upo kwenye kitabu hiki.

Vile vile, baaadhi ya majibu ya mazoezi yametolewa. Maelekezo ya namna ya kusahihisha baadhi ya maswali yasiyokuwa na majibu ya moja kwa moja yametolewa.

## III) Wanafunzi wenye mahitaji maalumu

Wapo baadhi ya wanafunzi wenye mahitaji maalumu ambao ni sharti wahusishwe katika ufunzaji na ujifunzaji. Hali ya wanafunzi hao hazifai kuwa kikwazo kwao kujifunza na kufunzwa. Wanafunzi hao ni kama vile wenye:

i) Matatizo ya kuona vyema
ii) Matatizo ya kusikia
iii) Udhaifu wa kusoma, kuandika na kuelewa mambo kwa kasi
iv) Udhaifu wa mawasiliano, kwa mfano, mwanafunzi anaweza kuwa huzungumza kwa kigugumizi au hana uwezo wa kutamka ipasavyo.
v) Udhaifu wa viungo vya mwili
vi) Wanafunzi walio na uwezo wa kuelewa mambo kwa kasi kuliko wanafunzi wa kawaida.

Ni jambo zuri uweze kutambua uwezo na udhaifu wa kila mwanafunzi kabla ya somo, wakati wa somo na baada ya somo. Kwa namna hiyo utaweza kushughulikia mahitaji

ya kila mwanafunzi kwa njia mwafaka ili udhaifu wao usitatize kufanikiwa kwa somo lako.

Jedwali lifuatalo linaonesha mifano ya mahitaji maalumu na jinsi ya kuyashughulikia.

| **Mahitaji** | **Namna ya kuyashughulikia** |
|---|---|
| 1. Matatizo ya kuona ipasavyo | - Hakikisha mwanafunzi ameketi karibu au mbali na ubao kulingana na mahitaji yake<br>- Hakikisha mwanafunzi ameketi karibu au mbali na mwangaza kulingana na mahitaji yake<br>- Epuka vifaa vinavyoweza kutatiza uwezo wa kuona<br>- Jadili na mlezi au mzazi uwezekano wa matumizi ya miwani |
| 2. Matatizo ya kusikia | - Hakikisha mwanafunzi ameketi karibu nawe au popote pengine ambapo ataweza kusikia vizuri<br>- Shauri kuhusu matumizi ya kuongeza sauti<br>- Ikiwezekana, tumia lugha ya ishara |
| 3. Kutoweza kusoma, kuandika au kuelewa mambo upesi | - Hakikisha umewapa wanafunzi kama hawa muda zaidi kuliko wanafunzi wengine<br>- Wape kazi ya ziada<br>- Wazuie kudhalilishwa kwa namna yoyote<br>- Endesha somo kwa hatua nyepesi hadi zenye ugumu kwa utaratibu<br>- Watengee muda maalumu wa kurudia mambo yaliyosomwa baadaye |
| 4. Udhaifu wa kuwasiliana | - Tumia mbinu tofauti za mawasiliano ili kutosheleza mahitaji yao<br>- Watengee muda wa kueleza mawazo yao<br>- Wakinge kutokana na matendo yanayoweza kutatiza hisia zao |
| 5. Ulemavu katika viungo vya mwili | - Hakikisha umewapa wanafunzi muda wa ziada<br>- Hakikisha wana vifaa vya kurahihisha kazi yao kutegemea ulemavu wao<br>Shauriana na walezi au wazazi wao jinsi ya kuwasaidia |
| 6. Wanafunzi walio na uwezo wa kuelewa mambo upesi | - Hakikisha umewapa kazi ya ziada ili wasiwatatize wengine<br>- Hakikisha umewapa nafasi ya kukuza vipaji vyao<br>- Hakikisha umewapa kazi zenye ugumu kiasi kuliko kazi ya wanafunzi wengine |

## IV) Mahitaji na majukumu ya jumla ya mwalimu katika ufundishaji na ujifundishaji

Yapo mahitaji ya jumla na ya kimsingi ambayo huhitajika ili kuafikia malengo ya kila kipindi. Mahitaji hayo ni kama vile: kufanya utafiti, kuandaa ratiba, kutwaa uongozi wa darasa, kuwahusisha wanafunzi katika ujifunzaji, kutathmini na kurekodi maendeleo ya wanafunzi, kuandaa wanafunzi kwa kazi za jozi au vikundi au darasa zima na kadhalika.

### Kufanya utafiti

Ni sharti mwalimu yeyote awe mtafiti. Je, pana jambo lolote ambalo hulielewi vizuri lakini ambalo litakufaa wakati wa kufundisha? Iwapo lipo, ni sharti ulitafitie ili kulielewa kabla ya kusimama mbele ya wanafunzi wako.

### Kuandaa ratiba

Andaa ratiba ya kazi yako. Upo mpangilio wa mafunzo ya mwaka mzima ambao huhitajika kutayarishwa kabla ya muhula wa kwanza kuanza na upo mpangilio wa vipindi wa kutumiwa kila siku. Ni sharti uwe na vitu hivyo viwili.

Ratiba yako ya kipindi ni sharti kilenge kufanikisha ujifunzaji na kuzua mazingira changamfu ambapo wanafunzi wote watashiriki na kufurahia somo lako. Unapoandaa kipindi:

i) Onesha vigezo vya ufaulu na mabadiliko ya mwenendo unapoanza kufundisha sura mpya.

ii) Jumuisha kazi mbalimbali zitakazofanywa na wanafunzi ili kukuza ujifunzaji na kupatikana kwa ujuzi unaotarajiwa.

    Kazi hizo ziwe za kuwasisimua wanafunzi. Wanafunzi wenye mahitaji maalumu au uzito wa kuelewa wawe na kazi nyepesi zitakazowawezesha kuafikia lengo lile lile. Kazi hizo zikuze stadi zote nne za lugha (kusikiliza, kuzungumza, kuandika na kusoma). Mfano: kuigiza mbele ya darasa mazungumzo fulani waliyosoma, kutengeneza tangazo la biashara, kuchora ramani au watu au mifugo mbalimbali na kupachika katika ukuta wa darasa, kuimba/kuandika shairi/wimbo kuhusu mada fulani, kusimuliana hadithi na kadhalika. Baadhi ya kazi hizo zipo kwenye Kitabu cha Mwanafunzi na kitabu hiki.

iii) Hakikisha kuwa una orodha ya zana au vifaa vyote kwa ajili ya kipindi husika.

Zana na vifaa vilivyopendekezwa kwa kila mada au sura zinaweza kutumika katika kufundishia pamoja na nyingine ambazo utaona zinafaa kutokana na mazingira yako. Unashauriwa kuwa mbunifu, kutumia na kutafuta zana mbadala kulingana na upatikanaji wa vifaa hivyo katika mazingira yako. Baadhi ya vifaa ambavyo vinaweza kutumika mara kwa mara ni pamoja na redio, picha za vifaa na vitu mbalimbali katika mazingira mbalimbali, picha za watu wa rika mbalimbali wakiwa katika miktadha tofauti, simu ya mkononi, kanda za sauti zenye mazungumzo na hotuba za Kiswahili, vitabu, matini au vifungu mbalimbali vya mazungumzo.

Zingatia vifaa visivyohitaji kununuliwa na vinavyopatikana kwa urahisi katika mazingira ya shule. Baadhi ya zana hizi unaweza kujitengenezea mwenyewe au kuwahusisha wanafunzi katika kuzitengeneza. Vifaa vingine vinapatikana katika mazingira ya shule kama vile mchanga, vijiti, na kadhalika. Pia unaweza kupata vifaa kutoka kwa walimu wanaofunza masomo mengineyo, mfano ramani (mwalimu wa Jiografia), rula (mwalimu wa Hisababti) au unaweza kuwapeleka wanafunzi katika eneo ambapo kifaa fulani kilipo.

iv) Hakikisha kuwa maelekezo/maagizo ya kufanya kazi fulani yanaeleweka kwa urahisi.

v) Zingatia uwezekano wa ratiba yako ya siku au wiki nzima kutatizwa na baadhi ya mambo kama vile sikuukuu, mkutano au shughuli ya kighafla au kidharura na kadhalika. Sharti pawepo mbinu za kuhakikisha kuwa kipindi au vipindi vitakavyoathirika vimefunzwa.

**Kutwaa uongozi wa darasa**

Silabasi hii inampa mwanafunzi kipaumbele katika ufundishaji na ujifunzaji. Kutokana na hali hii, baadhi yao huenda wakatumia vibaya fursa hii kwa kushiriki katika mambo yasiyokuwa na umuhimu wowote.

Kama mwalimu, lazima uhakikishe kuwa umetwaa uongozi wa darasa kwa kuwaelekeza wanafunzi kufanya kila jambo ipasavyo. Japo kuna kanuni za jumla za shule ambazo kila mwanafunzi anastahili kufuata, ni bora uje na kanuni zako vilevile za darasa. Unaweza kuwahusisha wanafunzi katika kutengeneza kanuni hizo kisha zibandikwe kwenye ukuta wa darasa. Wanafunzi wafahamu hatari ya kukiuka kanuni hizo na uhakikishe kuwa zimefuatwa kila unapofunza.

**Kuwahusisha wanafunzi kikamilifu katika ufundishaji na ujifunzaji**

Lengo kuu la silabasi hii ni kuwapa wanafunzi fursa ya kujenga maarifa yao wenyewe. Ili kuafikia haya, hakikisha kuwa:

i) ujifunzaji unakuwa hai, wa kina, wa kuvutia na wenye ujenzi wa tabia

ii) umewaongoza wanafunzi ndani na nje ya darasa kushiriki kupitia mbinu mbalimbali shirikishi kuendeleza ujifunzaji kama mwanafunzi mmoja, katika jozi au katika makundi. Sisitiza ushirikiano katika ujifunzaji.

iii) umetoa mwongozo kwa wanafunzi katika kujenga maarifa yao wenyewe kuliko kuwapatia maarifa

iv) umewahusisha wanafunzi wote katika ujifunzaji wakiwemo wanafunzi wenye uzito wa kuelewa na mahitaji maalumu katika kufanikisha kujifunza somo lililokusudiwa kwa ufanisi

v) wape baadhi ya wanafunzi fursa ya kuwafunza wengine mbele ya darasa au kuwaimbia au kuongoza katika kufanya shughuli fulani muhimu

vi) jenga uhusiano mwema kati yako na wanafunzi ili wakuone kama mtu anayewajali na kuwapenda

vii) andaa mikakati ya kuwawezesha wanafunzi kuendelea kujifunza au kukitumia kile walichojifunza darasani hasa wanapokuwa nje ya darasa.

**Kutathmini na kurekodi maendeleo ya wanafunzi**

Ufundishaji na ujifunzaji ni mchakato unaohusisha hatua mbalimbali na kipindi fulani cha wakati. Yapo malengo matatu makuu: kuna lengo la kila kipindi, muhula na mwaka mzima. Kama mwalimu, sharti ufanye tathmini za kutimizwa au kutotimizwa kwa malengo haya kwa kila mwanafunzi darasani. Matokeo ya utathmini wako ni sharti yarekodiwe ili uweze kuyatumia baadaye.

Tathmini ni mchakato wa kupima ufundishaji na ujifunzaji kwa kukusanya na kutafsiri vigezo binafsi vya mwanafunzi katika mchakato wa kujifunza na kuvitolea hukumu kuhusu mafanikio ya mwanafunzi kuhusu upimaji wa viwango vilivyotolewa. Tathmini ni sehemu muhimu katika mchakato wa kujifunza. Katika mtalaa wa upimaji wa ujuzi, tathmini inapaswa iwe imelenga katika ujuzi ambao mwanafunzi atapewa, mazingira mchanganyiko au magumu yanayohusiana na maisha yake ya kila siku na kuambiwa atumie aliyojifunza katika kupambana au kujitatulia matatizo hayo. Tathmini itapangwa au kufanywa katika ngazi nzifuatazo: Tathmini katika ngazi za shule, mitihani ya wilaya, tathmni ya kitaifa (LARS) na mtihani wa taifa.

**Aina za tathmini**

***i) Tathmini endelezi ifanyikayo shuleni (Tathmini ya ujifunzaji)***

Tathmini endelezi inatumia mbinu rasmi na zisizo rasmi zitumikazo shuleni kuangalia kama ujifunzaji unafanyika kama inavyokusudiwa au la. Unaweza kutumia mbinu zifuatazo katika kufanya tathmini endelezi:

- Unapoandaa somo lako, onesha vigezo vya ufaulu na mabadiliko ya mwenendo unapoanza kufundisha sura mpya.
- Baada ya kumaliza kila mada, hakikisha kuwa wanafunzi wote wamemudu yaliyoongelewa katika ujuzi upatikanao katika kila mada kabla ya kuanza kujifunza mada inayofuata.
- Pima jinsi kila mwanafunzi atakavyomudu vizuri somo lake pamoja na tafakuri tunduizi zilizoelezwa katika muhtasari.
- Rekodi kiwango cha ujuzi katika jedwali. Tazama mfano uliotolewa.

***Jedwali la kurekodi kiwango cha ujuzi uliopatikana***

| Jina la mwanafunzi | Ujuzi wa kusoma na kuandika | Ujuzi wa kuwasiliana na wenzake | Ujuzi wa ubunifu | Ujuzi wa tafakuri tunduizi | Ujuzi wa kufanya utafiti na kutatua matatizo | Ujuzi wa kushirikiana na wenzake |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Kaliza | √√ | √√√ | √ | √√√ | √ | √√ |
| Musoni | √ | √√√ | √√ | √ | √ | √√√ |
| Umuhire | √√√ | √ | √√√ | √√√ | √ | √√ |
| Gabiro | √√ | √ | √√√ | √ | √√√ | √√ |

**Maelezo**

√√√: Mwanafunzi ana ujuzi uliotajwa

√√: Mwanafunzi ana ujuzi wa wastani

√: Mwanafunzi hana ujuzi uliotajwa

Kutokana na haya, utapata picha halisi kuhusu maendeleo ya ujifunzaji wa kila mwanafunzi.

***ii) Upimaji wa jumla (Upimaji wa kujifunza)***

Wakati upimaji unapotumiwa kurekodi ujuzi uliopatikana katika ujifunzaji wa mwanafunzi, inakuwa inalenga upimaji wa jumla. Upimaji wa jumla hutoa picha ya ujuzi au mwelekeo maalum kwa muda fulani.

Makusudi muhimu ya upimaji wa jumla ni kutathmini kuwa malengo ya kujifunza yameafikiwa na kutumia matokeo ya kurekodi au ngazi ya mwanafunzi, kwa kutoa uamuzi wa maendeleo yake kwa kuchaguliwa katika ngazi nyingine ya elimu au ngazi ya kupata cheti.

Tathmini hii ni lazima iweke pamoja mwelekeo au maoni ambapo mwanafunzi ataweza kuonesha alivyomudu ujuzi wote alioupata katika ujifunzaji. Inaweza ikawa upimaji shuleni au nje ya shule kwa muundo wa mitihani ya taifa.

Upimaji wa jumla shuleni hususan ule wa kila mtihani wa somo unapaswa kufanyika mara moja mwishoni mwa kila muhula wa masomo na mara moja tena mwishoni mwa kila mwaka wa masomo. Wastani wa matokeo ya upimaji wa jumla shuleni kwa kila somo utapimwa, kurekodiwa na kuwekwa miongoni mwa matokeo ya mtihani wa mwisho kitaifa.

Maswali ya majaribio yametolewa mwishoni mwa kila sura katika Kitabu cha Mwanafunzi kama njia ya kutathmini mwanafunzi katika upimaji wa jumla.

**Vigezo katika kuandika upimaji wa kiujumlishaji**

Kabla ya kuandaa karatasi ya maswali, mpango wa kile kitakachoulizwa lazima uandaliwe kwa kuonesha sura au mada zitakazoulizwa, idadi ya maswali kwa kila kiwango cha *Bloom`s taxonomy* na kuonesha alama zilizopangwa kwa kila swali. Katika mtihani upimao ujuzi, maswali kutoka katika kila kiwango cha *Bloom`s taxonomy* yanatakiwa yapewe uzito kuliko yale yanayotoka katika kiwango cha maarifa na ufahamu.

Kabla ya kuandaa karatasi ya maswali, jaribio au maswali ya mtihani lazima yapangwe sambamba na upimaji wa ujuzi kwa kufanya yafuatayo:

- Kutambua mada za kuuliza kutoka muhtasari kulingana na somo
- Kufupisha yaliyomo katika somo ukifikiria kuwa ndio msingi wa zoezi
- Kutambua matokeo ya kujifunza yatakayopimwa katika zoezi
- Kuandaa jedwali la mambo muhimu yanayotakiwa

- Kuhakikisha kuwa vitenzi vilivyotumiwa katika uandaaji wa maswali havihitaji kumbukumbu za kukumbuka peke yake bali vinavyopima mawanda ya ujuzi.

**Kuwaandaa wanafunzi kwa kazi za wanafunzi wawili wawili na kazi za vikundi**

Kazi ya kushirikiana inahakikisha kuwa ujifunzaji unatawaliwa na utendaji wa watu, unakuwa hai na shirikishi, na wenye kuzingatia ushirikiano. Mbali na kazi za kushirikiana zilizopo kwenye Kitabu cha Mwanafunzi, unaweza kubuni na kuwapatia wanafunzi kazi mbalimbali za kufanya au kwa ajili ya majadiliano ya papo kwa papo.

***Jinsi ya kuwapanga wanafunzi katika vikundi***

Zipo njia mbili kuu unazoweza kutumia katika kuandaa kikundi: kuwaweka wanafunzi wenye uwezo sawa pamoja au kuwaweka wanafunzi wenye uwezo mbalimbali pamoja.

***Kuwaweka wanafunzi wenye uwezo sawa pamoja***

Waweke wanafunzi wenye uwezo sawa katika kikundi kimoja endapo unalenga kuwapa wanafunzi wenye uwezo tofauti tofauti kazi zisizofanana. Mfano:

- Ikiwa una wanafunzi wenye uzito wa kuelewa, unaweza kuwaweka katika kikundi kimoja ili uweze kuwapa usaidizi maalumu. Kwa mfano, unaweza kuwafunza tena ujuzi ambao hawakuelewa wakati wa kipindi au kuwapa kazi maalumu itakayowasaidia kupata ujuzi uliokusudiwa.
- Unaweza kuwaweka wanafunzi wenye uzito wa kuelewa katika kikundi kimoja kisha ukawaongezea mwanafunzi mmoja au wawili wenye wepesi wa kuelewa wawasaidie.
- Unaweza kuwaweka wanafunzi wenye wepesi wa kuelewa pamoja ili kuwapa kazi za ziada wenzao wangali wakifanya kazi ya awali.
- Endapo una wanafunzi wasiosikia, unaweza kuwaweka katika kikundi kimoja ili waweze kutumia lugha ya ishara pamoja.
- Ikiwa una vifaa maalumu kwa kila kundi fulani la wanafunzi wenye uwezo mmoja, unaweza kuwaweka katika kikundi kimoja ili watumie vifaa hivyo.

***Kuwaweka wanafunzi wenye uwezo mbalimbali pamoja***

Waweke wanafunzi wenye uwezo mbalimbali pamoja ikiwa wanafanya kazi sawa. Mfano, kazi mbalimbali katika Kitabu cha Mwanafunzi ni sawa. Hapa, hakikisha kuwa kila kikundi kina wanafunzi wenye uzito wa kuelewa, wepesi wa kuelewa na wenye mahitaji maalum pale ambapo hamna vifaa maalumu kwa wanafunzi. Unapofanya hivyo, wahimize wanafunzi wenye wepesi wa kufahamu kuwasaidia wenzao ili wawe katika kiwango kimoja. Fanya vivyo hivyo katika kazi ya wanafunzi wawili wawili. Mwambie mwanafunzi mwenye wepesi wa kuelewa kumsaidia mwenzake ili naye afikie kiwango chake.

***Upana wa kikundi***

Zipo aina mbili za vikundi: kikundi kidogo na kikundi kikubwa. Kwa kawaida, kikundi hujumuisha wanafunzi kati ya watano na wanane kwa kila kikundi na vikundi visivyozidi vinane katika darasa zima.

Hata hivyo, upana au wingi wa vikundi utategemea idadi ya wanafunzi katika darasa lako pamoja na kazi husika wanayostahili kufanya katika kikundi.

Unaweza kuwaweka wanafunzi katika kikundi cha wanafunzi kati ya watatu na wanne. Idadi hii inafaa zaidi kwa zoezi jepesi linalohitaji uhusika mwingi wa kila mwanafunzi. Mfano: zoezi la imla litahitaji kila mwanafunzi kutaja au kuandika na kutamka maneno au vifungu fulani vya maneno. Kwa kuwa zoezi hili linalenga kukuza ujuzi wa kutamka au matamshi bora, inahitaji kila mwanafunzi kushiriki. Hapa basi, unaweza kuwa na kikundi cha wanafunzi watatu watatu au wawili wawili.

Endapo kazi inahitaji utafiti wa kina na mjadala, unaweza kuwaweka wanafunzi kati ya watano na wanane katika kikundi kimoja. Hata hivyo, idadi hii itabadilika kutegemea idadi ya wanafunzi katika darasa zima.

Kila kikundi kiwe na kiongozi. Viongozi wanaweza kuwa wanafunzi wenye uwezo tofauti tofauti wa kufahamu. Si lazima kiongozi awe mwanafunzi mwenye wepesi wa kufahamu pekee. Wape wanafunzi wenye uzito wa kufahamu na wenye mahitaji maalumu fursa ya kuongoza kama wenzao.

Kumbuka kuwa zipo kazi ambazo zinaweza kufanywa na wanafunzi wawili wawili kama vile kuigiza mazungumzo ya wahusika wawili, kuimba au kujibizana, kuzungumza, kusoma au kujadili mambo fulani katika vitabu vyao, kufanya mazoezi fulani pamoja na kadhalika.

**Hatua za kufuata unapofunza vikundi au kutathmini kazi za vikundi**

Hakikisha kuwa umepitia kazi fulani ya kikundi unapojiandaa kwa somo. Kazi hiyo ioane na ujuzi unaotarajiwa kupatikana mwishoni mwa kipindi husika na uwaelekeze wanafunzi vilivyo ili waafikie ujuzi huo. Kazi nyingi za vikundi na wanafunzi wawili wawili zipo katika Kitabu cha Mwanafunzi. Baadhi ya kazi hizo zinaweza kufanywa kama sehemu ya ujifunzaji katika kipindi fulani.

Amua upana wa kila kikundi na ikiwezekana, orodha ya majina ya wanafunzi watakaounda kila kikundi.

Baada ya kuamua idadi ya wanafunzi katika kila kikundi, fuata hatua hizi tano:

**i) Fanya maandalizi kwa makini**

Endapo utatumia vikundi vikubwa vyenye viongozi, waambie viongozi kuhusu mambo unayotarajia wafanye kisha uwape vifaa watakavyotumia. Unapowapa viongozi wa vikundi maagizo, hakikisha kuwa wanafunzi wengineo wanasoma yaliyomo ubaoni au kuchora au kuimba wimbo fulani au kushika na kuzungumzia vifaa tofauti tofauti.

Kila kikundi kiwe na kifaa fulani kama kiini cha kazi wanayofanya. Kifaa hicho kinaweza kuwa kitu chochote ikiwemo karatasi ambayo kiongozi wao anatumia kuandikia hoja zinazojadiliwa.

**ii) Toa maagizo yanayoeleweka**

Waambie wanafunzi kazi mahususi wanayotarajiwa kufanya na jinsi ya kuifanya. Ni sharti wafahamu wanayotarajiwa kufanya katika kikundi na matokeo yake mwishoni.

**iii) Chunguza maendeleo ya kila kikundi**

Wanapofanya kazi ya kikundi, hakikisha umezuru kila kikundi haraka iwezekanavyo ili uhakikishe kuwa wanafanya kazi hizo kwa usahihi. Hii ndiyo sababu ya kuunda vikundi vichache vyenye wanafunzi wengi ili irahisishe kazi yako ya kuvichunguza.

Hakikisha kuwa kila kikundi kimekamilisha kazi yake kwa muda uliovitengea. Hakikisha pia kuwa kila kikundi kimepata fursa ya kuwasilisha matokeo yao chini ya dakika zilizosalia baada ya kujadiliana. Tumia mbinu wanazoelewa kuonesha kuwa muda wa kujadiliana umeisha.

**iv) Uwasilishaji wa vikundi**

Hakikisha kuwa umetenga muda wa kupata ripoti ya yaliyojadiliwa au kutathmini ujuzi waliotarajiwa kupata kwa kuwapa shughuli fulani.

Hakikisha kuwa kila kikundi kimepata nafasi ya kutosha kuwasilisha ripoti zao au kutathminiwa.

Hakikisha kuwa kazi zote zimeoneshwa kwa darasa zima kufikia kipindi fulani cha wakati bila kubagua kazi unazodhani kuwa hazijafanywa vizuri au ipasavyo.

**v) Kila kazi lazima iwe na lengo maalumu**

Lengo linaweza kuwa kuweza kusoma au kutamka maneno fulani, kuonesha aina fulani za mazao na umuhimu wao, kupendekeza njia za kufanya au kuzuia jambo fulani, kuigiza mazungumzo fulani na kadhalika.

Wakati wa kazi za vikundi, hakikisha kuwa kila mwanachama ana shughuli ya kufanya kikundini. Wahimize viongozi kuwahusisha, kuwasaidia na kuwahamasisha wanafunzi wote kwenye kikundi. Kwa mfano katika kikundi kimoja, wanachama mbalimbali wanaweza kufanya kazi hizi:

- Kiongozi ahakikishe kuwa kila mwanafunzi anashiriki na kuwa wanafunzi wenye wepesi wa kuelewa au wenye kupenda kusema hawatawali mjadala kiasi cha kuwatenga wenzao
- Atakayewasilisha sharti asikize kwa makini ili ikiwezekana, awasilishe ripoti yake kwa kukariri au kupitia uchoraji au jedwali na kadhalika.
- Mwenye kuwakumbusha wenzake kuhusu wakati lazima amakinike ili kengele ikilia asikie na ahakikishe kuwa shughuli za kikundi zinakamilika kwa wakati uliotengwa.
- Anayesimamia rasilimali ahakikishe kuwa kikundi kina vifaa vyote muhimu na kuwa vifaa hivyo vimetumika kwa njia inayofaa.

Kumbuka kutembea kutoka kikundi kimoja hadi kingine wakati wa kazi za vikundi au wanafunzi wawili wawili. Kazi yako iwe kusikiliza kwa makini yanayojiri katika kila kikundi na utoe usaidizi pale tu panapohitajika. Unapotembea na kuchunguza maendeleo ya kila kikundi, tathmini jinsi wanafunzi wanavyofanya kazi zao, jinsi kila mwanafunzi anavyoshiriki na ushirikiano uliopo baina ya wanachama.

Kumbuka kuwa kazi za vikundi huwa na kelele. Baadhi ya kazi hizi zinaweza kufanywa nje ya darasa ili kuepuka kuwapigia kelele wenzao katika madarasa mengine.

**Kazi ya mwanafunzi binafsi**

Zipo kazi fulani ambazo sharti zifanywe na mwanafunzi akiwa pekee. Hali hii itakuweza kutathmini hatua ambazo kila mwanafunzi amepiga katika upatikanaji wa ujuzi na maarifa. Kazi nyingi zinazohusu kuandika au kuchora hufanywa na mwanafunzi binafsi. Kupitia njia hii, unaweza kuchunguza maandishi ya kila mwanafunzi au uwezo wao wa kuchora na kufasiri maneno. Pia, unaweza kupima uwezo wao wa kusoma au kutamka maneno fulani.

**Kazi za wanafunzi wenye mahitaji maalumu**

Ikiwezekana, hakikisha kuwa kuna vifaa kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu. Unapowapa wanafunzi kazi mbalimbali, hakikisha kuwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu wamepewa kazi tofauti zitakazowawezesha kupata ujuzi uleule.

Mfano, mwanafunzi mwenye uzito wa kuona anaweza kufahamu mambo mbalimbali kwa kuguza. Ikiwa kazi fulani inahitaji wanafunzi kuangalia na kutaja majina ya vifaa fulani, unaweza kumpa mwanafunzi mwenye uzito wa kuona vitu hivyo ili naye aviguse na kutaja majina yao. Ikiwa kazi fulani inahitaji wanafunzi kuchora, wape wanafunzi wenye ugumu wa kuona vifaa vitakavyowawezesha kufinyanga vitu hivyo. Mfano: unaweza kumpa udongo au vifaa maalumu vya kutumia katika ufinyanzi.

Baadhi ya wanafunzi wenye matatizo ya kiakili huenda wasiweze kuchora lakini wakawa na uwezo wa kutumia rangi mbalimbali chini ya usaidizi wako au wenzao.

Endapo kuna kazi inayohitaji wanafunzi kutaja kwa sauti majina ya vifaa fulani vinavyooneshwa ubaoni, wape wanafunzi wasioweza kusema fursa ya kuonesha vitu hivyo kwa kutumia kijiti au rula.

**Kazi za ziada**

Baadhi ya wanafunzi wenye wepesi wa kuelewa huenda wakamaliza zoezi fulani mbele ya wenzao. Hakikisha kuwa umewapa mazoezi zaidi yanayohusiana na lengo la kipindi husika ili wasikae bila kazi ya kufanya.

Wapo wanafunzi wenye uzito wa kufahamu. Unaweza kuwapa kazi za ziada baada ya kipindi ili wafanye baadaye. Kazi hizo zilenge kuwafanya kuafikia lengo la somo. Watengee muda baada ya kipindi kupitia kazi hizo. Unaweza kufanya hivyo wakati wa mapumziko.

## V) Vidokezo vya kutumia mwongozo wa mwalimu kwa kurejelea Kitabu cha Mwanafunzi na silabasi

Silabasi na Kitabu cha Mwanafunzi ni vifaa viwili muhimu ambavyo ni sharti uvitumie na kurejelea kila wakati.

Silabasi itakuongoza kufahamu mambo muhimu unayostahili kutilia maanani wakati wa kufunza somo fulani. Hakikisha kuwa umesoma na kufahamu matarajio ya silabasi kwa kila kipengele unachotarajia kufunza katika kipindi fulani.

Ni sharti urejelee Kitabu cha Mwanafunzi kila unapofunza lolote lililoandikwa kitabuni humo. Baada ya kufunza jambo hilo ni sharti uwaongoze wanafunzi kuyarudia uliyoyafunza kwa kuyarejelea vitabuni mwao.

Zipo kazi nyingi za vikundi na wanafunzi wawili wawili katika Kitabu cha Mwanafunzi. Kazi hizi zijumuishe kama sehemu za kazi zako zote unazopanga kutumia katika ufundishaji na ujifunzaji. Njia bora zaidi ya kufunza stadi za lugha kama vile kusoma na kuandika ni kupitia Kitabu cha Mwanafunzi. Stadi za Kuzungumza na Kusikiliza pia zinaweza kuafikiwa kupitia Kitabu cha Mwanafunzi pale unapowapa wanafunzi fursa ya kuzungumzia michoro iliyomo vitabuni humo au kusimulia tena hadithi au kuigiza mazungumzo kwenye kitabu mbele ya darasa.

Kumbuka kuwa yamo baadhi ya mambo katika mwongozo huu ambayo hayamo katika vitabu vya wanafunzi. Mambo haya ni nyongeza yako ya kukutajirishia kazi yako.

Nambari za kurasa unazohitaji kurejelea katika kila kipengele zimeandikwa katika kitabu hiki ili zirahisishe kazi yako.

## vi) Ramani ya yaliyomo

| | **Sura 1**<br>**Mazungumzo na majadiliano (Msamiati na mawasiliano katika shughuli za kilimo na ufugaji)** | **Sura 2**<br>**Utungaji (Barua kuhusu matembezi, Barua za kirafiki, Barua za mwaliko, Simu,Tangazo/Ilani)** | **Sura 3**<br>**Matumizi ya lugha katika mazingira mbalimbali (rejesta za mpira na burudani)** | **Sura 4**<br>**Mazungumzo na mawasiliano katika shughuli mbalimbali za kijamii (Msamiati katika kazi za jumuiya)** |
|---|---|---|---|---|
| **Idadi ya vipindi** | 20 | 12 | 20 | 20 |
| **Shabaha** | i) Kuelewa na kutumia msamiati wa mazao nchini Rwanda na kuutumia katika mawasiliano ya kila siku<br>ii) Kuelewa msamiati kuhusu kilimo na ufugaji na kuutumia katika mawasiliano ya kila siku<br>iii) Kuutambua msamiati wa wanyama wa porini na kuutumia katika mawasiliano<br>iv) Kutumia kwa usahihi nomino, vivumishi, viwakilishi na vielezi<br>v) Kuelewa wakati uliopita -li- na ujao -ta- na vitenzi vya silabi moja | i) Kuandika barua za kirafiki na rasmi kwa kufuata muundo na kanuni zake<br>ii) Kutambua na kutumia istilahi muhimu katika matangazo mbalimbali<br>iii) Kutumia alama mbalimbali za uandishi | i) Kutumia kwa usahihi lugha ya rejesta mbalimbali<br>ii) Kutumia majina ya ngeli ya KI-VI na kuyatungia sentensi za umoja na wingi<br>iii) Kutumia majina ya ngeli ya KI-VI pamoja na vivumishi | i) Kutumia msamiati wa kazi za jumuiya kulingana na mazingira tofauti nchini<br>ii) Kutumia msamiati wa shughuli za kijamii kulingana na mazingira tofauti nchini<br>iii) Kuuliza maswali kwa usahihi<br>iv) Kutambua na kutumia aina saba za maneno ya Kiswahili katika mawasiliano ya kila siku |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mbinu** | i) Kufanya mazoezi ya kutumia kamusi ili kupata maana ya maneno ya kilimo na ufugaji<br>ii) Majadiliano ya wanafunzi wawili wawili na katika vikundi<br>iii) Kuainisha na kubainisha aina za maneno ya Kiswahili<br>iv) Kutunga sentensi sahihi | i) Kuainisha matini mbalimbali kwa usahihi<br>ii) Majadiliano ya wanafunzi wawili wawili na katika vikundi<br>iii) Kuainisha na kubainisha aina za maneno ya Kiswahili<br>iv) Kutunga sentensi sahihi | i) Kuigiza katika vikundi rejesta mbalimbali<br>ii) Kubainisha na kuainisha aina mbalimbali za rejesta<br>iii) Majadiliano ya wanafunzi wawili wawili na katika vikundi<br>iv) Kufanya kazi za mradi<br>v) Kutunga sentensi sahihi | i) Kusoma vifungu vya habari na kujibu maswali<br>ii) Majadiliano ya wanafunzi wawili wawili na katika vikundi<br>iii) Kuainisha na kubainisha aina mbalimbali za maneno<br>iv) Kutunga sentensi sahihi |
| **Zana na vifaa** | Picha za aina mbalimbali za mazao, mifugo na wanyama wa porini. | Majarida, vitabu, kalamu, karatasi, bahasha, stempu, picha ya mtu akitumbukiza barua kwenye kisanduku cha posta. | Mchezo uliorekodiwa, mpira, picha za wachezaji uwanjani, picha za wachezaji mashuhuri, picha za maeneo mbalimbali yanayojulikana kuwa na rejesta maalumu kama vile kanisani, hospitalini, mahakamani na kadhalika. | Picha zinazoonesha matukio ya shughuli mbalimbali za kijamii kama vile *umuganda*, mkutano, harusi, mazishi, n.k. |
| **Shughuli za wanafunzi** | - Kufanya mazoezi ya kutumia kamusi ili kupata maana za maneno mapya yanayojitokeza katika zana za kujifunzia kuhusu kilimo na ufugaji.<br>- Kuoanisha shughuli mbalimbali za kilimo zijulikanazo nchini Rwanda kwa kuzingatia majira ya mwaka. | - Kutokana na fani ya kila aina ya matini walizopatiwa (barua, matangazo, mwaliko), wanafunzi waainishe matini hizo kwa usahihi.<br>- Kila mwanafunzi azungumzie barua ya kirafiki aliyoiandika mara yake ya kwanza kwa kueleza mwandikiwa na ujumbe aliompelekea na lugha aliyoitumia. | - Katika makundi, wanafunzi wapewe rejesta mbalimbali za mpirani na burudani na kuziigiza.<br>- Licha ya rejesta za michezo na burudani, wanafunzi wapewe rejesta nyingine tofauti zitumiwazo katika mazingira mbalimbali kama vile hotelini, mahakamani, bungeni, n.k. | - Kusoma vifungu vya habari kuhusu shughuli mbalimbali za kijamii na kujibu maswali ya ufahamu na kisha kutoa muhtasari wa kifungu cha habari husika bila kuzidi aya moja.<br>- Wakishirikiana katika vikundi, wanafunzi wajadili shughuli za kijamii walizoshiriki na kisha kuwasilisha mbele ya darasa. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | - Kuandika, katika vikundi, vifungu vya habari vielezeavyo mazao, zana za kilimo na aina za majina ya mifugo ifugwayo katika maeneo wanamoishi.<br>- Kujadiliana majina ya mazao na mifugo isiyopatikana katika maeneo yao.<br>- Kufanya mjadala mdogo kuhusu faida ya aina fulani ya mazao na mifugo mbalimbali.<br>- Kuainisha na kubainisha aina za maneno kama vile vielezi, viwakilishi na vivumishi katika vifungu vya habari vilivyotolewa.<br>- Kutunga sentensi zinazohusiana na kilimo na mifugo katika wakati uliopo na uliopita, hali uyakinishi na ukanushi.<br>- Kubaini sentensi zenye kuonesha hali ya yakinishi na kanushi. | - Katika vikundi wanafunzi wachague wenyewe mada za kuandikia barua za kirafiki, mwaliko, tangazo na ilani na kisha waandike wakizingatia matumizi sahihi ya kanuni za utungaji.<br>- Wanafunzi washiriki kusoma barua, tangazo au ilani kwa sauti na kisha kujibu maswali yatokanayo na maudhui ya hicho kilichosomwa. | - Kubainisha na kuainisha aina mbalimbali za rejesta kutokana na matini walizopewa na wahakikishe wanaeleza sifa za msingi za aina hiyo ya rejesta.<br>- Wanafunzi washiriki katika majadiliano kuhusu dhana ya michezo na burudani katika kujenga afya.<br>- Wanafunzi wafanye kazi ya mradi wa kukusanya rejesta zinazotumika katika mazingira mbalimbali na kuzitolea maoni darasani.<br>- Kubainisha matumizi sahihi na yasiyo sahihi ya ngeli za KI-VI.<br>- Wanafunzi watunge sentensi fupi kadhaa wakitumia majina ya ngeli ya KI-VI umoja na wingi. | - Kila mwanafunzi kusimulia au kueleza mambo muhimu yanayojitokeza katika shughuli ya kijamii aliyoshiriki zaidi.<br>- Kupitia vifungu mbalimbali vya habari, wanafunzi washiriki katika kuainisha na kubainisha aina mbalimbali za maneno kama yanavyojitokeza katika vifungu hivyo.<br>- Wanafunzi wafanye mazoezi ya kutunga sentensi kwa kutumia wakati ujao hali yakinishi na hali kanushi. |
| **Ujuzi unaopatikana** | Uwezo wa kusikiliza, kuzungumza, kujadili, kusoma na kuandika kuhusu shughuli za kilimo na ufugaji. | Uwezo wa kuandika barua kuhusu ziara au matembezi aliyoyafanya, barua za kirafiki na kadi za mialiko ya aina mbalimbali kwa kufuata taratibu za uandishi. | Uwezo wa kusikiliza, kusoma, kuandika na kubaini sifa na dhima za rejesta mbalimbali katika mazingira ya michezo na burudani. | Uwezo wa kusikiliza, kuzungumza, kujadili, kueleza, kusoma na kuandika matini mbalimbali kuhusu shughuli au kazi za jumuiya kulingana na mazingira tofauti nchini. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Stadi za kujifunza** | - Kutumia msamiati sahihi katika mawasiliano yanayohusu shughuli za kilimo na ufugaji.<br>- Kugawa majira ya mwaka katika miezi yajitokezamo nchini Rwanda.<br>- Kwa kutumia msamiati uhusuo kilimo na mifugo, kufanya utungaji sahihi wa tungo kimaandishi na kimazungumzo.<br>- Kufanya mjadala kuhusu masuala ya kilimo na ufugaji.<br>- Kulinganisha na kutofautisha utokeaji wa matumizi ya aina mbalimbali za maneno katika mawasiliano yanayohusu kilimo.<br>- Katika mawasiliano, kutumia kwa usahihi wakati uliopo (kuhusu vitenzi vyenye silabi moja) na wakati uliopita katika hali yakinishi na hali kanushi. | - Kulinganisha na kutofautisha miundo ya barua za matembezi na aina nyinginezo za kirafiki, matangazo, mialiko na ilani.<br>- Kutumia vyema kanuni za uandishi katika utungaji wa barua za matembezi, kirafiki, matangazo, na ilani.<br>- Kuandika barua, ilani na matangazo kwa usahihi kutokana na malengo husika.<br>- Kutumia kwa usahihi alama za uandishi katika utungaji wa barua za kirafiki, mialiko, matangazo, n.k. | - Kutumia rejesta za michezo na burudani katika mazungumzo ya kila siku katika mazingira mbalimbali.<br>- Kujadili sifa za msingi za aina mbalimbali za rejesta zitokeazo katika michezo na burudani.<br>- Kulinganisha na kutofautisha msamiati unaojitokeza katika aina mbalimbali za michezo na burudani.<br>- Kutumia maarifa waliyoyapata kuhusu rejesta za michezo na burudani kuchunguza aina nyingine za rejesta zinazojitokeza katika jamii na namna zinavyotumika katika mawasiliano.<br>- Kujenga uwezo wa kufanya mawasiliano kwa kuzingatia rejesta ya mazingira husika.<br>- Kutumia kwa ufasaha majina ya ngeli ya KI-VI na U-ZI kwa kuzingatia mabadiliko yanayojitokeza toka umoja kwenda wingi. | - Kutumia msamiati maalum katika mawasiliano yanayohusisha shughuli mbalimbali za kijamii.<br>- Kupangilia makundi ya shughuli mbalimbali za kijamii zilizopo katika jamii.<br>- Kuunda maelekezo ya mambo yanayopaswa kuzingatiwa katika shughuli mbalimbali za kijamii.<br>- Kulinganisha na kutofautisha shughuli moja ya kijamii dhidi ya shughuli nyingine.<br>- Kutumia aina mbalimbali za maneno katika utungaji wa tungo sahihi za Kiswahili.<br>- Kutunga sentensi mbalimbali kwa kutumia wakati ujao hali yakinishi na hali kanushi. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Maadili na mwenendo mwema** | i) Kuwa na mwelekeo chanya kuhusu somo la Kiswahili<br>ii) Kuridhika na shughuli za kilimo<br>iii) Kuheshimu kazi za watu wanaojishughulisha na kilimo na ufugaji<br>iv) Kuwa na moyo wa ushirikiano | i) Kuonyesha adabu na heshima kwa watu mbalimbali anaowaandikia barua za kirafiki na rasmi<br>ii) Kujenga ushirikiano miongoni mwa wanajamii kwa kudumisha mawasiliano na upendo | i) Kuonyesha adabu na heshima kwa watu mbalimbali katika michezo na burudani<br>ii) Kuonyesha shauku ya kupenda michezo<br>iii) Kujenga urafiki pamoja na ushirikiano kwa watu wa rika zote | Kuonyesha heshima na ushirikiano wakati wowote kwenye shughuli mbalimbali za kijamii |
| **Masuala mtambuka** | i) Mafunzo kuhusu uzalishaji mali<br>ii) Mafunzo ya mazingira na maendeleo ya kudumu | Mafunzo ya amani na maadili | i) Mafunzo ya amani na maadili<br>ii) Mafunzo dhidi ya mauaji ya kuangamiza (kimbari) | i) Mafunzo dhidi ya mauaji ya kuangamiza (kimbari)<br>ii) Mafunzo ya amani na maadili |
| **Upimaji/ Tathmini** | i) Matumizi ya msamiati sahihi katika mawasiliano yanayohusu ufugaji na kilimo<br>ii) Matumizi ya aina mbalimbali za maneno ya Kiswahili katika mawasiliano<br>iii) Matumizi ya wakati uliopo na wakati uliopita katika hali ya uyakinishi na ukanushi<br>iii) Kujibu maswali ya marudio ya sura kwa usahihi | Uandishi wa barua mbalimbali za kirafiki, mialiko, matangazo na ilani kwa kuzingatia miundo sahihi na kanuni za kiuandishi na uwasilishaji wa ujumbe kwa namna iliyokusudiwa | Kuwasiliana kwa kutumia rejesta mbalimbali na kujua aina mbalimbali za rejesta | Uelewa wa mawasiliano yanayojitokeza katika shughuli mbalimbali za kijamii |

### vii) Andalio la somo

**Jina la shule**: .................                **Jina la Mwalimu:** .........................

| **Muhula** | **Tarehe** | **Somo** | **Kidato** | **Mada** | **Idadi ya masomo** | **Muda** | **Idadi ya wanafunzi** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | 03/01/2017 | Kiswahili | Cha pili | Ya kwanza | 1 /20 | Dakika 40 | 56 |

| | |
|---|---|
| **Aina ya wanafunzi wenye mahitaji maalum ya kielimu watakaoshughulikiwa katika somo, idadi yao kulingana na mahitaji yao** | matatizo ya kutoona vizuri :1<br>matatizo ya kutosikia vizuri: 1 |
| **Mada** | Msamiati wa msingi kuhusu mazao na shughuli za kilimo na ufugaji nchini Rwanda. |
| **Uwezo uhitajiwao katika mada** | Wanafunzi waweze kusikiliza, kuzungumza, kujadili, kusoma na kuandika kuhusu shughuli za kilimo na ufugaji |
| **Kichwa cha somo** | Msamiati wa msingi kuhusu shughuli za kilimo |
| **Malengo ya kujifunza** | Kulingana na msamiati wa msingi uliopendekezwa kutoka kifungu cha habari, wanafunzi watakuwa na uwezo wa kutumia kwa usahihi msamiati huo katika mawasiliano yanayohusu shughuli za kilimo. |
| **Mahali ambapo somo litafundishiwa** | Darasani |
| **Vifaa au zana kwa wanafunzi wote** | Kitabu cha Mwanafunzi, daftari, kalamu, Kamusi ya Kiwahili Sanifu, vifaa halisi kama jembe, fyekeo, panga, mbegu za aina mbalimbali kama mahindi, maharage, karanga, viazi, n.k. |
| **Marejeo** | Kamusi ya Kiswahili Sanifu, TUKI, Dar es Salaam (2004), Kitabu cha Mwalimu, MK Publishers, Kigali (2015), Mpangilio wa masomo, muhtasari wa somo |

| **Muda na hatua za somo** | **Mbinu za kufundishia na kujifunzia**<br>Kazi katika makundi: wanafunzi wajadiliane kuhusu msamiati husika kabla ya kuchunguza maana yake kutoka kamusi ya Kiswahili sanifu. | | **Uwezo wa jumba na masuala mtambuka pamoja na maelezo kwa kifupi** |
|---|---|---|---|
| | **Wajibu wa mwalimu** | **Wajibu wa mwanafunzi** | |
| **Utangulizi**<br>**Dakika 5** | ♦ Mwalimu aulize wanafunzi mmoja kwa mmoja walichokula nyumbani huku akiandika kwenye ubao majina ya vyakula wanavyotaja<br>♦ Kutokana na swali alilouliza na majibu yaliyotolewa, mwalimu aombe wanafunzi wajaribu kufumbua somo linahusu nini.<br>♦ Mwalimu aandike kichwa cha somo ubaoni pamoja na malengo mahususi ya somo husika.<br>Kwa kumhusisha katika somo yule mwanafunzi aliye na matatizo ya kutoona vizuri, mwalimu atampa nafasi karibu na ubao. | ♦ Wanafunzi wajibu mwalimu aina za vyakula walivyokula vikiwemo vinavyotokana na shughuli za kilimo<br>♦ Wanafunzi wajaribu kutaja fikra zao kwa kujibu swali la mwalimu.<br>♦ Wanafunzi wafuate kwa makini na kujitayarisha kuingia kwenye somo lenyewe | **Uwezo wa jumba:**<br>**Mawasiliano katika lugha rasmi:** kwa matumizi bora ya lugha kwa kupitia njia ya kujibu maswali ya mwalimu pamoja na kuwasiliana katika makundi. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Somo jipya Dakika 30** | Mwalimu anagawa vitabu, kila mwanafunzi na nakala yake kisha awaambie wafungue kwenye ukurasa husika na kusoma kimya kwa muda wa dakika tano.<br><br>Mwalimu awasomee wanafunzi kwa sauti inayosikika iwezekanavyo kwa kumwezesha mwanafunzi mwenye matatizo ya kutosikia vizuri kushiriki katika somo huku akizingatia alama za uakifishaji.<br><br>Mwalimu awaongoze wanafunzi kusoma mmoja baada ya mwingine aya moja moja na kueleza maana ya maneno mapya yaliyomo. Iwezekanavyo, atumie vifaa vya ufundishaji kama mbegu za maharage, mahindi, viazi kulingana na kifungu cha ufahamu.<br><br>Mwalimu awaongoze wanafunzi katika makundi yao wafanye zoezi la kujaza nafasi zilizoachwa wazi katika sentensi kwa kutumia msamiati waliopewa kuhusu shughuli za kilimo.<br>Mwalimu asahihishe kazi za wanafunzi katika makundi yao kisha awaongoze kusahihisha kwenye ubao | Wanafunzi wafungue vitabu na kusoma kimya yaliyo kwenye ukurasa huo.<br><br>Wanafunzi wasikilize kwa makini huku wakitumia vitabu vyao.<br><br>Wanafunzi wasome kwa sauti inayosikika kwa kuzingatia matamshi sahihi ya sauti za Kiswahili pamoja na kushiriki katika kueleza maneno mapya.<br>Hali kadhalika, wanafunzi watazame na kuoanisha vifaa na msamiati kutoka kwenye kifungu cha ufahamu.<br>Katika makundi yao, wanafunzi waandike sentensi zenye nafasi wazi kwenye madaftari yao na kuzijaza kwa kutumia msamiati waliopewa.<br><br>Wanafunzi washiriki katika kusahihisha kwa kujaza sentensi ubaoni. | **Ushirikiano, utawala binafsi na stadi za maisha**: wanafunzi katika makundi yao wanachagua viongozi ili wawaongoze kwa kuheshimiana katika kufanya kazi husika<br><br>**MASUALA MTAMBUKA**<br><br>**Usawa wa jinsia:** wanafunzi wanafanya kazi katika makundi yanayohusisha wasichana na wavulana bila ubaguzi wowote.<br><br>**Malezi yasiyokuwa na ubaguzi wowote:** wanafunzi wenye matatizo mbalimbali kama kutosikia na kutoona vizuri wanasaidiwa na wenzao pamoja na mwalimu darasani |
| **Hitimisho Dakika 5** | Mwalimu achukue mifano mitano ya mazao yaliyozungumziwa katika kifungu cha habari moja baada ya jingine na kuwataka wanafunzi wataje jina la kila zao. | Wanafunzi washiriki kwa kutoa majibu haraka haraka kwa kufuata mwongozo waliopewa na mwalimu. | |
| **Tathmini ya mwalimu** | Lengo za ujifunzaji limefikiwa. | | |

**Maelezo mafupi kuhusu namna ya kutumia kielelezo cha kipindi**

Utaratibu wa somo ni mpangilio wa jinsi mwalimu atalifundisha lengo lake darasani. Utaratibu wa somo huwa na utangulizi, mwili na hitimisho. Ukianza na utangulizi unapata kuwa ni jinsi mwalimu atakavyoanza somo lake. Azma kuu hapa ni kuwatia wanafunzi ari ya kufunzwa ama hata kuwazindua kutoka ndoto za mchana na kuzirudisha akili zao darasani.

Nao mwili wa utaratibu au mpangilio huu huwa na lengo, vifaa na utaratibu wa kufunzia. Sehemu hii hupangwa hatua kwa hatua. Hatua hizo ndizo zifuatwazo wakati wa kufundisha darasani.

Lengo huwa ni sehemu ya funzo ambayo itafunzwa katika kipindi hicho kimoja lakini utaratibu huwa ni hatua atakazofuata mwalimu wakati wa kufundisha lengo hilo. Sehemu hii hujibu maswali; *Je, mwalimu anataka afanye nini darasani mwake?Je, wanafunzi wanahitajika kufanya mambo gani?*

Ikumbukwe hapa kuwa ni sharti mwanafunzi awekewe mkazo wa juu katika utaratibu huu wa kufundisha na kujifunza. Ni sharti aongozwe katika kujigundulia anayofunzwa *Je, wanafunzi wanahitajika kufanya nini?* bali si kwa kujazia maarifa akilini mwake bila yeye mwenyewe kushiriki.

Nazo nyenzo ama vifaa, kama ulivyoona hapo awali, huwa ni vile vitu ambavyo utatumia darasani ili kuwarahisishia wanafunzi kuelewa vilivyo linalofundishwa. Ni jambo la kufaa sana iwapo utajitahidi kutumia nyenzo za kila namna sana sana zile ambazo hazihitajiki kununuliwa. Yapo mambo mengi katika mzingira ya shule ambayo yanaweza kuwa nyenzo ama kufanyiziwa nyenzo.

Jambo jingine hapa ni kwamba kila unapotayarisha somo lako ni sharti ukumbuke mada kuu na ndogo ambazo ndizo asili ya anayoyatayarishia. Mtazamo wa namna hii hukuwezesha kuona jinsi masomo yanavyohusiana.

Nayo jinsi ya kutumia wakati uliotengewa kila kipindi ni jambo muhimu pia. Kama ilivyotajwa hapo juu, wakati uliopewa wa dakika 40 huhitaji kugawanywa kwa hekima. Kama ilivyooneshwa hapo juu, sehemu kubwa ya wakati huo huwa kwa kuwaongoza wanafunzi katika kukuza stadi zao za lugha. Kusikiliza huweza kukuzwa kwa mambo kama vitendawili na vitanzandimi nako kuzungumza kunaweza kukuzwa kwa mijadala na hata kujibu maswali. Kusoma kunaweza kukuzwa kwa mazoezi mengi ya kusoma makala mbalimbali nako kuandika kunaweza kukuzwa kwa kuandika majibu ya mazoezi, kuandika barua na hata mitungo. Itafaa ikikumbukwa hapa kuwa stadi hizi nne huingiliana mumo kwa mumo japo zinaweza kutengwa.

Jambo jingine hapa ni kwamba zipo kazi za vikundi. Vikundi hivi vina azma ya kuwafanya wanafunzi kufanya mazoezi ya jambo lililofunzwa. Mbali na hilo, wanapata kujinoa katika mambo ya kusema mbele ya wenzao kwa kujiamini pamoja na kujizoesha

kutafiti. Mbali na haya, wanafunzi hupata fursa ya kujifunza kutoka kwa wenzao na kuiga wale walio wazuri zaidi. Haya na mengineyo ndiyo faida ipatikanayo kutoka kwa kazi ya vikundi hivi.

Isitoshe, kila kipengele cha kufunzwa kimedokezewa hatua zake za jinsi ya kukifunza. Hii ni pamoja na msamiati. Vile vile, una ruhusa ya kuyaongezea wanafunzi mazoezi. Unaweza kuwapa wanafunzi mazoezi ya ziada na ya ujumla baada ya kumaliza kufunza mada kuu fulani.

Nayo majibu ya mazoezi mengi yaliyomo vitabuni mwa wanafunzi yametolewa mwongozoni humu. Lakini pale ambapo wanafunzi wanahitajika kutunga sentensi, kwa mfano, ama pale ambapo wanajadiliana, hapana majibu yaliyotolewa. Itakuwa juu yako wewe mwalimu kuwaelekeza.

Pia ni muhimu sana kukumbuka hapa kwamba unaweza kuwa na wanafunzi wenye mahitaji maalumu darasani mwako. Hawa ni sharti wafunzwe na wenzao bila kutengwa na ni sharti wenzao watiwe moyo wa kuwasaidia siyo kwa huruma lakini kwa moyo wa urafiki. Nawe inakubidi uwe karibu nao na kutenga wakati wa kuwasaidia mmoja mmoja ama kwa vikundi vikundi bila kuonyesha dalili zozote kuwa wao ni tofauti na wenzao. Wanafunzi wa namna hii huhitaji kuonyeshwa kwamba kasoro zao haziwezi kuwarudisha nyuma.

Karibu!

Sura ya 1

# Mada kuu: Mazungumzo na majadiliano (Vipindi 20)

## Mada ndogo: Msamiati na mawasiliano katika shughuli za kilimo na ufugaji

### Uwezo upatikanao katika mada

Uwezo wa kusikiliza, kuzungumza, kujadili, kusoma na kuandika kuhusu shughuli za kilimo na ufugaji.

**Mbinu za kufundishia na kujifunzia**

i) Kufanya mazoezi ya kutumia kamusi ili kupata maana za maneno mapya yanayojitokeza katika zana za kujifunzia kuhusu kilimo na ufugaji.

ii) Kuoanisha shughuli mbalimbali za kilimo zijulikanazo nchini Rwanda kwa kuzingatia majira ya mwaka.

iii) Kuandika, katika vikundi, vifungu vya habari vielezeavyo mazao, zana za kilimo na aina za majina ya mifugo ifugwayo katika maeneo wanamoishi.

iv) Kujadiliana majina ya mazao na mifugo isiyopatikana katika maeneo ya wanafunzi.

v) Kufanya mjadala mdogo kuhusu faida ya aina fulani ya mazao na mifugo mbalimbali.

vi) Kuainisha na kubainisha aina za maneno kama vile vielezi, viwakilishi na vivumishi katika vifungu vya habari vilivyotolewa.

vii) Kutunga sentensi zinazohusiana na kilimo na mifugo katika wakati uliopo na uliopita, hali ya uyakinishi na ukanushi.

viii) Kubaini sentensi zenye kuonesha hali ya yakinishi na kanushi.

### Uhusiano wa mada na masomo mengine

Mada hii inahusiana na masomo ya Jiografia na Kilimo kwa kuzingatia ufundishaji wa usafirishaji wa mazao kutoka sehemu moja hadi nyingine na mafunzo ya jumla kuhusu kilimo na ufugaji nchini Rwanda.

### Vigezo vya tathmini na upimaji

Uwezo wa kutumia msamiati sahihi katika mawasiliano yanayohusu ufugaji na kilimo, kutumia aina mbalimbali za maneno katika mawasiliano hasa vivumishi, vielezi na viwakilishi, kutumia wakati uliopo na uliopita katika hali ya uyakinishi na ukanushi.

### Zana na vifaa

Picha za aina mbalimbali za mazao, mifugo na wanyama wa porini.

## Kipindi cha 1

### Funzo

Utangulizi wa somo la Kiswahili, kidato cha pili.

### Shabaha

Kufikia mwishoni mwa kipindi hiki, mwanafunzi aweze:

i) Kuwa na ufahamu wa kutosha kuhusu yale anayotarajiwa kujifunza katika kidato cha pili.

ii) Kuwa na ari ya kuongeza kiwango chake cha Kiswahili.

**Zana na vifaa muhimu kwa kipindi hiki**

i) Kitabu cha Mwanafunzi

ii) Silabasi ya kidato cha pili

iii) Vifaa husika vya wanafunzi wenye mahitaji maalumu.

### Mbinu

Mhadhara pamoja na kuwashirikisha wanafunzi kuuliza maswali.

## Utaratibu

***Hatua ya 1***

Kwa kuwa hiki ni kipindi cha kwanza katika mwaka mpya na vilevile kidato hiki cha pili, unaweza kuanza kufunza kwa kuwauliza wanafunzi maswali ya kuwaongoza kuzungumzia likizo yao.

***Hatua ya 2***

Waongoze wanafunzi wayajue yale wanayotarajiwa kukamilisha mwaka huu.

***Hatua ya 3***

Watie wanafunzi hamu ya kutaka kuitekeleza kazi ya darasa hili.

***Hitimisho***

Wape wanafunzi fursa ya kuulizia lile ambalo hawakulielewa katika yote ambayo umepitia.

### Maadili na mwenendo mwema

Wanafunzi wawe na mwelekeo chanya kuhusu somo la Kiswahili.

### Tathmini

Tathmini uelewa wa wanafunzi kuhusu mada mbalimbali wanazotarajiwa kusoma katika Kidato cha Pili.

## Kipindi cha 2 na 3

### Funzo

Msamiati wa mazao nchini Rwanda

**Shabaha**

Kufikia mwisho wa kipindi hiki, mwanafunzi awe na uwezo wa:

i) Kuelewa msamiati wa mazao nchini Rwanda.

ii) Kuutumia vilivyo msamiati huo wa mazao katika mawasiliano yake ya kila siku.

**Zana na vifaa muhimu kwa vipindi hivi**

i) Vifaa halisi tofauti tofauti vya mazao ya nchini Rwanda.

ii) Michoro au picha mbalimbali za mazao ya nchini Rwanda.

iii) Kitabu cha Mwanafunzi.

iv) Vifaa vya wanafunzi wenye mahitaji maalumu.

**Mbinu**

Mhadhara, kuwashirikisha wanafunzi kuuliza na kujibu maswali, kusoma na kujibu maswali ya kifungu.

**Kipindi cha 2**

**Utaratibu**

***Hatua ya 1***

Onyesha wanafunzi michoro ya mazao mbalimbali. Wape wanafunzi fursa ya kutambua mazao husika. Baadaye, taja jina la kila zao. Waambie wanafunzi wataje kila jina wakikuiga. Fanya hivyo mpaka uridhike kuwa wamelipata vizuri. Halafu eleza maana ya kila msamiati wa mazao.

***Hatua ya 2***

Sasa, tunga sentensi ukitumia msamiati uliofunza na uwape wanafunzi wengi iwezekanavyo fursa ya kutunga sentensi zaidi wakitumia msamiati huo.

Baadhi ya msamiati wa mazao ni kama vile mkahawa, mbuni, mgomba, maharagwe, mtama, nanasi, muhogo, mbatata, viazi vitamu, mahindi, mhindi, miharagwe na kadhalika.

***Hatua ya 3***

Waongoze wanafunzi kuulizana maswali kuhusu msamiati waliojifunza. Kwa mfano:

i) Ni mazao yapi yanayokuzwa katika eneo utokako?

ii) Eleza maana ya neno mbaazi.

iii) Wanyarwanda wengi hupanda mmea gani?

iv) Ni zao lipi lituletealo pesa za kigeni nyingi kuliko mazao mengine?

***Hatua ya 4***

Waongoze wanafunzi kusoma kifungu chini ya ‘Msamiati wa mazao nchini Rwanda’ katika Kitabu cha Mwanafunzi, ukurasa wa 1 na kujibu maswali chini yake.

Baada ya hayo, waongoze wanafunzi kufanya masahihisho ya maswali waliyoyafanya.

### Maadili na mwenendo mwema

Kuridhika na shughuli za kilimo.

### Tathmini

Mwanafunzi adhihirishe stadi za kusikiliza, kuzungumza, kusoma na kuandika.

**Zoezi la ziada**

1. Wanafunzi wataje mazao ya kienyeji nchini Rwanda na mazao ya kisasa.
2. Wanafunzi walinganishe na kutofautisha faida za mazao ya kienyeji na mazao ya kisasa.

**Majibu ya zoezi**

1. Mwanafunzi atafute maana ya maneno husika na atungie sentensi sahihi.
2. Mwanafunzi ajibu vilivyo na aeleze faida za kila zao alilotaja.

   Mfano: Matikitimaji. Faida: Matunda haya ni maarufu sana katika hoteli nyingi. Mkulima anaweza kuuza mazao yake katika hoteli na akapata faida kubwa.
3. Mwanafunzi atunge sentensi sahihi kama vile:
   a) Ndizi za mgomba huu ni tamu sana.
   b) Dona ni unga wa mahindi.
   c) Kahawa huzaliwa na mbuni.
   d) Chipsi hutengenezwa kutoka kwa mbatata.
   e) Je, zipo aina ngapi za maharagwe?
   f) Ni sharti utumie majani chai kutengeneza chai.
4. Majina ya mazao na faida zake ni kama ifuatavyo:
   a) Kiazi kikuu. Faida: Ni chakula cha nyumbani na pia huuzwa ili kumpa mkulima mapato.
   b) majani ya mchai. Faida: Hutumiwa katika kuandaa kinywaji cha chai. Huuzwa katika nchi za nje na kuletea nchi yetu pesa za kigeni.
   c) Kabichi. Faida: Ni mboga maarufu. Hutumiwa kama chakula nyumbani na mkulima anaweza kuuza kabichi sokoni na kujipatia mapato.
   d) Karoti. Ni mboga maarufu. Hutumiwa kama chakula nyumbani na mkulima anaweza kuuza kabichi sokoni na kujipatia mapato.
   e) Kitunguu. Ni kiungo maarufu kinachotumiwa wakati wa kukaanga vyakula mbalimbali. Hutumiwa pia katika kachumbari. Hutumiwa nyumbani na mkulima anaweza kuuza kitunguu sokoni na kujipatia mapato.
   f) Nanasi.faida: Nanasi hutoa maji matamu yanayomaliza kiu. Maji hayo hutumiwa kutengeneza sharubati au soda.

## Kipindi cha 3

### Funzo

Kazi ya wanafunzi wawili wawili na kikundi

## Utaratibu

***Hatua ya 1***

Wanafunzi wataje msamiati mbalimbali wa mazao waliojifunza na kufunzwa katika kipindi kilichotangulia.

***Hatua ya 2***

Waongoze wanafunzi kufanya kazi ya wanafunzi wawili wawili na ile ya kikundi katika Kitabu cha Mwanafunzi, ukurasa wa 4. Hakikisha kuwa wanafunzi wote wameshiriki.

***Hatua 3***

Kila kikundi kiwasilishe matokeo yake mbele ya darasa.

## Kipindi cha 4 na 5

### Funzo

Msamiati kuhusu shughuli za kilimo nchini Rwanda

### Shabaha

Kufikia mwishoni mwa vipindi hivi, mwanafunzi awe na uwezo wa:

i) Kuelewa msamiati kuhusu shughuli za kilimo nchini Rwanda.
ii) Kuutumia vilivyo msamiati huo katika mawasiliano yake ya kila siku.

**Zana na vifaa muhimu kwa vipindi hivi**

i) Unaweza kutumia michoro ama picha za msamiati wa shughuli za kilimo.
ii) Unaweza kuwapeleka wanafunzi vilipo vifaa unavyofunza.
iii) Unaweza kutumia vifaa halisi vya maneno unayofunza (*Kumbuka hapa kuwa katika kufunza msamiati wowote ule, kutumia kifaa halisi ndiyo njia nzuri zaidi ya kumfanya mwanafunzi kuelewa linalofunzwa.*)
iv) Kitabu cha Mwanafunzi.
v) Vifaa vya wanafunzi wenye mahitaji maalumu.

### Mbinu

Kujadiliana katika vikundi vya wanafunzi wawili.

## Kipindi cha 4

## Utaratibu

### *Hatua ya 1*

Unaweza kuanza hapa kwa kuwaonyesha wanafunzi kifaa, mchoro ama kitendo cha neno unalofundisha. Kwa mfano, ikiwa unafundisha kuvuna, unaweza kuiga kitendo cha kuvuna hindi na kulitupa pahali fulani. Hakikisha kuwa maigizo yako hayawapotoshi wanafunzi. Ama ikiwa unafundisha neno fyekeo, waonyeshe fyekeo utamke huku na wao wakitamka, tunga sentensi na uwaongoze na wao kulitungia sentensi sahihi neno lilo hilo. Ama ikiwa unafunza trekta, wapeleke wanafunzi lilipo trekta na ulifunze neno hilo na mengineyo husika. Baadhi ya maneno ya kufunzwa hapa ni yale yaliyomo vitabuni mwao.

### *Hatua ya 2*

Kwa mbinu hizo hizo, wafunze wanafunzi maneno zaidi yapatikanayo katika mazingira yao. Maneno kama uhifadhi wa udongo, mmomonyoko, tufani, upepo mkali kiangazi na kadhalika yanaweza kuongezwa na kuhusishwa na shughuli za kilimo.

### *Hatua ya 3*

Waongoze wanafunzi kutazama michoro na kukisoma kifungu kilichomo vitabuni mwao. Wape fursa ya kuulizia yale ambayo hawakuyaelewa.

### *Hatua ya 4*

Waongoze wanafunzi katika kufanya maswali ya kifungu na kusahihisha majibu.

### Maadili na mwenendo mwema

Kuheshimu kazi za watu wanaojishughulisha na kilimo.

### Tathmini

Tathmini uwezo wa mwanafunzi kushiriki katika mazungumzo huku akitumia Kiswahili sanifu.

### Majibu ya maswali

1. Mwanafunzi atafute maana za maneno aliyopewa katika kamusi na atunge sentensi sahihi. Ukumbuke hapa kuwa muundo wa sentensi unaweza kuwa sahihi lakini maana ya neno ikawa potovu. Hapo mwanafunzi atakuwa amenoa.

Mifano ya sentensi

a) Mkulima ameutia upanga makali.
b) Fyekeo jipya limenunuliwa.
c) Plau inakokotwa na ng’ombe.
d) Mkulima analiendesha trekta polepole.

e) Mbolea imesambazwa shambani.
f) Samadi itaongeza rutuba shambani.
g) Udongo wa shamba letu unahitaji mbolea.
h) Mimea hukua vizuri kwenye udongo wenye rutuba.
i) Tulizing'oa kwekwe zote zilizomea katikati ya mihindi.
j) Mbegu zote zimepandwa kwa uangalifu.
k) Mche uliopandwa juzi utakua vyema.
l) Pampu iliyotumiwa jana imeoshwa.

2. Manufaa ya kilimo yaliyotajwa hapa ni kutumia mazao kuwa ni chakula chetu, kuyauza mazao hayo na kupata pesa za matumizi yetu mengine na kupata pesa za kigeni, kuimarisha uchumi wa nchi yetu Rwanda na kuimarisha wakulima wengi.

   Manufaa mengine matano ambayo hayakutajwa hapa ni kupiga vita uchochole, kusaidia katika usafishaji wa hali ya hewa, kuimarisha uzalishaji na ukuzaji wa mifugo, kuimarisha afya ya Wanyarwanda, na kutia ari ya kufanya utafiti zaidi wa kuimarisha mazao.
3. Kauli hii si kweli kwa sababu Karekezi anawahimiza wenzake wasome hadi chuo kikuu ndipo wawe wakulima bora zaidi.
4. Yanasaidia mkulima kuelewa vilivyo kazi yake ya kilimo.
5. 1) kuvuna 2) kupiga dawa 3) kufyeka
   4) kupanda mbegu 5) kunyunyizia maji 6) kupalilia
   7) kulima
6. a) i) plau ii) trekta/tingatinga iii) fyekeo iv) jembe v) upanga vi) shoka
   b) Hakikisha kuwa kila sentensi ni sahihi.
7. kufyeka, upanga, kuvuna, jembe, palilia, koboa, kulima, fyekeo, plau, trekta,

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | K | U | F | Y | E | K | A |
| | | | Y | | O | U | G |
| A | T | K | E | R | T | V | N |
| M | K | | K | | A | U | A |
| I | O | | E | | | N | P |
| L | B | | O | P | L | A | U |
| U | O | J | E | M | B | E | |
| K | A | I | L | I | L | A | P |

Mifano ya sentensi
1. Tulishauriwa **kufyeka** kwekwe kabla ya kuanza kulima.
2. Mkulima ameutia **upanga** makali.
3. Kazi iliyobaki katika shamba hilo ni **kuvuna**.
4. **Jembe** hilo limetiwa mpini mwingine.

5. Kaitesi ame**palilia** mihindi yote.
6. Wakulima wote **wamekoboa** madeni yao.
7. Kazi ya kulima inahitaji bidii.
8. **Fyekeo** jipya limenunuliwa.
9. **Plau** inakokotwa na ng'ombe.
10. Mkulima analiendesha trekta polepole.

## Kipindi cha 5

Kazi ya wanafunzi wawili wawili

### Shabaha

Kufanya marudio ya Kipindi cha 4.

### Mbinu

Majadiliano ya wanafunzi wawili wawili.

### Mwenendo mwema

Kukuza moyo wa kushirikiana.

### Tathmini

Tathmini uwezo wa mwanafunzi wa kuzungumza kwa kujiamini huku akitumia lugha sahihi.

## Utaratibu

### *Hatua ya 1*

Wanafunzi wazungumzie waliyosoma katika kipindi cha awali.

### *Hatua ya 2*

Andaa wanafunzi kwa kazi ya wanafunzi wawili wawili (Kitabu cha Mwanafunzi, ukurasa wa 9).

### *Hatua ya 3*

Waongoze wanafunzi katika kujadiliana kuhusu shughuli za kilimo nchini Rwanda na faida zao. Wape wanafunzi hao fursa ya kuwasilisha hoja zao mbele ya darasa zima.

### Zoezi la ziada

1. Wanafunzi wataje tamaduni mbalimbali zinazohusiana na kilimo nchini Rwanda.
2. Wanafunzi wabuni vilabu vya wakulima chipukizi. Kila kikundi kipendekeze shughuli za kilimo ambazo watashiriki kwazo. Pia, wafanye utafiti ili waibuke na mbinu bora watakazotumia katika kufanikisha shughuli zao za kilimo.

3. Wanafunzi wazungumzie umuhimu wa kuheshimu kazi za watu hasa kilimo kwa kuwa hakuna kazi duni.
4. Wanafunzi wafanye mjadala kuhusu: mbinu za kilimo za kisasa ni bora kuliko mbinu za kilimo za jadi.

**Majibu ya zoezi la ziada**

1. Tamaduni zinazohusiana na kilimo ni kama vile ushirikiano katika shughuli mbalimbali za kilimo kama vile kuvuna, kupanda na kupalilia. Utamaduni mwingine ni wa kuombea mazao yaliyopandwa ili yanawiri.
2. Shughuli za kilimo ziwe kama vile ufugaji wa sungura, kilimo cha kabichi, kilimo cha karoti miongoni mwa shughuli nyingine. Utafiti udhihirishe jinsi kilimo walichokichagua wanafunzi hutekelezwa. Kwa mfano, kuoteza mbegu za kabichi na kuhamisha miche katika shamba lililoandaliwa.
3. Mazungumzo haya yanalenga kujenga maadili ya kuheshimu kazi za watu wengine. Mazungumzo yadhihirishe thamani na faida za kazi watakazozungumzia.
4. Mjadala uibue hoja kama vile: kilimo cha kisasa kimerahisishwa na ugunduzi wa sayansi na teknolojia, shughuli za kilimo cha kisasa hufanywa katika muda mfupi zikilinganishwa na shughuli za kilimo cha jadi.

## Kipindi cha 6 na 7

### Funzo

Msamiati wa shughuli za ufugaji nchini Rwanda

### Shabaha

Kufikia mwishoni mwa vipindi hivi, mwanafunzi aweze:

i) Kufahamu msamiati wa kutosha kuhusu shughuli za ufugaji nchini Rwanda,
ii) Kutumia vilivyo msamiati huo aliojifunza katika mawasiliano yake ya kila siku,
iii) Kuridhika na shughuli za ufugaji kama mojawapo ya njia za kupigana dhidi ya umaskini,
iv) Kuheshimu kazi ya watu wanaojishughulisha na ufugaji na tamaduni mbalimbali zinazohusiana na ufugaji,
v) Kufurahia na kujivunia utajiri utokeapo katika ufugaji,
vi) Kuwashauri wenzake kupata masomo ya kilimo na ufugaji kwa ajili ya manufaa ya jamii.

**Zana na vifaa muhimu kwa vipindi hivi**

i) Vifaa halisi: Hapa, wanafunzi wako watafaidika sana iwapo utawapeleka kuliko na vifaa na matendo yanayofunzwa hapa. Mathalan, wanafunzi wakipelekwa shambani watapata maneno kama mfugaji, fuga, wanyama, wadudu, mzinga,

nyuki, kata sufu, kama ng'ombe, pandisha mitamba, josho, atamisha, fuga ng'ombe ndani kwa ndani, kuchunga mifugo, safisha makao ya mifugo, tibu, na kadhalika.

ii) Kitabu cha Mwanafunzi

iii) Vifaa vya wanafunzi wenye mahitaji maalumu.

**Mbinu**

Mhadhara, kuwashirikisha wanafunzi kutembelea shamba la mfugaji.

## Kipindi cha 6

### Utaratibu

***Hatua ya 1***

Unaweza kulianza somo hili kwa kuwaongoza wanafunzi kukumbuka baadhi ya yale waliyojifunza katika kipindi cha awali.

***Hatua ya 2***

Ikiwa wanafunzi wamepelekwa kuliko msamiati wa kipindi hiki, mwalimu afunze maana ya mfugaji kwa kumwashiria mwenye shamba na kumweleza, kumtungia sentensi na kuwapa wanafunzi fursa ya kutunga sentensi zao. Fanya vivyo hivyo mpaka msamiati wote wa kimsingi kuhusu ufugaji utajwe.

***Hatua ya 3***

Waongoze wanafunzi kutazama michoro na kusoma vifungu vya maneno katika Kitabu cha Mwanafunzi.
Waelekeze wanafunzi kujibu maswali ya sehemu hii pamoja na mazoezi mengineyo. Unaweza kuwaongezea swali ama maswali kulingana na jinsi walivyo wanafunzi wako. Kwa mfano unaweza kuwapa swali la kuambatanisha kifaa na kazi yake.

***Hatua ya 4***

Waongoze wanafunzi katika kusahihisha majibu yao.

**Maadili na mwenendo mwema**

Kuheshimu kazi za watu wanaojishughulisha na ufugaji.

**Tathmini**

Tathmini uwezo wa mwanafunzi wa kujibu maswali kwa usahihi.

**Majibu ya maswali**

1. Wanafunzi waorodheshe majina ya mifugo yaliyomo kifunguni na uhakikishe kuwa umuhimu uliotajwa ni sahihi.

**Mifano ya majibu**

1. kondoo
2. ng'ombe
3. kuku
4. punda

2. Mwanafunzi aeleze vilivyo faida za shughuli za ufugaji alizosoma katika kifungu husika.

**Mifano ya majibu**

1. Kilimo cha ufugaji wa ng'ombe wa maziwa humpa mkulima maziwa ya kutumiwa nyumbani na pia mapato baada ya kuuza maziwa ya ziada.
2. Kilimo cha ufugaji wa kuku humpa mkulima mayai na nyama ya kuku. Anaweza kuuza mayai na kuuza kuku ili kujipatia mapato.
3. Kilimo cha nyuki huzalisha asali ambayo mkulima huuza na kupata mapato.
4. Mkulima huuza sufu ya kondoo na kupata faida.
5. Punda humsaidia mkulima kubeba mizigo.

3. a) rina
   b) kata sufu
   c) kama
   d) wanaoshwa
   e) lisha
   f) chunga
   g) anasafisha zizi
   h) anamtibu kuku

4. Mwanafunzi atunge sentensi sahihi akitumia hayo maneno aliyopewa. Arejelee mifano ya sentensi katika vifungu alivyosoma.

## Kipindi cha 7

### Funzo

Kazi ya wanafunzi wawili wawili na kikundi

### Shabaha

Kubainisha na kujadiliana kuhusu shughuli za ufugaji.

### Mbinu

Kuwashirikisha wanafunzi kufanya shughuli za wanafunzi wawili wawili na za vikundi.

## Utaratibu

***Hatua ya 1***

Wanafunzi wazungumzie waliyosoma katika kipindi cha awali. Waulize maswali kama vile: *Je, tulitaja majina ya mifugo gani? Je, ufugaji una faida gani*?

***Hatua ya 2***

Waongoze wanafunzi kufanya kazi ya wanafunzi wawili wawili kisha wafanye mjadala wa darasa zima.

Hakikisha kuwa wanafunzi wote wameshiriki na kuwa hoja zinazotolewa ni sahihi. Warekebishe panapohitajika.

**Maadili na mwenendo mwema**

Kuheshimu kazi za watu wanaojishughulisha na ufugaji.

**Tathmini**

Tathmini uwezo wa mwanafunzi wa kuzungumza kuhusu shughuli za ufugaji kwa kujiamini na kwa kutumia lugha sanifu.

**Zoezi la ziada**

1. Wanafunzi watoe sababu ya kufurahia na kujivunia ufugaji.
2. Wanafunzi wataje tamaduni mbalimbali zinazohusiana na ufugaji.
3. Katika vilabu vya wakulima chipukizi walivyobuni awali, kila kikundi kipendekeze shughuli za ufugaji ambazo watashiriki kwazo. Pia, wafanye utafiti ili waibuke na mbinu bora watakazotumia katika kufanikisha shughuli zao za ufugaji.

## Kipindi cha 8

**Funzo**

Majira ya mwaka nchini Rwanda **Shabaha**

Kufikia mwishoni mwa kipindi hiki, mwanafunzi aweze:

i) Kuyatambua majira ya mwaka nchini Rwanda.
ii) Kuutumia vilivyo msamiati husika katika mazingira yake popote pale.

**Zana na vifaa muhimu kwa kipindi hiki**

i) Michoro mbalimbali inayoonyesha misimu na shughuli mbalimbali zinazofanywa katika misimu hiyo
ii) Kitabu cha Mwanafunzi
iii) Vifaa vya wanafunzi wenye mahitaji maalumu.

**Mbinu**

Mhadhara na kuwashirikisha wanafunzi kujibu maswali darasani.

## Utaratibu

### *Hatua ya 1*

Unaweza kuianza sehemu hii kwa kuwauliza wanafunzi maswali kuhusu hali ya hewa ya siku hiyo na siku iliyopita.

Unaweza kuuliza maswali kama: *Je, huu ni msimu gani? Je, hapa tunavuna maharagwe mwezi gani? Mvua nyingi huwepo mnamo mwezi gani? Wakulima hufyeka mashamba yao lini? n.k.*

***Hatua ya 2***

Waongoze wanafunzi kufahamu maana ya neno majira au msimu.

***Hatua ya 3***

Igawe misimu katika migao yake mmoja mmoja huku ukiieleza. Kumbuka kuwa itafaa maelezo yako yakijihusisha sana na msamiati uliomo vitabuni mwa wanafunzi kama vile majira, misimu, hali ya hewa, masika, kulima, kupanda, kupaliliwa, stawisha, kuvuna, ardhi, vuli, kuza, kipupwe na kadhalika.

***Hatua ya 4***

Waongoze wanafunzi kuzungumzia michoro na kusoma kifungu cha habari kilichopo katika Kitabu cha Mwanafunzi. Katika kufanya hivyo, hakikisha ya kuwa umewahusisha wanafunzi wote huku ukiwajali wale ambao wana upungufu fulani fulani.

***Hatua ya 5***

Waelekeze wanafunzi kujibu maswali yaliyomo vitabuni mwao, ukurasa wa 13 halafu uwaongoze kufanya kazi ya wanafunzi wawili wawili.

**Tathmini**

Uwezo wa kutambua majira ya mwaka na kutumia msamiati wa majira katika mazingira mwafaka na kujibu maswali kwa usahihi.

**Zoezi la ziada**

Wanafunzi wataje mambo zaidi yanayofanyika katika majira mbalimbali nchini Rwanda.

**Majibu ya maswali** . Wanafunzi wajibu maswali haya kulingana na mazingira yao. **Mfano:**

a. Juni, Julai na Agosti. Majira ya kiangazi.
b. Juni, Julai na Agosti. Majira ya kiangazi.
c. Septemba, Oktoba na Novemba. Majira ya kipupwe.
d. Septemba, Oktoba na Novemba (Majira ya kipupwe) na Machi, Aprili na Mei (Majira ya masika).
e. Machi na Aprili katika majira ya masika.
   Septemba na Oktoba: Majira ya kipupwe.
f. Disemba, Januari na Februari. Majira vuli. Juni, Julai na Agosti majira ya kiangazi.
g. Machi, Aprili na Mei. Majira ya masika.

2. Vuli ni wakati ambapo zipo mvua ndogo ndogo lakini kipupwe ni msimu wenye baridi kali.
3. kiangazi, masika, kipupwe, vuli

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | K | | | | | E |
| | | I | | | | | W |
| | M | A | S | I | K | A | P |
| | | N | | L | | | U |
| | | G | | U | | | P |
| | | A | | V | | | I |
| | | Z | | | | | K |
| | | I | | | | | |

## Kipindi cha 9

### Funzo

Msamiati wa wanyama wa porini nchini Rwanda

### Shabaha

Kufikia mwishoni mwa kipindi hiki, mwanafunzi aweze:

i) Kuutambua msamiati wa wanyama wa porini nchini Rwanda.

ii) Kuutumia msamiati watakaojifunza kwa njia iliyo sahihi katika mawasiliano yake.

**Zana na vifaa muhimu kwa kipindi hiki**

i) Unaweza kutumia michoro na picha mbalimbali za wanyama wa porini. Kwa kuwa wanyama hawa hawawezi kuletwa darasani, ni vizuri ufanye mipango ya kuwapeleka wanafunzi wako kuliko na mbuga ya wanyama ambapo wanaweza kuona aina nyingi za wanyama.

ii) Kitabu cha Mwanafunzi

iii) Vifaa vya wanafunzi wenye mahitaji maalumu.

### Mbinu

Kuwashirikisha wanafunzi kuzungumza kuhusu wanyama wa porini wanaopatikana nchini Rwanda, kusoma kifungu na kujibu maswali kwa usahihi.

## Utaratibu

### *Hatua ya 1*

Ikiwa unatumia picha ama michoro, tumia mbinu ya kawaida ya kuwaonyesha wanafunzi picha husika. Tamka jina ama neno lake huku wanafunzi wakikuiga.

### *Hatua ya 2*

Waelekeze wanafunzi kutunga sentensi zao wakitumia msamiati uliowapa. Fanya vivi hivi hadi msamiati ulionuia kuufunza umekwisha.

***Hatua ya 3***

Waongoze wanafunzi kukisoma kifungu kilichopo katika Kitabu cha Mwanafunzi. Pale ambapo wanahitajika kuzungumzia jambo fulani kama vile kuwatambulisha wanyama na kueleza wanakopatikana, endelea kuwaongoza kufanya hivyo.

***Hatua ya 4***

Waelekeze wanafunzi kujibu maswali ya sehemu hii yaliyomo vitabuni mwao halafu uwaongoze kusahihisha majibu yao.

Kumbuka hapa kwamba unaweza kubadilisha badilisha mtindo wa kusahihisha. Mara hii unaweza kutumia mtindo wa kila mwanafunzi kujisahihishia kazi yake ambayo utaipitia kuhakikisha ya kuwa alisahihisha vilivyo. Pia, wanaweza kubadilishana vitabu na wasahihishe. Ama unaweza kukusanya vitabu vyao ukaenda ukavisahihisha. Mwishoni ni sharti uipitie kazi hiyo ya wanafunzi.

**Masuala mtambuka**

Kuthamini utunzaji mazingira.

**Tathmini**

Uwezo wa kubainisha wanyama wa porini wanaopatikana nchini Rwanda na kutumia msamiati wa wanyama wa porini katika mazingira mwafaka na kujibu maswali kwa usahihi.

**Zoezi la ziada**

Wanafunzi wataje wanyama mbalimbali wa porini ambao hawakutajwa katika kitabu chao na darasani.

**Majibu ya maswali**

1. a) Mwanafunzi ajibu ihitajikanavyo. Mfano: simba, chui, fisi.
   b)Mwanafunzi ajibu ihitajikanavyo. Mfano: ndovu, nyati, pundamilia.
2. Nyani ana ngoko ilhali sokwe hana/Sokwe ana akili kubwa kuliko nyani/ Sokwe hana mkia ilhali nyani anao.
3. a) fisi b) ndovu c) nyani d) tembo e) pundamilia
4. Mwanafunzi ajibu ihitajikanavyo.
5. a) nyati b) ndovu/tembo c) kifaru d) simba e) duma
6. Ongoza utafiti huu.

## Kipindi cha 10

**Funzo**

Umuhimu wa wanyama wa porini nchini Rwanda (Kitabu cha Mwanafunzi, ukurasa wa 18)

**Shabaha**

Kufikia mwishoni mwa kipindi hiki, mwanafunzi aweze:

i) Kuutambua umuhimu wa wanyama wa porini nchini Rwanda na kuweza kuwathamini wanyama hao.

ii) Kuyatumia waliyojifunza katika mawasiliano yao ya kila siku.

**Zana na vifaa muhimu kwa kipindi hiki**

i) Hapa, itabidi utumie michoro sana sana. Michoro hiyo inaweza kuwa ya pesa za kigeni, ustawi wa uchumi, watalii wakinunua bidhaa za hapa kwetu, kundi la wanafunzi wakitazama wanyama kwa uongozi wa mwalimu wao na kadhalika.

ii) Kitabu cha Mwanafunzi

iii) Vifaa vya wanafunzi wenye mahitaji maalumu.

**Mbinu**

Mhadhara, kuwashirikisha wanafunzi kuzungumza kuhusu mada na kusoma maelezo ya Kitabu cha Mwanafunzi na kujibu maswali.

## Utaratibu

***Hatua ya 1***

Unaweza kuanza kwa kuwauliza wanafunzi maswali kuhusu yale waliyojifunza katika kipindi kilichopita. Halafu kwa kuwaongoza vilivyo na kwa michoro na maelezo yako kwa njia ya maswali, wafunze malengo ya sehemu hii.

Unaweza kuuonyesha mchoro na uwaulize jina la mnyama wanayemwona na halafu uwaongoze kugundua umuhimu wa mnyama huyo. Wakigundua umuhimu huo kwa mchoro wa kwanza, itakuwa rahisi kwao kueleza matumizi mengineyo.

***Hatua ya 2***

Imarisha yale uliyofunza kwa kuwaongoza wanafunzi kuisoma sehemu hii iliyomo vitabuni mwao.

Kumbuka kuwashirikisha wanafunzi wote na wala usiwaruhusu wanafunzi wale wale kujibu kila swali linaloulizwa.

***Hatua ya 3***

Waelekeze wanafunzi kusoma kifungu kilichopo katika Kitabu cha Mwanafunzi, ukurasa wa 18 na kujibu maswali yaliyouliziwa chini yake. Baada ya hayo, wanafunzi wafanye kazi ya kikundi.

**Mwenendo mwema**

Kuthamini utunzaji mazingira.

**Tathmini**

Tathmini uwezo wa mwanafunzi wa kuzungumza kuhusu umuhimu wa wanyama wa porini, kusoma na kujibu maswali kwa usahihi.

**Zoezi la ziada**

Waulize wanafunzi maswali haya:

i) Nini maana ya jangili?
ii) Je, kuna majangili hapa Rwanda?
iii) Majangili hupata wapi soko lao?
iv) Ni wizara gani katika serikali yetu ambayo inahusika na wanyama wa porini?
v) Eleza jinsi hela zinazotokana na wanyama wa porini zinavyowafaidi wanakijiji wako.

**Majibu ya maswali**

1. - Kuleta fedha za kigeni kwa kuvutia watalii/kuletea nchi mapato
   - Hunufaisha vizazi vijavyo
   - Watu hujifunza mengi kuhusu wanyama hao wanapowaona

   (Kubali majibu mengineyo ambayo ni sahihi)
2. Kupitia mbuga zilizotengewa wanyama. Kupitisha sheria kali dhidi ya wanaowinda wanyama wa porini. Kuwepo kwa askari wanaolinda mbuga mbalimbali za wanyama.

## Kipindi cha 11 na 12

### Funzo

Nomino

### Shabaha

Kufikia mwishoni mwa vipindi hivi, mwanafunzi aweze:

i) Kueleza waziwazi maana ya nomino.
ii) Kuainisha nomino mbalimbali.
iii) Kutumia kwa njia iliyo sahihi nomino yoyote ile.

**Zana na vifaa muhimu kwa vipindi hivi**

i) Mifano mingi ya nomino utakayotumia hapa ni ya majina yanayoweza kuchoreka ama kupigwa picha ama kuletwa darasani kama kifaa halisi. Lakini majina mengine ni muhali kuchora, kupiga picha ama kuleta darasani. Kwa mfano, nomino wema ni jina ama nomino ya dhahania. Utakapokuwa unayafunza haya, utategemea sana maelezo.
ii) Kitabu cha Mwanafunzi
iii) Vifaa vya wanafunzi wenye mahitaji maalumu.

### Mbinu

Mhadhara huku michoro ya nomino na vitu halisi vikitumiwa.

## Kipindi cha 11

### Funzo

Nomino za pekee, za kawaida na za jamii

### Utaratibu

***Hatua ya 1***

Tanguliza kipindi hiki kwa kuwaeleza wanafunzi maana ya nomino kwa kutumia vifaa vilivyomo darasani na nje ya darasa. Ni baada tu ya kuhakikisha kuwa wanaelewa nomino ni nini ambapo utaanza kufunza namna au aina zake.

***Hatua ya 2***

Kwa kutumia vifaa mbalimbali, funza nomino za pekee, za kawaida na za jamii. Sehemu ya vifaa vya majina ya pekee ni majina ya wanafunzi darasani. Navyo vya majina ya kawaida pia vinaweza kuwa vitu darasani.

Unaweza kuyafunza haya na mengineyo kwa kutumia mbinu ya kawaida ya kufunza msamiati kwa njia ya maswali.

Hali kadhalika unapokuwa unafunza, ni sharti uendelee kuwatathmini wanafunzi wako iwapo wanakuelewa ama la. Hili unalitekeleza hatua kwa hatua na kwa njia ya maswali.

Isitoshe, ni sharti kila nomino inayofunzwa itungiwe sentensi kudhihirisha matumizi yake.

***Hatua ya 3***

Kama ulivyofanya katika hatua iliyopita, waongoze wanafunzi kujua aina na matumizi ya nomino mbalimbali zilizotajwa.

***Hatua ya 4***

Waongoze wanafunzi wako katika kusoma maana na mifano mbalimbali ya nomino katika Kitabu cha Mwanafunzi. Kama ilivyo kawaida, hakikisha kuwa wanafunzi wote wameshiriki na kwamba wale wenye upungufu fulani wanashughulikiwa ipasavyo.

***Hatua ya 5***

Waongoze wanafunzi kufanya mazoezi ya kila sehemu pamoja na kujibu maswali ya sehemu hii.

### Tathmini

Kufanya mazoezi yaliyomo katika Kitabu cha Mwanafunzi kwa usahihi.

### Kipindi cha 12

**Funzo**

Nomino za dhahania na wingi

**Shabaha**

Mwanafunzi aweze kubainisha nomino za dhahania na kutumia nomino katika sentensi kwa usahihi.

**Mbinu**

Mhadhara na kuwashirikisha wanafunzi katika kujibu maswali ya darasani.

### Utaratibu

***Hatua ya 1***

Wanafunzi wazungumzie na wakumbushane waliyosoma katika kipindi kilichotangulia.

***Hatua ya 2***

Kwa kutumia vifaa mbalimbali, funza nomino za dhahania na wingi.

Unaweza kuyafunza haya na mengineyo kwa kutumia mbinu ya kawaida ya kufunza msamiati kwa njia ya maswali.

Hali kadhalika unapokuwa unafunza, ni sharti uendelee kuwatathmini wanafunzi wako iwapo wanakuelewa ama la. Hili unalitekeleza hatua kwa hatua na kwa njia ya maswali.

Isitoshe, ni sharti kila nomino inayofunzwa itungiwe sentensi kudhihirisha matumizi yake.

***Hatua ya 3***

Kama ulivyofanya katika hatua iliyopita, waongoze wanafunzi kujua aina na matumizi ya nomino mbalimbali.

***Hatua ya 4***

Waongoze wanafunzi wako katika kusoma maana na mifano mbalimbali ya nomino katika Kitabu cha Mwanafunzi. Kama ilivyo kawaida, hakikisha kuwa wanafunzi wote wameshiriki na kwamba wale wenye upungufu fulani wanashughulikiwa ipasavyo.

***Hatua ya 5***

Waongoze wanafunzi kufanya mazoezi ya kila sehemu pamoja na kujibu maswali ya sehemu hii.

**Tathmini**

Kufanya mazoezi yaliyomo katika Kitabu cha Mwanafunzi kwa usahihi.

**Zoezi la ziada**

Unaweza pia kuwauliza wanafunzi maswali kama vile:

1. Je, nomino ni nini?
2. Utaelezaje nomino ya wingi?
3. Kuna tofauti gani kati ya nomino ya wingi na ile ya kawaida?
4. Majina ya jamii ni majina ya aina gani?
5. Nomino ya dhahania hutofautianaje na nomino nyinginezo?

**Majibu ya zoezi**

| | |
|---|---|
| Nomino za pekee | Rwanda, Mwenyezi Mungu |
| Nomino za kawaida | kazi, wanyama, ndege, wadudu, ng'ombe, mbuzi, kondoo, farasi, nguruwe, ndege, kuku, bata, nyuki, mfugaji, njia, ng'ombe wa gredi |
| Nomino za wingi | mazingira, mifugo, maziwa, chumvi, sukari |
| Nomino za dhahania | ufugaji, matokeo, mapato, magonjwa, umaskini |
| Nomino za jamii | chane za ndizi |

## Kipindi cha 13 na 14

### Funzo

Vivumishi

### Shabaha

Kufikia mwishoni mwa vipindi hivi, mwanafunzi aweze:

i) Kueleza waziwazi maana ya vivumishi.
ii) Kuainisha vivumishi mbalimbali.
iii) Kutumia kwa njia iliyo sahihi vivumishi vyovyote vile.

**Zana na vifaa muhimu kwa vipindi hivi**

i) Unaweza kutumia michoro japo baadhi ya vivumishi kama vile bora vitahitaji maelezo pekee.
ii) Kitabu cha Mwanafunzi
iii) Vifaa vya wanafunzi wenye mahitaji maalumu.

### Mbinu

Mhadhara na kuwashirikisha wanafunzi kujibu maswali ya darasani.

## Kipindi cha 13

### Funzo

Vivumishi vya sifa, vya pekee na vionyeshi

## Utaratibu

### *Hatua ya 1*

Unaweza kulianza somo hili kwa kuwauliza wanafunzi maswali yanayolenga marudio ya maana na matumizi ya baadhi ya vivumishi walivyojifunza hapo awali.

Halafu kwa kutumia vifaa ulivyotayarisha, funza vivumishi vya sifa, vya pekee na vionyeshi.

### *Hatua ya 2*

Waongoze wanafunzi kuisoma sehemu hii iliyomo vitabuni mwao. Hakikisha ya kuwa wanafunzi wote wanashiriki katika kusoma huko.

### *Hatua ya 3*

Waongoze wanafunzi kujibu maswali kutoka kila sehemu uliyoifunza.

## Tathmini

Kufanya mazoezi yaliyomo katika Kitabu cha Mwanafunzi kwa usahihi.

**Majibu ya mazoezi**

**Zoezi**

a) Hakikisha kuwa kivumishi kinajitokeza baada ya nomino na kwamba kinazingatia ngeli ya nomino.

b) Hakikisha kuwa kivumishi kinajitokeza baada ya nomino na kwamba kinazingatia viambishi sahihi vya ngeli ya nomino husika.

c) i) Tupe ndizi chache. ii) Mihindi mirefu inafaa. iii) Farasi mkubwa atanibeba.
iv) Mazizi safi hayaleti magonjwa. v) Upanzi bora ni huu.
vi) Wakulima nadhifu wanapita.

d) Wanafunzi warejelee vifungu vinavyohusu wanyama wa porini na kilimo walivyosoma katika Kitabu cha Mwanafunzi.

**Zoezi**

i) Kila sehemu
ii) Kila kitu
iii) Kila kitu
iv) Kila kitu
v) Kila kitu

**Zoezi (chini ya o-ote)**

1. lolote
2. yote
3. wote
4. lolote
5. zote

**Zoezi**

a) 1. mengine 2. linginelo/jinginelo 3. nyinginezo
4. wengine 5. mingineyo

b) Wanafunzi waige mifano iliyotolewa katika Kitabu cha Mwanafunzi na watunge sentensi sahihi. Ifuatayo ni mifano ya sentensi:
Umoja: Sikuuzii farasi huyu, nitakuuzia farasi mwingine.
Wingi: Hatuwauzii farasi hawa, tutawauzia farasi wengine.

c) Wanafunzi waige. mifano iliyotolewa katika Kitabu cha Mwanafunzi na watunge sentensi sahihi. Ifuatayo ni mifano ya sentensi:
Umoja: Mlishe punda huyo na mwingineye.
Wingi: Walishe punda hao na wengineo.

**Zoezi**

1. yaya haya 2. yule 3. hao hao 4. hii

5. a) hao
b) Mifano ya sentensi
i) umoja: Mkulima huyu ni hodari.
wingi: Wakulima hawa ni hodari.
ii) umoja: Mkulima huyu huyu alipewa tuzo.
wingi: Wakulima hawa hawa walipewa tuzo.
iii) umoja: Mkulima yuyu huyu alipanda mbegu.
wingi: Wakulima wawa hawa walipanda mbegu.

## Kipindi cha 14

### Funzo

Vivumishi vya idadi, viulizi na vimilikishi

### Shabaha

Mwanafunzi aweze kubainisha vivumishi vya idadi, viulizi na vimilikishi na kutumia vivumishi hivyo katika sentensi kwa usahihi.

### Mbinu

Mhadhara na kuwashirikisha wanafunzi kujibu maswali ya darasani.

### *Hatua ya 1*

Unaweza kulianza somo hili kwa kuwauliza wanafunzi maswali kutokana na kipindi cha awali.

Halafu kwa kutumia vifaa ulivyotayarisha, funza vivumishi vya idadi, viulizi na vimilikishi.

***Hatua ya 2***

Waongoze wanafunzi kuisoma sehemu hii iliyomo vitabuni mwao. Hakikisha ya kuwa wanafunzi wote wanashiriki katika kusoma huko.

***Hatua ya 3***

Waongoze wanafunzi kujibu maswali kutoka kila sehemu uliyoifunza.

Wanafunzi waonyeshe kuwa wameelewa vivumishi mbalimbali kwa kuvitungia sentensi zilizo sahihi.

***Hatua ya 4***

Limalizie somo lako kwa kuwaongoza wanafunzi kuunda muhtasari wa yote waliyosoma. Jambo hili litekelezwe kwa njia ya kuuliza maswali.

**Tathmini**

Kufanya mazoezi yaliyomo katika Kitabu cha Mwanafunzi kwa usahihi.

**Majibu ya mazoezi**

**Zoezi**

a) i) wachache ii) sita iii) mmoja iv) mengi
v). manane

b) Mifano ya sentensi:
i) Kondoo kumi wanafugwa.
ii) Ng'ombe wengi wamenunuliwa.

**Zoezi**

a) 1. yapi 2. upi 3. zipi 4. wapi 5. kupi

b) 1. mangapi 2. ngapi 3. wangapi 4. mingapi 5. vingapi

**Zoezi**

1. yenu 2. yetu 3. zao 4. yangu

5. lake 6. wako

**Zoezi** 1.

| | |
|---|---|
| Vivumishi vya sifa | nzuri, mema, bora, ndogondogo, kubwa, vikali, mbaya, mazuri, kizuri |
| Vivumishi vya pekee | mwenye, vyote |
| Vivumishi vya idadi | moja, wengi, mbili |
| Vivumishi vionyeshi | yaya haya |
| Vivumishivimilikishi | mwangu, langu |

2. Mifano ya sentensi

   a) Mbegu nzuri zimepandwa shambani.

   b) Mkulima mwenye bidii ametuzwa.

   c) Ndama wawili wamenyweshwa maziwa.

   d) Ng'ombe huyu hutoa maziwa mengi.

   e) Shamba langu lina miti mirefu.

## Kipindi cha 15

### Funzo

Viwakilishi

### Shabaha

Kufikia mwishoni mwa kipindi hiki, mwanafunzi aweze:

i) Kueleza waziwazi maana ya viwakilishi.
ii) Kuainisha viwakilishi tofauti tofauti.
iii) Kutumia kwa njia iliyo sahihi viwakilishi vya kila namna.

### Zana na vifaa muhimu kwa kipindi hiki

i) Unaweza kuwatumia wanafunzi wa humo darasani pamoja na vifaa vinginevyo vipatikanavyo darasani kufunza viwakilishi ama vibadala vya sehemu hii.
ii) Kitabu cha Mwanafunzi
iii) Vifaa vya wanafunzi wenye mahitaji maalumu.

### Mbinu

Mhadhara na kuwashirikisha wanafunzi kujibu maswali ya darasani.

## Utaratibu

### *Hatua ya 1*

Anza kwa kueleza maana ya neno kiwakilishi. Unaweza kulitekeleza hili kwa kuwatumia wanafunzi kadhaa.

Baada ya hayo, funza viwakilishi huru. Unaweza kumwelekeza mwanafunzi mmoja atunge sentensi akitumia neno *mimi*. Halafu akiwa na mwenzake watumie neno *sisi*. Fanya vivyo hivyo hadi uvimalize.

Utakapofikia viwakilishi viambata, mtindo utakuwa ule ule. Lakini kwa vingine, utashurutika kutumia vifaa ulivyovitayarisha.

***Hatua ya 2***

Waongoze wanafunzi kusoma vifungu chini ya viwakilishi kwa minajili ya kuimarisha uwelewa wa yale uliyofunza hapo juu.

***Hatua ya 3***

Waongoze wanafunzi wajibu, hatua kwa hatua, mazoezi yote ya sehemu hii. Ikiwa watayajibu kwa kuzungumza masahihisho yafanywe pale kwa pale. Lakini ikiwa ni kwa kuandika, masahihisho yafanywe kulingana na mbinu iliyotumika lakini ni sharti uyapitie madaftari yao.

***Hatua ya 4***

Waongoze wanafunzi kuzungumzia yale muhimu waliyojifunza katika sehemu hii ya viwakilishi.

**Tathmini**

Kufanya mazoezi yaliyomo katika Kitabu cha Mwanafunzi kwa usahihi.

**Zoei la ziada**

Unaweza kuwauliza maswali ya tathmini kama vile:

1. Kwa maneno yako mwenyewe, kieleze kiwakilishi.
2. Viwakilishi huru vinatofautianaje na viwakilishi ambata?
3. Viwakilishi vionyeshi huashiria kilipo kitu. Usemi huu si sawa? Eleza.
4. Viwakilishi vionyeshi ni vya ujirani wa karibu, mbali kidogo na halafu ujirani wa mbali. Lieleze jambo hili kwa mifano miwili.
5. Pana tofauti gani kati ya viwakilishi viulizi na viwakilishi vimilikishi?

**Majibu ya zoezi**

**Zoezi A.**

Mifano ya sentensi

1. Mimi napenda kilimo.
2. Huyo ndiye mwenye shamba kubwa.
3. Wangapi wanapenda ufugaji?
4. Langu lina miti mirefu.

**Zoezi B.**

**Majibu ya zoezi la kifungu**

1. Fisi alikuwa mnyama mvivu aliyependa vya bwerere.
2. Kwa sababu fisi hakupenda kulima na alikula sana.
3. Alimkomesha fisi kwa kumjazia pilipili katika chakula alichompa.
4. Mfano: Nadhani baada ya kula chakula chenye pilipili, fisi alikoma kwenda kwa binadamu.

5. Mifano ya sentensi
    1. Huyu hapendi kufanya kazi, anapenda tu kula.
    2. Alidhani kuwa huyo binadamu naye alimpenda.
    3. Mbona hiki cha leo ni kikali jinsi hii?

## Kipindi cha 16

### Funzo

Vielezi

### Shabaha

Kufikia mwishoni mwa kipindi hiki, mwanafunzi aweze:
i) Kueleza waziwazi maana ya vielezi.
ii) Kuainisha vielezi.
iii) Kutumia kwa njia iliyo sahihi vielezi vilivyofunzwa.

**Zana na vifaa muhimu kwa kipindi hiki**

i) Unaweza kutumia michoro na vifaa halisi kufunzia somo hili. Mathalan, unaweza kuwa na picha ama mchoro wenye watu wengi kisha ukawa na mwingine wenye watu wengi zaidi. Hapo utaweza kufunza dhana ya kielezi *sana* au *zaidi*.
ii) Kitabu cha Mwanafunzi
iii) Vifaa vya wanafunzi wenye mahitaji maalumu.

### Mbinu

Mhadhara na kuwashirikisha wanafunzi kujibu maswali ya darasani.

## Utaratibu

### *Hatua ya 1*

Lianze somo hili kwa kurudia baadhi ya yale uliyofunza katika somo lililopita kabla ya kuwaongoza wanafunzi kujua maana ya kielezi.

Baada ya hayo, waongoze wanafunzi kujua maana na matumizi ya vielezi vya namna pamoja na vielezi vya wakati.

Iwapo una wanafunzi wenye upungufu fulani fulani, hakikisha kuwa kila unapofunza lolote darasani unawaongoza ili wawe na wenzao pamoja.

### *Hatua ya 2*

Kwa mbinu zizo hizo, waongoze wanafunzi wote kujua maana na matumizi ya vielezi mbalimbali vilivyotajwa.

### *Hatua ya 3*

Waongoze wanafunzi kusoma vifungu chini ya vielezi, Kitabu cha Mwanafunzi

Kama ilivyo kawaida, washirikishe wanafunzi wote katika kusoma huko.

***Hatua ya 4***

Waelekeze wanafunzi kujibu maswali yaliyomo vitabuni mwao. Ni sharti wanafunzi waonyeshe kuelewa waliyofunzwa kwa namna wanavyojibu maswali hayo. Iwapo pana wanafunzi ambao wanaonekana kuwa hawakuelewa vilivyo, ni sharti utenge wakati wa kuwaongoza ili wafikie kiwango kile kile cha wenzao.

***Hatua ya 5***

Wanafunzi waongozwe kuunda muhtasari wa yale waliyoyasoma katika sehemu hii na kuyaandika madaftarini mwao.

**Tathmini**

Kufanya mazoezi yaliyomo katika Kitabu cha Mwanafunzi kwa usahihi.

**Majibu ya zoezi**

Gakwerere alikuwa mfugaji mwenye bidii nyingi **sana** tangu **zamani**. Mwanzoni, Gakwerere alikuwa akifuga ng'ombe wa kienyeji. Aliwalisha ng'ombe hao **uwanjani** na **pembeni mwa** mashamba. Hata hivyo, ng'ombe hao hawakuwa wakimpa kiasi cha maziwa alichotarajia. Angewakamua **mara moja tu kwa siku**. Alikata shauri kuanzisha ufugaji wa ng'ombe wa gredi.

Mfugaji huyu aliwapeleka ng'ombe wake wa kienyeji **sokoni** na kuwauza **mnamo Novemba**. Baada ya kuwauza, aliamka **alfajiri** na kufunga safari ya kuzuru shamba la kisasa la Nyinawumuntu. Bi Nyinawumuntu alikuwa mfugaji na mkulima mashuhuri sana katika eneo hilo alilokaa Gakwerere. Alipofika huko, alimpata bibiye yupo na wakaanza kupiga bei. Baada ya kukubaliana bei, alinunua mitamba wawili **kwa bei nafuu**. Alilipa papo hapo kwa sababu hakutaka kuwa na deni.

Kumaliza hivi tu, yule bibi alimpa Gakwerere gari lake ili alitumie kuwasafirisha ng'ombe wake. Gakwere alimshukuru kwa wema wake na akawasafirisha hao mitamba wake hadi kwake.

Alipofika nyumbani kwake, mfugaji huyo alianza kuwalisha ng'ombe wake **kwa njia za kisasa**. Kwa kuwa walikuwa wakilishwa **kwa lishe bora ya ng'ombe**, hakuchukua muda mrefu kuwapandisha. Muda ulipowadia, walizaa ndama wawili wenye afya nzuri.

Baada ya muda usio mrefu, Gakwerere alianza kuvuna matokeo ya jasho lake la kila siku. Hakuamini kiasi cha maziwa alichokuwa akikama **kila asubuhi na jioni**.

Aliweka akiba **kwa muda**. Hatimaye, mfugaji huyu alinunua gari. Alitumia gari hilo kuwatafutia na kuwabebea chakula ng'ombe hao wake wa gredi.

Hakikisha kuwa sentensi zilizotungwa ni sahihi.

## Kipindi cha 17

### Funzo

Matumizi ya wakati uliopo -na- na vitenzi vya silabi moja (hali yakinishi na kanushi).

### Shabaha

Kufikia mwishoni mwa kipindi hiki, mwanafunzi aweze:

i) Kuvitambua na kuvitumia vilivyo vitenzi vyenye silabi moja.
ii) Kutumia kwa njia iliyo sahihi wakati uliopo -na-.
iii) Kutunga sentensi sahihi za hali yakinishi na kanushi akitumia wakati uliopo -na-.

### Zana na vifaa muhimu kwa kipindi hiki

i) Unaweza kutumia vitendo vya wanafunzi unapokuwa unafunza funzo hili, kwa mfano: mwanafunzi ale au asile  na kadhalika.
ii) Kitabu cha Mwanafunzi
iii) Vifaa vya wanafunzi wenye mahitaji maalumu.

### Mbinu

Mhadhara na kuwashirikisha wanafunzi kutenda vitendo mbalimbali na kujibu maswali ya darasani.

## Utaratibu

### *Hatua ya 1*

Unaweza kulianza somo lako kwa kurudia yale waliyofunzwa katika kipindi kilichopita.

Kwisha hili, unaweza kuwaeleza maana ya wakati kwa kuwauliza wataje na kuzitungia sentensi nyakati za Kinyarwanda. Wakimaliza hilo na uone kabisa kuwa wameelewa maana ya wakati, chagua wakati uliopo na uanze kuufunza kwa kuulinganisha na huo wa kienyeji.

### *Hatua ya 2*

Kwa mbinu hiyo hiyo, waongoze wanafunzi kutaja vitenzi vichache vya silabi moja vya lugha yao ya mama. Waelekeze kutunga sentensi chache kwa maneno hayo kabla ya kuwaongoza kutaja vitenzi kama hivyo lakini vya Kiswahili huku wakivitungia sentensi.

Kumbuka hapa ya kuwa mbinu hii itakufaa sana iwapo darasa lako ni la wanafunzi wa Kinyarwanda pekee. Akiwemo mwingine ambaye haielewi lugha hiyo itabidi utumie mbinu tofauti.

***Hatua ya 3***

Sasa waongoze wanafunzi kutunga sentensi wakitumia kiambishi -na- ulichofunza katika hatua 1 wakitumia vitenzi vya silabi moja ambavyo umevifunza katika hatua 2 hapo juu.

***Hatua ya 4***

Waongoze wanafunzi kukumbuka hali yakinishi na hali kanushi. Unaweza kutumia vitendo vya hapo darasani kama vile: Ninaandika ubaoni na Siandiki ubaoni.

Baada ya hapo, waongoze wanafunzi kutunga sentensi zaidi za hali hizi mbili lakini wakitumia wakati uliopo pamoja na vitenzi vya silabi moja.

***Hatua ya 5***

Waongoze wanafunzi kusoma sehemu hii iliyomo vitabuni mwao na uwaelekeze kufanya kazi ya wanafunzi wawili wawili.

**Maadili na mwenendo mwema**

Kukuza moyo wa ushirikiano.

**Tathmini**

Kufanya mazoezi yaliyomo katika Kitabu cha Mwanafunzi kwa usahihi.

Hakikisha kuwa majibu au hoja wanazotaja wanafunzi ni sahihi.

## Kipindi cha 18

**Funzo**

Matumizi ya wakati uliopita -li- na vitenzi vya silabi moja (hali yakinishi na kanushi).

(Kitabu cha Mwanafunzi, ukurasa wa 40)

**Shabaha**

Kufikia mwishoni mwa kipindi hiki, mwanafunzi aweze:

i) Kuvitambua na kuvitumia vilivyo vitenzi vya silabi moja.
ii) Kutumia kwa njia iliyo sahihi wakati uliopita -li-.
iii) Kutunga sentensi sahihi za hali yakinishi na kanushi akitumia wakati uliopita -li-.

**Zana na vifaa muhimu kwa kipindi hiki**

i) Matumizi ya vitendo mbalimbali darasani
ii) Kitabu cha Mwanafunzi
iii) Vifaa vya wanafunzi wenye mahitaji maalumu.

**Mbinu**

Mhadhara na kuwashirikisha wanafunzi kutenda vitendo mbalimbali na kujibu maswali ya darasani.

## Utaratibu

### *Hatua ya 1*

Lianze somo lako kwa kurudia yale waliyofunzwa katika kipindi kilichopita.

Waongoze wanafunzi kukumbuka nyakati za kikwao kabla ya kufunza wakati uliopita kwa kuufananisha na ule wa kikwao.

### *Hatua ya 2*

Waongoze wanafunzi kutaja vitenzi vyote vya silabi moja walivyovitumia katika kipindi kilichopita. Halafu wataje vingine zaidi ambavyo havikutumika katika kipindi kilichopita huku wakivitungia sentensi.

### *Hatua ya 3*

Sasa waongoze kutunga sentensi wakitumia wakati uliopita -li- pamoja na vitenzi vya silabi moja vikiwa pamoja na vile walivyovitaja katika hatua ya pili hapo juu. Ni sharti sentensi hizo ziwe katika hali yakinishi na hali kanushi. Kila sentensi inayotungwa ni sharti ifanyiwe ukanusho wake kabla ya kutungwa inayofuata.

### *Hatua ya 4*

Waelekeze wanafunzi kuisoma sehemu hii iliyomo vitabuni mwao (ukurasa wa 40) halafu uwaongoze kuifanya kazi ya vikundi inayohusika na sehemu hiyo pamoja na kuisahihisha.

### Maadili na mwenendo mwema

Kukuza moyo wa ushirikiano.

### Tathmini

Kufanya mazoezi yaliyomo katika Kitabu cha Mwanafunzi kwa usahihi.

## Kipindi cha 19

### Funzo

Ufupisho wa mambo yote yaliyofunzwa na kusomwa katika sura hii.

### Shabaha

Kufikia mwishoni mwa kipindi hiki, mwanafunzi aweze:

i) Kukumbuka mambo muhimu yaliyofunzwa katika sura hii ya kwanza.
ii) Kuyatumia kwa ufasaha mambo hayo katika mawasiliano yao ya kila siku.

### Zana na vifaa muhimu kwa kipindi hiki

Kitabu cha Mwanafunzi

### Mbinu

Kuwauliza mwanafunzi maswali kutoka masomo ya Sura ya Kwanza huku akiyajibu kwa usahihi.

## Utaratibu

***Hatua ya 1***

Rejelea yale yote yaliyofunzwa katika sura hii. Kwa mfano, chukua kipindi cha kwanza na ukiulizie maswali ya kuwakumbusha wanafunzi yale waliyojifunza pale. Unaweza kuuliza maswali kama vile:

1. Taja mazao manne yakuzwayo sana hapa kwetu.
2. Ni shughuli gani za kilimo zitekelezwazo hapa Rwanda?
3. Yaeleze maneno haya ya ufugaji: kuatamisha, kulisha mifugo, kurina, kukata pembe, kukama na kadhalika.
4. Kuna majira gani ya mwaka hapa kwetu Rwanda na majira hayo huhusikaje na ukulima wetu?
5. Ni mnyama gani aliye mkubwa kushinda wote porini?

***Hatua ya 2***

Kwa mbinu hii hii ya marudio kwa maswali, waulize wanafunzi maswali zaidi ya kutathmini ujuzi waliopata.

**Tathmini**

Tathmini stadi na ujuzi wa masomo ya Sura ya Kwanza.

## Kipindi cha 20

**Funzo**

Maswali ya marudio (Kitabu cha Mwanafunzi,

**Shabaha**

Kufikia mwishoni mwa kipindi hiki, mwanafunzi aweze:

Kujitathmini na kuona kama ameyaelewa vilivyo yote aliyofunzwa katika sehemu hii.

**Zana na vifaa muhimu kwa kipindi hiki**

i) Kitabu cha Mwanafunzi.

**Mbinu**

Kujibu maswali ya marudio madaftarini na baadaye kusahihisha majibu ya mwanafunzi.

## Utaratibu

***Hatua ya 1***

Baada ya kuwapongeza wanafunzi na kuwatia ari ya kujibu mawali ya sehemu hii, waelekeze wanafunzi kujibu mawali ya sehemu hii.

***Hatua ya 2***

Waongoze wanafunzi kusahihisha majibu yao ya sehemu hii.

**Tathmini**

Tathmini uwezo wa mwanafunzi wa kujibu maswali ya marudio.

**Majibu ya marudio**

1. Mifano ya mazao: muhogo, papai, shamba, mharagwe, mtama, fyekeo, mkulima, embe, mkahawa, majani ya mchai
   Mifano ya ufugaji: kuku, kondoo, ng'ombe, nguruwe, punda, ndama, maziwa, mayai, zizi, malisho
2. Masika – kulima, kupanda na kupalilia
   Kiangazi – kuvuna
   Kipupwe – kupanda/kupalilia/kulima
3. a) masika b) kiangazi c) kipupwe
4. Mifano ya sentensi
   a) Mahindi yamekaushwa ili yasiharibike.
   b) Ndizi zote zimenunuliwa.
   c) Kahawa hii ina ladha nzuri.
   d) Viazi mviringo vinapendwa sana.
   e) Maharagwe yamepanda bei.
   f) Njugu zimevunwa leo.
5. i) fyekeo ii) jembe iii) trekta iv) upanga
6. Hakikisha kuwa sentensi zote ni sahihi.
   **Mifano ya sentensi**
   1. Mkulima ameutia upanga makali.
   2. Jembe hilo limetiwa mpini mwingine.
   3. Fyekeo jipya limenunuliwa.
   4. Plau inakokotwa na ng’ombe.
   5. Mkulima analiendesha trekta polepole.
7. Mfano wa jibu
   Kubuni nafasi za kazi kwa vijana kupitia kilimo cha kisasa. Kwa namna hiyo, vijana wataweza kupata mapato ya kuinua hali zao za maisha. Pia, ninaweza kuwafunza vijana na wananchi kwa jumla mbinu za kisasa za kilimo. Wakitumia mbinu hizo watafanya kilimo cha faida cha kuwasaidia kujiondoa katika umaskini.
8. **Mifano ya majibu**
   1. Punda: Punda wa Gwiza hubeba mizigo mingi.
   2. Ng’ombe: Kilimo cha ng’ombe wa maziwa kina faida kubwa.
   3. Kuku: Kuku wangu hutaga mayai kila siku.
   4. Ndama: Ndama wa Kaitesi hunyweshwa maziwa kwa chupa.
   5. Farasi: Farasi hufugwa na wakulima matajiri.

9. **Mifano ya vyuo vya kilimo nchini Rwanda ni kama vile:**
   1. Chuo Kikuu cha Rwanda – Chuo cha Kilimo na Tiba ya Mifugo *(University of Rwanda* (UR) - *College of Agriculture and Veterinary Medicine* (CAVM)
   2. Taasisi ya Utafiti wa Kilimo, Rwanda (*Rwanda Agricultural Research Institute (ISAR)*

10. **Mfano wa jibu**

    Umuhimu wa ufugaji: Wakulima hupata mbolea (samadi) kutokana na mifugo, wakulima hupata bidhaa kama vile mayai, maziwa, nyama, sufu kutokana na mifugo, wakulima hupata faida baada ya kuuza bidhaa zinazotokana na mifugo, ufugaji hubuni nafasi za ajira kwa wananchi miongoni mwa umuhimu mwingineo.

11. Tamaduni zinazohusiana na kilimo ni kama vile ushirikiano katika shughuli mbalimbali za kilimo kama vile kuvuna, kupanda na kupalilia. Utamaduni mwingine ni wa kuombea mazao yaliyopandwa ili yanawiri. Pia maombi ya kumshukuru Mwenyezi Mungu baada ya kuvuna mazao.

12. Mifano ya wanyama wa porini wapatikanao nchini Rwanda ni kama vile: nyani, sokwe, simba, pundamilia, twiga, fisi, chui, swara n.k.

13. a) simba – jamii ya paka/hula nyama/huishi katika vikundi.
    b) chui – hula nyama/huwinda sanasana usiku/ana madoadoa meusi mwilini
    c) swara – hula nyasi/hutembea katika vikundi
    d) sokwe – jamii ya nyani/hana mkia/ana uwezo wa kumwiga binadamu

14. **Faida za wanyama wa porini**
    1. Huwavutia watalii kuja nchini. Watalii huletea nchi yetu pesa za kigeni.
    2. Wanyama wa porini ni sehemu ya mazingira yetu.
    3. Wanyama wa porini hutumiwa na wanafunzi kusoma kuhusu wanyama.
    4. Wanyama wa porini ni sehemu ya mirathi ya taifa.

15. i. Kuhakikisha kwamba ujangili umepigwa marufuku ili kuhakikisha kwamba watalii wanapotembelea mbuga zetu wanawaona wanyama wote.
    ii). Kuwapa watalii diskaunti za kiingilio cha mbuga za wanyama wanapokuja wakiwa makundi ya watalii wengi.

16. Rejelea Kitabu cha Mwanafunzi
    a) Nomino ni maneno yanayotaja mtu, jina, kitu, hali, mahali au jambo.
    b) Vivumishi ni maneno yanayoongezea nomino maana.
    c) Vielezi pia huitwa viarifa. Ni maneno yafafanuayo vitenzi, vivumishi au vielezi vingine.
    d) Viwakilishi ama vibadala ni maneno ama viambata (sehemu za maneno) vinavyosimama badala ya majina.

17. Rejelea Kitabu cha Mwanafunzi

**a) Aina za nomino**

**Nomino za pekee**

Nomino za kipekee hutaja vitu au watu wenye sifa za kipekee. Zinapoandikwa katika sentensi, lazima zianze kwa herufi kubwa hata zikiwa katikati au mwishoni mwa sentensi. Nomino hizi pia huitwa nomino maalumu.

**Mifano ya nomino za kipekee:**

| | |
|---|---|
| Majina ya watu: | Ndoli, Abatoni, Ituze. |
| Majina ya Mungu: | Mola, Maulana, Rabuka na kadhalika. |
| Majina ya mataifa/nchi: | Rwanda, Kenya, Uganda, Marekani |
| Majina ya masomo: | Kilimo, Hisabati |
| Majina ya mji: | Kigali, Nairobi |
| Majina ya mlima: | Mlima Virunga |
| Majina ya mto: | Mto Akagera |

**Nomino za kawaida**

Nomino za kawaida hutaja vitu vya kawaida vinavyoweza kuchukua umoja na wingi kama jina lolote lile. Nomino hizo zinapoandikwa, huchukua herufi ndogo isipokuwa pale zinapojitokeza mwanzoni mwa sentensi. Mifano ya nomino za kawaida: mtu, ng'ombe, kondoo, mtume, mkulima, shamba

**Nomino za jamii**

Nomino za jamii pia huitwa nomino za makundi. Hizi ni nomino ambazo hutaja jumla ya vitu vingi au vitu katika makundi. Mifano wa nomino za jamii: chane ya ndizi, kija la maua, robota la pamba.

**Nomino za dhahania**

Katika kikundi hiki hupatikana nomino ambazo ni za kufikirika tu na wala hayawezi kuguswa. Chukua nomino kama urafiki. Urafiki ni neno la kufikirika au kudhaniwa tu na wala haliwezi kuonekana wala kushikika. Mifano ni kama vile: ukulima, njaa, shibe, uvunaji, upanzi.

**Nomino za wingi**

Hizi nazo ni nomino za vitu ambavyo daima hupatikana kwa wingi pekee au umoja pekee. Vitu vinavyotajwa na nomino hizi haviwezi kugawika. Mifano ya nomino za wingi: maziwa, sukari, chumvi, uji, chai, manukato, mvua na kadhalika.

**Nomino za vitenzi-jina**

Hizi ni nomino ambazo hutokana na vitenzi. Vitenzi hivyo huongezewa kiambishi cha awali 'ku' ili kuunda vitenzi jina. Mifano ni kama vile: kufyeka, kulima, kupanda na kufagia.

**b) Aina za vivumishi**

**Vivumishi vya sifa:** Haya ni maneno yatajayo tabia au sifa za kitu, hali au mtu na kiwakilishi chake. Mifano ni kama vile: njema, nzuri, mrembo, mrefu.

**Vivumishi vya pekee**

Vivumishi vya pekee hutoa habari kuhusu nomino au kiwakilishi chake kwa njia ya kipekee. Mifano ni kama vile: mwenye, yenye, mwenyewe, wote, wowote, mwingine, wengineo.

**Vivumishi vionyeshi**

Vivumishi vionyeshi au viashiria ni maneno ya kuonyesha alipo mtu au kitu, yaani ujirani. Kwa mfano, huyu, yule, hawa, huo.

**Vivumishi vionyeshi radidi**

Vivumishi hivi hutokana na kurudia vivumishi vionyeshi. Huleta maana ya kutilia mkazo. Kwa mfano, hawa hawa, lile lile, huo huo.

**Vivumishi viashiria visisitizi**

Hutumiwa kusisitiza jambo. Kwa mfano, lili hili, yuyo huyo.

**Vivumishi vya idadi**

Vivumishi vya idadi ni maneno yanayoonyesha idadi ya watu ama vitu. Vipo vivumishi vya idadi kamili, vivumishi vya idadi ya jumla na vivumishi vya idadi ya matokeo. Kwa mfano, vivumishi vya idadi kamili (tano, kumi, mbili), vivumishi vya idadi ya jumla/isiyo kamili (wengi, wachache)

**Vivumishi vya idadi ya matokeo**

Pia huitwa vivumishi vya nafasi katika orodha. Vivumishi hivi huonyesha nafasi ya nomino katika orodha. Mfano: mfugaji wa kwanza, simba wa mwisho, upanzi wa mwanzo.

**Vivumishi viulizi**

Hili ni kundi la vivumishi ambalo lina maneno yatumiwayo kuulizia maswali. Baadhi ya mifano ya vivumishi viulizi ni: yupi, zipi, ngapi, gani.

**Vivumishi vimilikishi**

Maneno katika kundi hili la vivumishi hujibu swali mtu, kitu au jambo ni la nani au lina nini? Kwa mfano, wangu, wetu, yako, yake.

**c) Aina za vielezi**

**Vielezi namna au jinsi**

Haya ni maneno ambayo huarifu jinsi ya kutendeka mambo. Mfano: sana, bure, kitoto, vizuri, upesi, kwa miguu, kwa bidii, bwe!

**Vielezi vya wakati**

Haya ni maneno yanayofafanua ama kueleza wakati wa kutokea tendo. Mathalan, ukisema Mgeni alifika jioni neno jioni ni kielezi cha wakati. Vipo vielezi vya wakati vya aina mbili: Vielezi vya wakati maalumu. Mifano: Januari, Disemba, Jumamosi,

saa tatu, kesho, leo, mtondo na kadhalika. Vielezi vinavyotaja wakati kwa jumla. Mifano: baadaye, zamani, daima, milele, awali, punde, karibuni, zama hizo.

**Vielezi vya kiasi/idadi**

Vielezi vya kiasi ni namna ya maneno ambayo hufafanua vitenzi kwa kujulisha limetokea mara ngapi tendo linalotajwa. Mifano:kila mara, kwa nadra, mara nyingi, tena na tena, mno, mara kumi, mara moja, mara nne, mara sita, mara kumi na mbili, mara ya kumi, mara ya kwanza, mara ya mwisho, mara ya ishirini.

**Vielezi vya mahali**

Haya nayo ni maneno ama mafungu ya maneno yanayofafanua panapotokea kitendo. Mara nyingi, maneno haya huwa ni majina ya mahali. Mifano: ndani, nje, karibu, juu, chini, kando, nyuma, pembeni.

18. Hivi ni vitenzi vyenye shina la silabi moja, kwa mfano:
    la - kula
    fa - kufa
    nywa - kunywa
19. a) wakati uliopo huwa na kiambishi -na- kama vile anacheza ilhali wakati uliopita huwa na kiambishi -li- kama vile alicheza.
    b) hali yakinishi ni kukubali kama vile anaimba nayo hali kanushi ni kukataa kama vile haimbi.
20. **Mfano wa funzo la Sura ya Kwanza ni kama vile:**

    Funzo la mazao na shughuli za ufugaji: Hili linafunza kuridhika na shughuli za kilimo na ufugaji kama njia mojawapo za kupigana na umaskini. Pia, kujivunia na utajiri utokanao na ufugaji na kilimo.

Sura ya 2

# Mada kuu: Utungaji (vipindi 12)

# Mada ndogo: Barua kuhusu matembezi, barua za kirafiki, barua za mwaliko, simu, tangazo/Ilani

**Uwezo upatikanao katika mada**

Mwanafunzi aweze kuandika barua kuhusu ziara au matembezi aliyoyafanya, barua za kirafiki na kadi za mialiko ya aina mbalimbali kwa kufuata taratibu za uandishi.

**Mbinu za kufundishia na kujifunzia**

i) Kutokana na fani ya kila aina ya matini walizopatiwa (barua, matangazo, mwaliko), wanafunzi waainishe matini hizo kwa usahihi.
ii) Kila mwanafunzi azungumzie barua ya kirafiki aliyoiandika mara yake ya kwanza kwa kueleza mwandikiwa na ujumbe aliompelekea na lugha aliyoitumia.
iii) Katika vikundi wanafunzi wachague wenyewe mada za kuandikia barua za kirafiki, mwaliko, tangazo na ilani na kisha waandike wakizingatia matumizi sahihi ya kanuni za utungaji.
iv) Wanafunzi washiriki kusoma barua, tangazo au ilani kwa sauti na kisha kujibu maswali yatokanayo na maudhui ya hicho kilichosomwa.

## Uhusiano wa mada na masomo mengine

Somo la ujasiriamali kuhusu maendeleo ya kibinafsi pia katika muundo wa biashara na utawala.

## Vigezo vya tathmini au upimaji

Uwezo wa kuandika barua mbalimbali za kirafiki, mialiko, matangazo na ilani akizingatia miundo sahihi na kanuni za kiuandishi na uwasilishaji wa ujumbe kwa namna iliyokusudiwa..

## Zana na vifaa

Majarida, vitabu, kalamu, karatasi, bahasha, stempu, picha ya mtu akitumbukiza barua kwenye kisanduku cha posta.

## Kipindi cha 1 na 2

## Kipindi cha 1

### Funzo

Barua ya kirafiki

**Shabaha**

Kufikia mwishoni mwa vipindi hivi, mwanafunzi aweze:

i) Kueleza waziwazi maana ya barua za kirafiki.
ii) Kuonyesha muundo kamili wa barua za kirafiki.
iii) Kutambua kanuni za kuandika barua za kirafiki.
iv) Kutumia maarifa aliyojifunza kumwandikia yeyote barua ya kirafiki.

**Zana na vifaa muhimu kwa kipindi hiki**

i) Unaweza kutumia barua za kirafiki tofauti tofauti
ii) Kitabu cha Mwanafunzi
iii) Vifaa vya wanafunzi wenye mahitaji maalumu.

**Mbinu**

Mhadhara, kuwashirikisha wanafunzi kujibu maswali ya darasani, kusoma na kujibu maswali kuhusu maelezo ya barua ya kirafiki.

## Utaratibu

### *Hatua ya 1*

Baada ya kujulisha malengo kwa wanafunzi kwa njia ya kuuliza maswali, waonyeshe barua ya kirafiki huku ukiwauliza maswali. Unaweza kuuliza:

i) Hii ni nini?
ii) Je, mnaona nini kwanza?
iii) Inafuatwa na nini?

Kwa kutumia maswali kama haya, waongoze wanafunzi kutambua maana ya barua ya kirafiki, anwani ya mwandishi, tarehe ya barua, maamkizi ya barua, ujumbe wa barua na hitimisho la barua.

### *Hatua ya 2*

Baada ya wanafunzi kuzijua sehemu hizo za barua, waongoze wanafunzi kujua undani wa kila sehemu. Mathalan, anuani huonyesha makazi ya mwandishi, na ujumbe wa barua ya kirafiki unaweza kuwa mrefu, na kadhalika.

### *Hatua ya 3*

Waongoze wanafunzi kusoma yaliyomo chini ya barua na barua ya kirafiki huku wakijibu maswali na kufanya mazoezi yaliyopo.

Hakikisha kuwa majibu ya kila sehemu ni sahihi.

### *Hatua ya 4*

Waongoze wanafunzi kufanyizia muhtasari wa sehemu hii ambao ni sharti wauandike madaftarini mwao.

**Maadili na mwenendo mwema**

Kuonyesha adabu na heshima kwa watu mbalimbali anaowaandikia barua za kirafiki.

**Tathmini**

Tathmini uwezo wa mwanafunzi wa kueleza muundo na kanuni za uandishi wa barua za kirafiki.

**Majibu ya mazoezi**

Hakikisha kuwa barua hizo zimezingatia muundo kamili wa barua ya kirafiki. Hoja zitiririke na ziandikwe kwa lugha iliyo sahihi. Aidha, ubunifu wa mwanafunzi ujitokeze.

## Kipindi cha 2

**Funzo**

Sehemu kuu za barua za kirafiki na kanuni za kuzingatiwa katika uandishi wa barua za kirafiki

**Shabaha**

Mwanafunzi aweze kuandika barua ya kirafiki kwa kufuata muundo na kanuni zake.

**Mbinu**

Mhadhara, kuwashirikisha wanafunzi kujibu maswali ya darasani, kusoma na kujibu maswali kuhusu maelezo ya barua ya kirafiki na kuandika barua za kirafiki.

***Hatua ya 1***

Wanafunzi wazungumzie waliyojifunza katika kipindi kilichotangulia. Wataje na kuonyesha sehemu kuu za barua za kirafiki.

***Hatua ya 2***

Waongoze wanafunzi kusoma yaliyomo katika Kitabu cha Mwanafunzi ili wafahamu kwa kina sehemu kuu za barua ya kirafiki na kanuni mbalimbali za kuzingatiwa katika uandishi wa barua za kirafiki. Baadaye, wanafunzi wafanye zoezi na kazi ya kikundi chini ya kifungu cha habari.

**Maadili na mwenendo mwema**

Kuonyesha adabu na heshima kwa watu mbalimbali anaowaandikia barua za kirafiki.

**Tathmini**

Tathmini uwezo wa mwanafunzi wa kuandika barua za kirafiki kwa kufuata muundo na kanuni zake.

**Zoezi la ziada**

Wanafunzi waandikiane barua za kirafiki kuhusu mada yoyote utakayochagua kisha wasome baadhi ya barua hizo mbele ya darasa. Hakikisha kuwa kila mwanafunzi

amefahamu vilivyo jinsi ya kuandika barua za kirafiki.

**Majibu ya zoezi**

S.L.P. 45,
Kigali,
RWANDA.

(Tarehe iandikwe hapa)

Kwa Shangazi Mpendwa,

U hali gani? Mimi nipo salama. Nia yangu kuu ya kukuandikia barua hii ni kukujulisha kuhusu mambo mawili makuu.

Kwanza, ningependa kukueleza kuwa ninazidi kutia bidii katika masomo. Juzi tulifanya majaribio na niliibuka nafasi ya tatu katika darasa letu. Ninatia bidii zaidi.

**Pili**, ninajua wewe unapenda sana kilimo cha ndizi. Juzi tulisoma kuhusu kilimo bora cha ndizi. Mwalimu wetu alitufunza mbinu mpya za kupanda ndizi. Tukifunga, nitakutembelea ili nikufunze mbinu hii mpya itakayokupa mavuno mengi zaidi.

Unisalimie wote waliopo nyumbani. Waambie nitawatembelea wakati wa likizo.

Wako Mpendwa,

(Jina la mwandishi liandikwe hapa)

## Kipindi cha 3 na 4

## Kipindi cha 3

### Funzo

Barua rasmi

### Shabaha

Kufikia mwishoni mwa vipindi hivi, mwanafunzi aweze:
i) Kueleza waziwazi maana ya barua rasmi.
ii) Kuwa na ujuzi wa istilahi zitumiwazo katika uandikaji wa barua rasmi.
iii) Kuonyesha muundo kamili wa barua rasmi.
iv) Kuonyesha waziwazi tofauti zilizopo kati ya barua ya kirafiki na barua rasmi.
v) Kutumia maarifa aliyojifunza kumwandikia yeyote barua rasmi.

**Zana na vifaa muhimu kwa vipindi hivi**

i) Unaweza kutumia barua rasmi mbalimbali
ii) Kitabu cha Mwanafunzi
iii) Vifaa vya wanafunzi wenye mahitaji maalumu.

### Mbinu

Mhadhara, kuwashirikisha wanafunzi kujibu maswali ya darasani, kusoma na kujibu maswali kuhusu maelezo ya barua rasmi.

## Utaratibu

### *Hatua ya 1*

Anza kwa kuwauliza wanafunzi maswali ya kuwakumbusha yale waliyojifunza katika kipindi kilichotangulia.

### *Hatua ya 2*

Waonyeshe wanafunzi barua rasmi huku ukiwauliza maswali kama vile:

i) Hii ni nini?
ii) Je, mnaona nini kwanza?
iii) Inafuatwa na nini?

Kwa kutumia maswali kama haya, waongoze wanafunzi kutambua maana ya barua rasmi, anwani ya mwandishi na mwandikiwa, tarehe ya barua, maamkizi ya barua, anwani, ujumbe wa barua na hitimisho la barua.

### *Hatua ya 3*

Waongoze wanafunzi kusoma na kuelewa yaliyomo katika Kitabu cha Mwanafunzi. Waongoze pia katika kufanya mazoezi chini yake. Hakikisha kuwa majibu ya kila sehemu wanayoyatoa ni sahihi.

### *Hatua ya 4*

Waongoze wanafunzi kuandika muhtasari wa sehemu hii ambao ni sharti wauandike madaftarini mwao.

### Maadili na mwenendo mwema

Kuonyesha adabu na heshima kwa watu mbalimbali anaowaandikia barua rasmi.

### Tathmini

Tathmini uwezo wa mwanafunzi wa kueleza muundo na kanuni za uandishi wa barua rasmi.

**Majibu ya mazoezi**

Hakikisha kuwa barua hizo zimezingatia miundo kamili ya barua rasmi, viwango vya juu vya urasmi katika matumizi ya lugha, mtiririko wa sentensi na usahihi wa kisarufi.

## Kipindi cha 4

### Funzo

Sehemu kuu na kanuni za barua rasmi

## Utaratibu

### *Hatua ya 1*

Wanafunzi wazungumzie waliyojifunza katika kipindi kilichotangulia.

### *Hatua ya 2*

Waongoze wanafunzi kusoma na kuigiza yaliyomo katika kifungu ili waelewe miundo na istilahi muhimu za barua rasmi pamoja na kutofautisha kati ya barua rasmi na barua ya kirafiki.

### *Hatua ya 3*

Waongoze wanafunzi kufanya mazoezi yaliyotolewa chini ya funzo hili. Hakikisha kila mwanafunzi anaweza kueleza muundo wa barua rasmi na kuzitofautisha na barua za kirafiki.

## Tathmini

### Zoezi la ziada

Waeleze wanafunzi wakuandikie barua rasmi wakieleza mambo muhimu waliyojifunza katika somo la leo.

**Majibu ya maswali**

i)
- Kuandikwa kwa anwani mbili (ya mwandishi juu na mwandikiwa chini yake).
- Kuandikwa kwa tarehe chini ya barua ya mwandishi kwa kuvuka mstari mmoja.
- Anayeandikiwa kutambuliwa kwa cheo chake kabla ya anwani yake.
- Kuandikwa kwa *Bwana* au *Bibi* au *Mheshimiwa* na kadhalika kabla ya kutajwa kwa jina la mwandikiwa.
- Kuandikwa kwa anwani baada ya kifupisho: *KUH* au *YAH* au *MINT* na kadhalika.
- Anwani kuandikwa kwa maneno yasiyozidi sita.
- Kutokuwepo kwa salamu.
- Kiini cha kuandikwa kwa barua kutolewa moja kwa moja.
- Kiwango cha juu cha urasmi kuzingatiwa.
- Mwandishi kujikita katika ujumbe wa kuandika barua.
- Huwa fupi.
- Katika hitimisho, mwandishi husema: *Wako mwaminifu* au *Wako mtiifu*, kisha sahihi ikifuatwa na jina na wakati mwingine cheo cha mwandishi.

ii) Hakikisha kuwa majibu au hoja wanazotoa wanafunzi ni sahihi.

| Barwa za kirafiki | Barwa rasmi |
|---|---|
| - Lugha isiyo rasmi hutumika. | - Lugha rasmi hutumika. |
| - Huweza kuwa ndefu. | - Huwa fupi. |
| - Huwa na anwani moja (ya mwandishi pekee). | - Huwa na anwani mbili (ya mwandishi na ya mwandikiwa). |
| - Haina kichwa. | - Huwa na kichwa. |
| - Huwepo salamu. | - Hakuna salamu. |
| - Mwandishi ana uhuru wa kuzungumzia mambo mengi apendavyo. | - Mwandishi hujikita katika kiini cha kwandikwa kwa barua. |

## Kipindi cha 5

### Funzo

Matangazo ya biashara

### Shabaha

Kufikia mwishoni mwa kipindi hiki, mwanafunzi aweze:
i) Kueleza maana na matumizi ya matangazo ya biashara.
ii) Kuainisha matangazo mbalimbali ya biashara.
iii) Kutambua na kutumia vilivyo istilahi muhimu kuandikia matangazo ya biashara.

**Zana na vifaa muhimu kwa kipindi hiki**

i) Unaweza kutumia mifano ya matangazo mbalimbali yaliyoandikwa.
ii) Kitabu cha Mwanafunzi.
iii) Matangazo yaliyonaswa kwenye vyombo mbalimbali.
iv) Unaweza kuwaelekeza wanafunzi kusikiliza matangazo ya televisheni na redio.
v) Vifaa vya wanafunzi wenye mahitaji maalumu.

### Mbinu

Mhadhara, kuwashirikisha wanafunzi kujibu maswali ya darasani, kusoma na kujibu maswali kuhusu maelezo ya barua rasmi na kuandika barua rasmi.

## Utaratibu

### *Hatua ya 1*

Unaweza kulianza somo hili kwa kuwaonyesha wanafunzi tangazo na kuwaeleza tangazo ni nini na matumizi yake ni yapi.

Baada ya hayo, unaweza kuwaongoza wanafunzi wajue maana ya matangazo ya biashara. Ikiwa tangazo ulilotumia hapo juu ni la biashara basi endelea kulitumia kama kifaa chako kabla ya kuwaonyesha matangazo mengine mbalimbali ya biashara.

Waonyeshe wanafunzi tangazo na uwaulize maswali ya maana, muundo, dhamira ya mwandishi na kadhalika. Unaweza kuuliza maswali kama vile:

i) Tangazo hili lina maana gani?
ii) Mwandishi ametumia muundo upi?
iii) Tangazo lina sehemu gani kuu?
iv) Mwandishi alinuia nini alipoliandika tangazo hili?

***Hatua ya 2***

Waongoze wanafunzi kuisoma sehemu hii iliyomo katika Kitabu cha Mwanafunzi. Hakikisha kwamba unashirikisha wanafunzi wote katika kusoma huko.

***Hatua ya 3***

Waelekeze wanafunzi kulifanya zoezi la sehemu hii lililomo vitabuni mwao huku ukiwasahihisha kabla ya kuwasaidia kuandika muhtasari wa sehemu hii.

**Maadili na mwenendo mwema**

Kuonyesha adabu na heshima kwa watu mbalimbali anaowaandikia barua rasmi.

**Tathmini**

Tathmini uwezo wa mwanafunzi wa kuandika barua rasmi kwa kufuata muundo na kanuni zake.

**Zoezi la ziada**

Wanafunzi waandike matangazo mbalimbali ya biashara kuhusu bidhaa wapendazo.

**Majibu ya zoezi**

1. Huwa na utangulizi wenye mvuto na hitimisho lenye kushawishi
2. - Matumizi ya takriri
   - Matumizi ya maneno mafupi mafupi
   - Matangazo kuambatana na muziki
   - Matumizi ya dayalojia

## Kipindi cha 6

**Funzo**

Matangazo ya mkutano na matangazo kuhusu ziara ya rais

**Shabaha**

Kufikia mwishoni mwa kipindi hiki, mwanafunzi aweze:

i) Kuandika matangazo ya mikutano mbalimbali.
ii) Kutambua matangazo kuhusu ziara ya rais.

**Zana na vifaa muhimu kwa kipindi hiki**

i) Kitabu cha Mwanafunzi
ii) Matangazo yaliyonaswa kwenye vyombo mbalimbali
iii) Matangazo ya redio na televisheni
iv) Vifaa vya wanafunzi wenye mahitaji maalumu.

## Utaratibu

### *Hatua ya 1*

Unaweza kuanza kufundisha hapa kwa kuwauliza wanafunzi maswali yanayolenga kuwakumbusha maana na matumizi ya matangazo.

Halafu kwa kutumia mbinu zile zile ulizotumia katika kipindi kilichopita, waonyeshe wanafunzi matangazo ya mkutano.

### *Hatua ya 2*

Ukimaliza hilo, funza tangazo la ziara ya rais. Hapa tumia pia mbinu ulizotumia katika *hatua ya 1* hapo juu.

### *Hatua ya 3*

Waongoze wanafunzi kutazama mifano ya matangazo ya mkutano na ziara ya rais katika vitabu vyao na kusoma maelezo chini yake. Waongoze pia katika kufanya mazoezi yaliyotolewa katika sehemu hii.

### *Hatua ya 4*

Waongoze wanafunzi katika kuunda muhtasari wa mambo muhimu waliyojifunza katika sehemu hii.

### Maadili na mwenendo mwema

Kujenga ushirikiano miongoni mwa wanajamii kwa kudumisha mawasiliano na upendo.

### Tathmini

Uwezo wa kuandika matangazo ya mikutano.

**Zoezi la ziada**

Waambie wanafunzi kuandika tangazo la mkutano wa wanafunzi wote wa kidato cha pili na walimu wa Kiswahili. Lengo kuu liwe kujadiliana kuhusu changamoto zinazokumba ufunzi wa somo hili na jinsi ya kukuza Kiswahili.

**Majibu ya zoezi**

Hakikisha kuwa kanuni na muundo wa matangazo umezingatiwa. Lugha iwe sahihi na rasmi.

## Kipindi cha 7

### Funzo

Matangazo ya kuwachagua watu kujiunga na kikosi cha polisi na matangazo kuhusu nafasi ya kazi

### Shabaha

Kufikia mwishoni mwa kipindi hiki, mwanafunzi aweze:

i) Kueleza maana na matumizi ya matangazo husika.
ii) Kuainisha matangazo mbalimbali husika.
iii) Kuandika matangazo husika.

### Zana na vifaa muhimu kwa kipindi hiki

i) Kitabu cha Mwanafunzi
ii) Matangazo yaliyonaswa kwenye vyombo mbalimbali
iii) Matangazo ya redio na televisheni
iv) Vifaa vya wanafunzi wenye mahitaji maalumu.

### Mbinu

Kuwashirikisha wanafunzi kusikiliza matangazo ya kuwachagua watu kujiunga katika kikosi cha polisi na matangazo kuhusu nafasi za kazi yaliyorikodiwa na kutazama matangazo yaliyoandikwa.

### Utaratibu

#### *Hatua ya 1*

Unaweza kuanza kufundisha hapa kwa kuwauliza wanafunzi maswali yanayolenga kuwakumbusha maana na matumizi ya matangazo.

Halafu kwa kutumia mbinu zile zile ulizotumia katika kipindi kilichopita, waonyeshe wanafunzi matangazo yanayolenga kutangaza nafasi fulani kama vile kikosi cha polisi, kazi, zabuni na kadhalika.

#### *Hatua ya 2*

Waongoze wanafunzi kutazama mifano ya matangazo katika sehemu hii katika vitabu vyao na kusoma maelezo chini yake. Waongoze pia katika kufanya mazoezi yaliyotolewa katika sehemu hii.

#### *Hatua ya 4*

Waongoze wanafunzi katika kuzungumzia muhtasari wa mambo muhimu waliyojifunza katika sehemu hii.

### Maadili na mwenendo mwema

Kujenga ushirikiano miongoni mwa wanajamii kwa kudumisha mawasiliano na upendo.

### Tathmini

Uwezo wa kuandika matangazo ya kuwachagua watu kujiunga katika kikosi cha polisi na matangazo kuhusu nafasi za kazi.

### Zoezi la ziada

Waambie wanafunzi kuandika matangazo kuhusu nafasi za kazi katika shule hii.

**Majibu ya zoezi**

Hakikisha kuwa sifa zilizotolewa ni sahihi.

## Kipindi cha 8

### Funzo

Ilani

### Shabaha

Kufikia mwishoni mwa kipindi hiki, mwanafunzi awe na uwezo wa:

i) Kueleza maana na matumizi ya ilani.
ii) Kuainisha ilani mbalimbali.
iii) Kuwasiliana vilivyo kuhusu ilani.

### Zana na vifaa muhimu kwa kipindi hiki

i) Kitabu cha Mwanafunzi
ii) Ilani mbalimbali zilizonaswa kwenye vyombo mbalimbali
iii) Ilani za televisheni na za redio
Kwa mfano, dhidi ya uchafuzi wa mazingira, dhidi ya kuvukia barabara mahali ambako hakujaruhusiwa.
iv) Vifaa vya wanafunzi wenye mahitaji maalumu
v) Ilani zilizoandikwa.

### Mbinu

Kuwashirikisha wanafunzi kusikiliza ilani zilizorikodiwa na kutazama ilani zilizoandikwa.

## Utaratibu

### *Hatua ya 1*

Ichukue ilani yoyote na uwaonyeshe wanafunzi. Waulize maswali kuhusu ilani hiyo ili waelewe maana na matumizi ya ilani.

### *Hatua ya 2*

Waongoze wanafunzi kutambua tofauti iliyopo kati ya ilani na matangazo. Mfano, tangazo hulenga kutoa habari fulani nayo ilani hulenga kutoa onyo fulani.

***Hatua ya 3***

Waelekeze wanafunzi kutazama na kusoma yaliyomo chini ya ilani katika vitabu vyao.

Waongoze kufanya zoezi la sehemu hii lililomo vitabuni mwao na kuhakikisha kuwa unawasahihisha pale kwa pale ama kwa kupitia vitabu vyao ama kwa yote mawili.

***Hatua ya 4***

Waelekeze wanafunzi kuandika au kuzungumzia muhtasari wa yale waliyosoma katika kipindi hiki.

**Tathmini**

Uwezo wa kuandaa na kuandika ilani kuhusu madhara ya uvutaji sigara.

**Zoezi la ziada**

Kila mwanafunzi aandike ilani kuhusu madhara ya uvutaji sigara.

**Majibu ya zoezi**

i) - Kutoa tahadhari au onyo.
- Jina la mtu au kampuni inayotoa ilani hiyo kuandikwa chini ya ilani husika.
- Madhara au matokeo ya kuenda kinyume na yaliyomo kwenye ilani kutolewa.
- Zipo madhara au hatua kuchukuliwa kwa watu wanaoenda kinyume na yaliyomo katika ilani.
- Huandikwa kwa herufi zenye wino nzito au herufi kubwa.
- Ni fupi fupi na kadhalika.

ii) Kubali jibu lolote sahihi linalozingatia muundo na yaliyomo katika ilani.

## Kipindi cha 9

**Funzo**

Mialiko

**Shabaha**

Kufikia mwishoni mwa kipindi hiki, wanafunzi wawe na uwezo wa:

i) Kueleza maana na matumizi ya mialiko.
ii) Kuainisha namna za mialiko.
iii) Kuwasiliana vilivyo kuhusu mialiko.
iv) Kuandika mialiko mbalimbali.

**Zana na vifaa muhimu kwa kipindi hiki**

i) Kitabu cha Mwanafunzi
ii) Mialiko mbalimbali iliyoandikwa kwenye kadi, karatasi, vibao n.k.
iii) Mialiko iliyonaswa kwenye vyombo kama vile vinasasauti au simu za mkono
iv) Mialiko ya televisheni na ya redio

v) Vifaa vya wanafunzi wenye mahitaji maalumu, kwa mfano, mialiko iliyorikodiwa na iliyoandikwa kwa maandishi ya wenye ulemavu wa kuona.

**Mbinu**

Kuwashirikisha wanafunzi kutazama mwaliko au kusikiliza mwaliko uliorikodiwa ili wachangie kuzungumzia kuhusu mialiko.

## Utaratibu

***Hatua ya 1***

Waonyeshe wanafunzi mwaliko wowote huku ukiwauliza maswali yanayolenga kufafanua maana ya mwaliko.

***Hatua ya 2***

Kwa kutumia kadi mbalimbali za harusi, funza maana, sifa na kanuni za mwaliko wa harusi.

***Hatua ya 3***

Kwa kuwaonyesha mialiko mingineyo, funza maana, sifa na kanuni za mialiko mingineyo kama vile mwaliko wa kutembelea mbuga za wanyama na mwaliko wa maonyesho ya vitabu.

***Hatua ya 4***

Wanafunzi wazungumzie tofauti zilizopo kati ya mialiko isiyokuwa rasmi (kama vile harusi, sherehe ya siku ya kuzaliwa na kadhalika) na mialiko rasmi (kama vile mwaliko wa kutembelea mbuga za wanyama, mwaliko wa kuhudhuria maonyesho na kadhalika).

***Hatua ya 5***

Sasa waongoze wanafunzi kusoma na kutazama mialiko mbalimbali vitabuni mwao (kuanzia ukurasa wa 64 hadi 66).

**Maadili na mwenendo mwema**

Kujenga ushirikiano miongoni mwa wanajamii kwa kudumisha mawasiliano na upendo.

**Tathmini**

Tathmini uwezo wa mwanafunzi wa kuandaa na kuandika mwaliko kwa wanafunzi wenzake ili kuhudhuria siku ya Kiswahili shuleni.

Baadaye, waongoze kufanya mazoezi katika sehemu hii.

**Zoezi la ziada**

i) Waeleze wanafunzi kuandika mwaliko kwa wanafunzi wenzao katika shule mbalimbali kuhudhuria siku ya Kiswahili shuleni humo.
ii) Wanafunzi waandike mialiko ya kualika marafiki zao kuhudhuria siku ya kusherehekea kuzaliwa kwao. Mfano uwe kama ufuatao:

**Familia ya Bwana na Bi. Mugabo**
S. L. P. 246,
**Remera.**
Ina furaha kumwalika Mhe./Prof./Dkt./Mhu./Bw./Bi.
………………………………………………………………………
………………………………..
Katika sherehe ya kukumbuka siku ya kuzaliwa kwa mwana wao, Lucy Umwali.

Sherehe itafanyika Ijumaa, tarehe 7/7/2017,
kuanzia saa nane alasiri katika ukumbi wa City Hall.
Mfawidhi wa sherehe atakuwa Bi. Ishimwe.

Kuja na kushiriki kwako kutaturidhisha.

Thibitisho kwa:
Bw. Mugabo,
S. L. P. 246,
**Remera.**

**Majibu ya mazoezi**

Hakikisha kuwa barua husika zinazingatia kanuni za mialiko.

## Kipindi cha 10 na 11

### Funzo

Aina za alama za uandishi na matumizi yake

### Shabaha

Kufikia mwishoni mwa vipindi hivi, mwanafunzi awe na uwezo wa:
i) Kutambua alama mbalimbali za uandishi.
ii) Kueleza maana na matumizi ya alama hizo.
iii) Kuzitumia vilivyo alama hizo.

**Zana na vifaa muhimu kwa vipindi hivi**
i) Kitabu cha Mwanafunzi
ii) Michoro ya alama tofauti tofauti baadhi zikiwa kwenye karatasi moja na nyingine kwenye kadi
iii) Vifaa vya wanafunzi wenye mahitaji maalumu.

**Mbinu**

Kushirikisha wanafunzi kutambua alama za uandishi na kuzitumia katika sentensi fupi.

## Kipindi cha 10

**Funzo**

Nukta (.), koma (,), nukta mbili au koloni (:), semi koloni au nukta na kituo (;) kistari kifupi (-) na alama ya hisi (!)

## Utaratibu

***Hatua ya 1***

Kwa kutumia michoro iliyopo kwenye vifaa mbalimbali kama vile kadi, funza maana na matumizi ya nukta (.), koma au mkato wa chini (,), nukta mbili au koloni (:), na semi koloni au nukta na kituo (;) kistari kifupi (-) na alama ya hisi (!). Kabla ya kufunza alama hizo, hakikisha ya kwamba wanafunzi wanaweza kuzibainisha vilivyo alama hizi katika sentensi fupifupi.

***Hatua ya 2***

Waongoze wanafunzi kuisoma sehemu hii iliyomo vitabuni mwao na kufanya mazoezi husika.

***Hatua ya 3***

Unaweza kuhitimisha somo hili kwa kuwauliza wanafunzi maswali ya kuambatanisha kadi na jina la kiakifishi pamoja na matumizi ya kiakifishi husika.

**Tathmini**

Tathmini uwezo wa mwanafunzi wa kutumia alama za uandishi zilizosomwa katika kipindi.

## Kipindi cha 11

**Funzo**

Kiulizi (?), parandesi (), mkwaju (/), mtajo (‘ ’ au “ ”), herufi kubwa (H) na herufi ndogo (h) (Kitabu cha Mwanafunzi, ukurasa wa 69-70)

***Hatua ya 1***

Wanafunzi wazungumzie waliyojifunza katika kipindi kilichotangulia.

***Hatua ya 2***

Kwa kutumia michoro kama vile kadi, funza maana na matumizi ya kiulizi (?), parandesi (), mkwaju (/), mtajo (‘ ’ au “ ”), herufi kubwa (H) na herufi ndogo (h). Kabla ya kufunza alama husika, hakikisha ya kwamba wanafunzi wanaweza kuzibainisha vilivyo alama hizi katika sentensi fupifupi.

***Hatua ya 3***

Waongoze wanafunzi kuisoma sehemu hii iliyomo vitabuni mwao na kufanya mazoezi husika.

***Hatua ya 4***

Unaweza kuhitimisha somo hili kwa kuwauliza wanafunzi maswali ya kuambatanisha kadi na jina la kiakifishi pamoja na matumizi ya kiakifishi husika.

**Zoei la ziada**

Wape wanafunzi kipande cha gazeti la Kiswahili au kitabu cha hadithi cha Kiswahili na uwaambie kubainisha alama mbalimbali za uakifishaji. Watambue jinsi alama hizo zilivyotumika na hata kubainisha pale ambapo alama hizo zimetumika visivyo.

**Majibu ya zoezi**

Ilikuwa asubuhi na mapema. Bw. **B**utera alipotoka kwake kwenda kazini, fikirani mwake alijikumbusha, “**P**indi nikifika ofisini, nitaomba ruhusa niende nimlipie binti yangu karo.”

**A**liabiri gari linaloelekea **R**uhango. Baada ya mwendo mfupi tu, lo! Gari hilo lilipata ajali! **L**iligongana na lori japo ng’ombe waliokuwemo njiani walikufa takriban wote, abiria walipata majeraha madogo madogo lakini ililazimu wapelekwe hospitalini. **H**ivyo, **B**utera hakutimiza azma yake.

**Majibu ya mazoezi ya ziada**

A.

Hakikisha kuwa kifungu hicho kimendikwa kwa lugha sahihi, kina mtiririko, na kuwa alama zote zimetumika kwa njia sahihi. Pawepo matumizi ya alama angalau sita za uakifishaji.

B.

Hakikisha kuwa alama zote zilizobainishwa ni sahihi.

## Kipindi cha 12

### Funzo

Maswali ya marudio

### Shabaha

Kufikia mwishoni mwa kipindi hiki, mwanafunzi aweze:

i) Kujitathmini na kuona kama ameyaelewa vilivyo yote aliyofunzwa na kujifunza katika sehemu hii.

**Zana na vifaa muhimu kwa kipindi hiki**

i) Kitabu cha Mwanafunzi

**Mbinu**

Kushirikisha wanafunzi kutambua alama za uandishi na kuzitumia katika sentensi fupi.

## Utaratibu

***Hatua ya 1***

Baada ya kuwapongeza wanafunzi na kuwatia ari ya kutaka kujifunza mengi zaidi kuhusu lugha hii, waongoze wanafunzi kujibu mawali ya sehemu hii.

***Hatua ya 2***

Waongoze wanafunzi kusahihisha majibu yao ya sehemu hii.

**Tathmini**

Tathmini uwezo wa mwanafunzi wa kutumia alama za uandishi zilizosomwa katika kipindi.

**Majibu ya maswali ya marudio**

1. Barua ambayo huandikiwa mtu au watu mbalimbali walio na uhusiano wa karibu na mwandishi.
2. a) Mifano: baba, mama, rafiki, kaka, dada, mpenzi, mke, mume, babu na kadhalika.
   b) Hakikisha kuwa barua hiyo imechukua muundo wa barua ya kirafiki. Lugha itumiwe kwa njia sahihi (lugha isiyokuwa na urasmi).
3. Anwani ya kuonyesha alipo mwandishi, tarehe kuonyesha barua imeandikwa lini, mtajo wa anayeandikiwa ili iwe wazi barua ni ya nani, mwili wa barua ambao una ujumbe wa barua hiyo, hitimisho ( kuaga aandikiwaye na utambulisho wa mwandishi).
4. Barua rasmi ni barua aandikiwayo mtu mwenye madaraka.
5. Barua ya kuomba kazi, barua ya kuomba kibali, barua ya kutaka upewe hati miliki ya shamba lako, barua ya kuomba uhamisho kikazi, barua kwa mhariri, barua ya malalamishi na kadhalika.
6. Hakikisha kuwa muundo kamili wa barua rasmi umetumika. Mwanafunzi atumie lugha rasmi.
7. Anwani ya mwandishi, tarehe, anwani ya mwandikiwa, mtajo wa anayeandikiwa, mintarafu, mwili wa barua, na hitimisho.
8. - Kuandikwa kwa anwani mbili (ya mwandishi juu na mwandikiwa chini yake).
   - Kuandikwa kwa tarehe chini ya barua ya mwandishi kwa kuvuka mstari mmoja.
   - Anayeandikiwa kutambuliwa kwa cheo chake kabla ya anwani yake.

- Kuandikwa kwa *Bwana* au *Bibi* au *Mheshimiwa* na kadhalika kabla ya kutajwa kwa jina la mwandikiwa.
- Kuandikwa kwa anwani baada ya kifupisho: *KUH* au *YAH* au *MINT* na kadhalika.
- Anwani kuandikwa kwa maneno yasiyozidi sita.
- Kutokuwepo kwa salamu
- Kiini cha kuandikwa kwa barua kutolewa moja kwa moja.
- Kiwango cha juu cha urasmi kuzingatiwa.
- Mwandishi kujikita katika ujumbe wa kuandika barua.
- Huwa fupi.
- Katika hitimisho, mwandishi husema: *Wako mwaminifu* au *Wako mtiifu*, kisha sahihi ikifuatwa na jina na wakati mwingine cheo cha mwandishi.

9.

| **Barua rasmi** | **Barua ya kirafiki** |
|---|---|
| Lugha rasmi hutumika. | Lugha isiyokuwa rasmi hutumika. |
| Huwa fupi. | Huweza kuwa ndefu. |
| Huwa na anwani mbili (ya mwandishi na mwandikiwa). | Huwa na anwani moja (ya mwandishi pekee). |
| Huwa na kichwa. | Haina kichwa. |
| Hakuna salamu. | Huwepo salamu. |
| Mwandishi hujikita katika kiini cha kuandikwa kwa barua/ujumbe. | Mwandishi ana uhuru wa kuzungumzia mambo mengi apendavyo. |
| Hutiwa sahihi na wakati mwingine cheo cha mwandishi hutajwa. | Haina sahihi wala cheo cha mwandishi hakitajwi popote. |
| Huandikiwa mtu katika mazingira rasmi/mtu asiyekuwa na uhusiano wowote au wa karibu na mwandishi. | Huandikiwa mtu aliye na uhusiano wa karibu na mwandishi. |

10. Kubali jibu lolote sahihi. Mfano: tangazo ni mpangilio wa maandishi kwa mtindo maalumu kwa lengo la kupasha ama kupokeza ujumbe fulani wa kidharura au muhimu.

11. Tangazo halina anwani ilhali barua rasmi inazo anwani mbili.

12. Tangazo la tanzia hulenga kutoa ujumbe wa huzuni kuhusu kifo cha mtu, tarehe na mahali pa mazishi ilhali la mkutano hulenga kutoa ujumbe wa mahali pa mkutano, ajenda, na tarehe ya mkutano.

13. a) Ilani ni tangazo ambalo hutahadharisha au kuarifu kuhusu aina ya jambo ama tukio ambalo linastahili kuepukwa au kutiliwa maanani.

 b) **Mfano wa ilani**

**Kumbuka kunawa mikono baada ya kutoka msalani!**




**Kunawa mikono huzuia magonjwa.**

14. a) - matangazo ya biashara huwa na utangulizi wenye mvuto na hitimisho lenye ushawishi
- yapo matumizi ya takriri
- huwa na maneno mafupi mafupi yenye mnato na ujumbe mzito
- huambatana na sauti ya kimuziki!
- wakati mwingine, hufuata mtindo wa dayalojia
- hutumia lugha ya kushawishi
- hueleza ubora wa bidhaa pekee na manufaa yake
- hutoa mwito wa kutembelewa kampuni husika.

b) Mfano wa tangazo la kibiashara kuhusu bidhaa

**Tangazo la Bidhaa**

Madaktari wa meno tisa miongoni mwa madaktari kumi hupendekeza dawa ya meno ya **MENO SAFI!**




**Kinga meno yako kwa kupiga mswaki na MENO SAFI!**

15. Hutoa maelezo kwa mtu au kikundi cha watu kufika katika eneo fulani kwa minajili ya shughuli fulani maalumu.
16. Kubali ufafanuzi wowote sahihi.

**Mfano:**

Tunapoandika au kusoma, tunaakifisha.

Tunatumia alama za uandishi.

Tunatambua kama usemi umekwisha, kuuliza swali, kushangaa, n.k.

Tunajua wapi tunafaa kupumua kidogo, kushusha au kupandisha sauti, n.k.

17. Kuandikia tarehe, kuonyesha kuwa sentensi imefika mwisho, kutumiwa katika ufupisho, hutumiwa katika uandishi wa tarehe na kadhalika.
18. Mifano na maelezo yarejelewe katika Kitabu cha Mwanafunzi.

**Mfano:**

1) Huwekwa mwishoni mwa sentensi. M.f: Nimechoka.

2) Hutumiwa kuonyesha ufupisho wa maneno. M.f: S.L.P. - Sanduku La Posta.

3) Hutumika kubainisha saa na dakika au tarehe. M.f: 3.20 - Saa tisa na dakika ishirini.

4) Hutumiwa kuonyesha vipashio vya pesa. M.f: Sh.10.50 - Shillingi kumi na thumuni hamsini.

5) Zikitumiwa mara tatu mfululizo (...), Huonyesha kutokamilika kwa sehemu husika. M.f: Nitakupa lakini ni sharti...

19. a) Alama zinazotumiwa kuonyesha maneno halisi ya msemaji.
    b) Mifano ya sentensi:
       i) "Msifanye uzembe katika masomo yenu," Mwalimu aliwashauri wanafunzi.
       ii) "Sielewi," Mwiza alisema akitikisa kichwa, "ni kwa nini alisema maneno hayo."

20. **Mfano wa jibu**

    Nimejifunza mambo yafuatayo katika sura hii:

    a) Kutofautisha barua rasmi na barua za kirafiki na kuandika aina hizi za barua.
    b) Kutumia alama za uandishi kama vile: nukta, mkato, koloni, nukta na kituo, kistari kifupi, alama ya mshangao, kiulizi, mabano, mkato, herufi kubwa na ndogo na alama za mtajo.

Sura ya 3

# Mada kuu: Matumizi ya lugha katika mazingira mbalimbali (vipindi 20)

# Mada ndogo: Rejesta za mpira na burudani

## Uwezo upatikanao katika mada

Mwanafunzi aweze kusikiliza, kusoma, kuandika na kubaini sifa na dhima za rejesta mbalimbali katika mazingira ya michezo na burudani.

**Mbinu za kufundishia na kujifunzia**

i) Katika makundi, wanafunzi wapewe rejesta mbalimbali za mpirani na burudani na kuziigiza.

ii) Licha ya rejesta za michezo na burudani wanafunzi wapewe rejesta nyingine tofauti zitumiwazo katika mazingira mbalimbali kama vile hotelini, mahakamani, bungeni, n.k.

iii) Kubainisha na kuainisha aina mbalimbali za rejesta kutokana na matini walizopewa na wahakikishe wanaeleza sifa za msingi za aina hiyo ya rejesta.

iv) Wanafunzi washiriki katika majadiliano kuhusu dhana ya michezo na burudani katika kujenga afya.

v) Wanafunzi wafanye kazi ya mradi wa kukusanya rejesta zinazotumika katika mazingira mbalimbali na kuzitolea maoni darasani.

vi) Kubainisha matumizi sahihi na yasiyo sahihi ya ngeli za KI-VI.

vii) Wanafunzi watunge sentensi fupi kadhaa wakitumia majina ya ngeli ya KI-VI umoja na wingi.

## Uhusiano wa mada na masomo mengine

Somo la historia kuhusiana na mada ihusuyo uvumilivu na heshima pia katika somo la karatasi ya maarifa kuhusu utalii, michezo, burudani na maendeleo.

## Vigezo vya tathmini au upimaji

Uwezo wa kuwasiliana kwa kutumia rejesta mbalimbali, kujua aina mbalimbali za rejesta.

## Zana na vifaa

Mchezo uliorikodiwa, mpira, picha za wachezaji uwanjani, picha za wachezaji mashuhuri, picha za maeneo mbalimbali yanayojulikana kuwa na rejesta maalumu kama vile kanisani, hospitali, mahakamani, n.k.

## Kipindi cha 1 na 2

### Funzo

Rejesta za mpira wa miguu

### Shabaha

Kufikia mwishoni mwa vipindi hivi, mwanafunzi aweze:

i) Kutambua maana ya rejesta ama sajili.
ii) Kubaini rejesta ya mpira wa miguu.
iii) Kutumia vilivyo lugha ya rejesta ya mpira katika mawasiliano yake ya kila siku.
iv) Kuzitambua na kuzizungumzia sifa za rejesta hii.

**Zana na vifaa muhimu kwa vipindi hivi**

i) Michoro mbalimbali
ii) Kuwapeleka wanafunzi kulipo na mchezo wa kandanda
iii) Vifaa vya wanafunzi wenye mahitaji maalumu
iv) Vifaa halisi vya msamiati wa mpira
v) Matangazo yaliyorekodiwa ya mpira wa miguu
vi) Kitabu cha Mwanafunzi.

### Mbinu

Kuwashirikisha wanafunzi kuzungumzia kuhusu mambo wanayoyajua kuhusiana na mchezo wa mpira wa miguu na baadaye kusoma pamoja maelezo yaliyomo katika Kitabu cha Mwanafunzi.

### Masuala mtambuka

Vipindi hivi vinatoa nafasi ya kuzungumzia masuala mtambuka kama vile: uhusika wa kijinsia, UKIMWI na jinsi michezo inavyoweza kutumiwa ili kujenga ushirikiano na kupinga uadui wa kimbari.

## Kipindi cha 1

### Funzo

Maelezo ya rejesta na matangazo ya mpira wa kandanda

## Utaratibu

***Hatua ya 1***

Unaweza kuanza kuwafunza kwa kuuliza maswali juu ya lugha ya vijana. Halafu utumie mfano huo kueleza maana ya rejesta ama sajili pamoja na rejesta ya mpira wa miguu. Eleza pia kuwa yapo maeneo yanayojulikana kuwa na rejesta maalumu kama vile michezoni, maeneo ya burudani, kanisani, hospitalini, mahakamani, sokoni, bungeni, hotelini na kadhalika.

***Hatua ya 2***

Baada ya hayo, tumia vifaa mbalimbali ulivyotayarisha kufunzia lugha ya mpira wa miguu kwa kutumia mbinu zile zile za kufunza msamiati.

***Hatua ya 3***

Waongoze wanafunzi kuisoma sehemu hii iliyomo vitabuni mwao. Kama ilivyo kawaida, hakikisha ya kuwa umewashirikisha wanafunzi wote katika usomaji.

***Hatua ya 4***

Waelekeze wanafunzi kujibu zoezi la sehemu hii kabla ya kuwaongoza kusahihisha majibu yao.

***Hatua ya 5***

Waongoze wanafunzi katika kutaja muhtasari wa yale waliyojifunza katika sehemu hii ili kuhakikisha kuwa malengo ya kipindi hiki yametimizwa.

**Maadili na mwenendo mwema**

Kuonyesha adabu na heshima kwa watu mbalimbali kwenye michezo.

**Tathmini**

Tathmini uwezo wa mwanafunzi wa kujibu maswali ya zoezi baada ya kusoma kifungu.

**Majibu ya zoezi**

**Mifano ya majibu**

1. Wanafunzi watunge sentensi sahihi kama vile:
   a) Kabumbu ni mchezo maarufu nchini Rwanda na ulimwenguni.
   b) Timu ya kabumbu ya shule ya wasichana ya Elimu Bora ilichuana na timu ya shule ya wasichana ya Tusonge Mbele.
   c) Fainali za Kombe la Dunia za mwaka 2004 katika mchezo wa kabumbu kwa wanaume zilifanyika nchini Afrika Kusini.
   d) Jumla ya timu kumi zitawania kombe hilo litakalotolewa na serikali.
   e) Katika mchezo wa kabumbu, wapinzani hushindania mpira.
2. a) Maana ya maneno ya rejesta ya mpira wa miguu ambayo hayakuorodheshwa
   i) golikipa – mchezaji anayezuia bao liingizwe langoni katika mpira wa miguu
   ii) kombora – mpira uliopigwa kwa nguvu
   iii) refa – mwamuzi katika mchezo wa mpira wa miguu
   iv) pambano – mashindano ya timu mbili katika mpira wa miguu
   v) pasi – upitishaji wa mpira kutoka kwa mchezaji mmoja hadi wa pili
   vi) timu – kikundi wa wachezaji cha upande mmoja katika mpira wa miguu

## Kipindi cha 2

Sifa za rejesta ya mpira wa miguu

***Hatua ya 1***

Waongoze wanafunzi kuzungumzia waliyojifunza katika kipindi kilichotangulia.

***Hatua ya 2***

Kupitia matangazo na vifungu mbalimbali, waongoze wanafunzi kutambua na kutaja sifa za sajili ya mpira wa miguu na michezo mingineyo.

***Hatua ya 3***

Waongoze wanafunzi katika kusoma na kufafanua sifa za matangazo ya mpira wa miguu katika Kitabu cha Mwanafunzi. Hakikisha kuwa wanafunzi wanaweza kutambua sifa hizo na kuzitolea mifano.

***Hatua ya 4***

Waongoze wanafunzi kufanya mazoezi yaliyomo katika sehemu hii.

**Suala mtambuka**

Kipindi hiki kinatoa nafasi ya kujadili umuhimu wa kuchukua tahadhari wakati wa kushiriki burudani kwa sababu maambukizi ya UKIMWI na matumizi ya dawa za kulevya hufanyika kwenye burudani.

**Zoezi la ziada**

Wape baadhi ya wanafunzi fursa ya kutangaza mpira mbele ya darasa wakizingatia waliyojifunza katika sehemu hii. Wanafunzi wengineo wasikilize kwa makini huku wakiandika sifa zinazojitokeza katika matangazo hayo kisha wazitaje baada ya matangazo.

## Kipindi cha 3 na 4

**Funzo**

Rejesta ya burudani

**Shabaha**

Kufikia mwishoni mwa vipindi hivi, mwanafunzi aweze:

i) Kutambua rejesta ama sajili ya burudani.
ii) Kubaini rejesta ya burudani.
iii) Kutambua sifa za rejesta ya burudani.
iv) Kutumia vilivyo lugha ya rejesta ya burudani katika mawasiliano yake ya kila siku.

**Zana na vifaa muhimu kwa vipindi hivi**

i) Michoro ama picha mbalimbali k.v. za bendi, ala za muziki, kipazasauti na kadhalika.

ii) Vifaa vya wanafunzi wenye mahitaji maalumu
iii) Vifaa halisi vya msamiati wa burudani
iv) Burudani iliyorekodiwa kama vile nyimbo za dini
v) Kitabu cha Mwanafunzi.

**Mbinu**

Kuwashirikisha wanafunzi katika vikundi kuzungumzia kuhusu mambo wanayoyajua kuhusiana na burudani baada ya kuutazama mchoro na baadaye kusoma pamoja kifungu katika Kitabu cha Mwanafunzi.

**Suala mtambuka**

Kipindi hiki kinatoa nafasi ya kujadili umuhimu wa kuchukua tahadhari wakati wa kushiriki burudani kwa sababu maambukizi ya UKIMWI na matumizi ya dawa za kulevya hufanyika kwenye burudani.

## Kipindi cha 3

Maelezo na kifungu cha habari kuhusu rejesta ya burudani

## Utaratibu

***Hatua ya 1***

Anza somo hili kwa kuwauliza wanafunzi maswali ya kurudia yale waliyoyajifunza katika kipindi cha pili hapo juu. Ni sharti waweze kueleza vilivyo maana ya rejesta.

***Hatua ya 2***

Baada ya utangulizi huo, tumia vifaa mbalimbali ulivyovitayarisha kufunzia maana na mifano ya rejesta ya burudani. Kwa mfano, unaweza kuonyesha picha ya bendi fulani na kuwaongoza wanafunzi katika kuijadili.

***Hatua ya 3***

Baada ya hayo, waongoze wanafunzi kusoma maelezo kuhusu rejesta ya burudani na kuigiza au kusoma kifungu cha habari chini ya rejesta ya burudani (Kitabu cha Mwanafunzi). Hakikisha ya kuwa umewashirikisha wanafunzi wote.

***Hatua ya 4***

Waelekeze wanafunzi katika kufanya mazoezi ya sehemu hii pamoja na kuyafanyia masahihisho majibu yao.

***Hatua ya 5***

Waongoze wanafunzi katika kuandaa muhtasari wa yale yaliyo muhimu na ambayo wamejifunza katika sehemu hii. Hakikisha kuwa malengo ya kipindi hiki yamefikiwa.

### Suala mtambuka
Kipindi hiki kinatoa nafasi ya kujadili umuhimu wa kuchukua tahadhari wakati wa kushiriki burudani kwa sababu maambukizi ya UKIMWI na matumizi ya dawa za kulevya hufanyika kwenye burudani.

### Tathmini
Tathmini uwezo wa mwanafunzi wa kutumia kwa usahihi lugha ya rejesta ya burudani katika mawasiliano.

## Kipindi cha 4

### Funzo
Sifa za rejesta ya burudani

### Utaratibu

***Hatua ya 1***
Waongoze wanafunzi kukumbuka na kuzungumzia mambo muhimu katika kipindi kilichotangulia. Kwa mfano, wataje maneno maalumu/msamiati wa burudani na wautungie sentensi sahihi.

***Hatua ya 2***
Kwa kutumia vifaa na zana mbalimbali pamoja na mifano waliyotoa wanafunzi, waongoze wanafunzi kutambua na kuzungumzia sifa za sajili ya burudani.

***Hatua ya 3***
Waongoze wanafunzi kusoma sifa za rejesta ya burudani katika Kitabu cha Mwanafunzi. Watoe mifano zaidi.

***Hatua ya 4***
Waongoze wanafunzi kufanya kazi ya wanafunzi wawili wawili. Hakikisha kuwa majibu yao ni sahihi.

### Maadili na mwenendo mwema
Kuonyesha adabu na heshima kwa watu mbalimbali kwenye burudani.

### Tathmini
Tathmini uwezo wa mwanafunzi wa kujibu maswali ya zoezi baada ya kusoma kifungu.

### Zoezi la ziada
Wape baadhi ya wanafunzi fursa ya kuwaburudisha wenzao kupitia njia yoyote ile kama vichekesho, shairi, kuimba wimbo wa kitamaduni na kadhalika. Baada ya burudani hizo, wazungumzie burudani husika na wataje sifa za burudani hizo.

## Kipindi cha 5 na 6

### Funzo
Umuhimu wa michezo na burudani

**Shabaha**

Kufikia mwishoni mwa vipindi hivi, mwanafunzi aweze:

i) Kuutambua umuhimu wa michezo na burudani.
ii) Kuelezea kwa ufasaha umuhimu wa michezo na burudani katika mwili wa binadamu.

**Zana na vifaa muhimu kwa vipindi hivi**

i) Michoro na picha za michezo na burudani mbalimbali.
ii) Picha za wanamichezo na waimbaji tofauti.
iii) Zana na vifaa halisi vya michezo na burudani.
iv) Kitabu cha Mwanafunzi.
v) Video za mashindano mbalimbali ya michezo na burudani.
vi) Vifaa vya wanafunzi wenye mahitaji maalumu
vii) Mtandao.

**Mbinu**

Kuwashirikisha wanafunzi katika vikundi kuzungumzia kuhusu umuhimu wa michezo baada ya kuitazama michoro na baadaye kusoma pamoja kifungu katika Kitabu cha Mwanafunzi.

**Masuala mtambuka**

Kipindi hiki kinatoa nafasi nzuri ya kujadili suala la kutumia michezo ili kuleta ushirikiano wa kijamii ili kuondoa uadui wa kimbari. Huu ni umuhimu mkubwa wa michezo.

## Kipindi cha 5

**Funzo**

Umuhimu wa michezo

### Utaratibu

***Hatua ya 1***

Unaweza kuanza somo hili kwa kuwaonyesha wanafunzi video fupi ya mashindano ya michezo mbalimbali pamoja na washindi wakitunukiwa zawadi. Baada ya hapo, waongoze wanafunzi kujadili yale waliyoyaona kwa kuwauliza maswali kama vile:

i) Huu ni mchezo gani?
ii) Wachezaji wamefaidika kwa njia gani?
iii) Umefaidikaje kwa kutazama video (au picha  au michoro) hii?
iv) Ungependa kuwa bingwa wa mchezo gani? Kwa nini?

***Hatua ya 2***

Kwa kutumia vifaa mbalimbali ulivyotayarisha, funza malengo ya sehemu hii. Unaweza kuanza kwa kuwaonyesha picha ya wachezaji wakifanya mazoezi ya viungo vya mwili.

Umuhimu wa michezo ni pamoja na:

i) Kukuza ushirikiano na umoja wa nchi
ii) Njia ya kujipatia mapato
iii) Afya nzuri
iv) Sifa nzuri kwa mchezaji na nchi yake
v) Kuwezesha mshiriki kuzuru kwingi na kujionea mengi ya huko na kadhalika.

***Hatua ya 3***

Waongoze wanafunzi watazame na kuijadili michoro hiyo iliyomo vitabuni mwao Unaweza kuwauliza wataje majina ya michezo kwenye mchoro. Majina hayo ni kama vile:

| | | |
|---|---|---|
| 1. mbio za nyika | 2. mpira wa kikapu | 3. mpira wa pete |
| 4. mpira wa magongo | 5. kuruka mbali | 6. kandanda/mpira wa miguu |

Baada ya hilo, waelekeze wanafunzi kukisoma kifungu katika Kitabu cha Mwanafunzi, ukurasa wa 80 na uwashirikishe wanafunzi wote.

***Hatua ya 4***

Waongoze wanafunzi katika kujibu maswali yaliyoulizwa pamoja na kufanya kazi ya kikundi waliyopewa. Hakikisha ya kuwa majadiliano yao yanafanywa vilivyo.

***Hatua ya 5***

Baada ya kuwaongoza wanafunzi kufanya masahihisho ya majibu yao, waongoze pia katika kufanya muhtasari wa yale waliyojifunza katika sehemu hii. Hakikisha kuwa malengo ya kipindi hiki yametimizwa.

**Maadili na mwenendo mwema**

Kuonyesha shauku ya kupenda michezo.

**Tathmini**

Tathmini uwezo wa mwanafunzi wa kujibu maswali kwa usahihi baada ya kusoma kifungu na kueleza kuhusu umuhimu wa michezo .

**Majibu ya maswali (Kitabu cha Mwanafunzi, ukurasa wa 80)**

1. - Huimarisha afya yetu
   - Huleta umoja miongoni mwa wanajamii
   - Huleta fahari
   - Huleta pato
2. Mazoezi ya viungo ambavyo hufanywa na wachezaji husaidia miili yao kuyeyusha mafuta ya ziada, kunyosha misuli, kuimarisha mapigo ya moyo hivyo basi kuimarisha usambazaji wa damu katika akili na viungo vinginevyo.
3. Watu wanapocheza au kwenda kutazama michezo, hujumuika pamoja/Watu wanaposhabikia timu fulani hasa timu ya taifa huja pamoja na kujenga urafiki.
4. Kubali hoja zozote sahihi kwa mujibu wa swali.

## Kipindi cha 6

### Funzo

Umuhimu wa burudani

### Shabaha

Mwanafunzi afahamu umuhimu wa burudani.

### Mbinu

Kuwashirikisha wanafunzi katika vikundi kuzungumzia kuhusu umuhimu wa burudani baada ya kuitazama michoro na baadaye kusoma pamoja kifungu katika Kitabu cha Mwanafunzi.

## Utaratibu

### *Hatua ya 1*

Unaweza kuanza somo hili kwa kuwaonyesha wanafunzi video fupi ya burudani fulani kama vile ngoma ya kienyeji. Baada ya hapo, waongoze wanafunzi kujadili yale waliyoyaona kwa kuuliza maswali kama vile:

i) Hii ni burudani gani?
ii) Ni nini faida za burudani?
iii) Umefaidikaje kwa kutazama video (au picha au michoro) hii?
iv) Ungependa kushiriki burudani gani? Kwa nini?

### *Hatua ya 2*

Kwa kutumia vifaa mbalimbali ulivyotayarisha, funza malengo ya sehemu hii. Unaweza kuanza kwa kuwaonyesha wanafunzi picha ya burudani nyinginezo hasa za kienyeji.

Umuhimu wa burudani ni pamoja na:

i) Kuleta umoja na ushirikiano
ii) Tulizo la akili baada ya kazi nyingi au masomo mengi
iii) Kuleta mapato
iv) Kukuza mazoezi ya viungo hivyo basi kuimarisha afya yetu
v) Kuwezesha mshiriki kuzuru kwingi na kujionea ya huko.

### *Hatua ya 3*

Waongoze wanafunzi kusoma kifungu cha habari katika ukurasa wa 81. Unaweza kuanza kwa kuwaongoza kuijadili michoro hiyo iliyomo vitabuni mwao. Baada ya hilo, waelekeze wanafunzi kukisoma kifungu husika. Hakikisha ya kuwa wanafunzi wote wanashiriki.

### *Hatua ya 4*

Waongoze wanafunzi katika kujibu maswali yaliyoulizwa chini ya kifungu husika pamoja na kufanya kazi ya wanafunzi wawili wawili iliyomo vitabuni mwao.

### *Hatua ya 5*

Baada ya kuwaongoza wanafunzi kufanya masahihisho ya majibu yao, waongoze pia katika kufanya muhtasari wa yale wanayoyaona kuwa ya muhimu katika kipindi hiki. Hakikisha kuwa malengo ya kipindi hiki yametimizwa.

### Maadili na mwenendo mwema

Kujenga urafiki pamoja na ushirikiano kwa watu wa rika zote.

### Tathmini

Tathmini uwezo wa mwanafunzi wa kujibu maswali kwa usahihi baada ya kusoma kifungu na kueleza kuhusu umuhimu wa burudani katika vikundi.

### Zoezi la ziada

1. Wanafunzi washiriki katika michezo mbalimbali. Baadhi yao watangaze michezo hiyo moja kwa moja.
2. Wanafunzi washiriki katika mazoezi ya kunyosha viungo kisha wataje umuhimu wa mazoezi hayo.

## Kipindi cha 7

### Funzo

Rejesta ya hotelini

### Shabaha

Kufikia mwishoni mwa kipindi hiki, mwanafunzi aweze:

i) Kutambua sajili ama rejesta ya hotelini
ii) Kubaini msamiati wa rejesta ya hotelini
iii) Kutumia vilivyo msamiati huo wa hotelini katika mawasiliano yake ya kila siku
iv) Kutambua sifa za rejesta ya hotelini.

### Zana na vifaa muhimu kwa kipindi hiki

i) Vifaa halisi vinavyohusiana na hoteli
ii) Kitabu cha Mwanafunzi
iii) Picha ama michoro ya msamiati wa hotelini
iv) Kuwapeleka wanafunzi hotelini na kuwaongoza kujua vilivyomo hotelini humo
v) Vifaa vya wanafunzi wenye mahitaji maalumu.

### Utaratibu

### *Hatua ya 1*

Unaweza kuianza sehemu hii kwa kuwauliza wanafunzi kuhusu rejesta ya jikoni. Kwa mfano:

i) Jiko, kama sehemu ya nyumba, ina umuhimu gani?
ii) Taja baadhi ya vitu vipatikanavyo jikoni mwenu.
iii) Kuna uhusiano gani kati ya jikoni na hotelini?

Kwa msingi huu, wajulishe wanafunzi kuwa lugha ya hotelini hujaa msamiati wa vyakula na vinywaji kama ilivyo lugha ya jikoni.

***Hatua ya 2***

Baada ya utangulizi huo, waongoze wanafunzi kuijua sajili ya hotelini kwa kufunza msamiati wake. Nao msamiati huo ufunzwe kwa zana na vifaa ulivyotayarisha. Iwapo shule iko karibu na hoteli ama mkahawa, wapeleke wanafunzi huko.

**Hatua ya 3**

Waongoze wanafunzi kusoma kifungu cha habari katika Kitabu cha Mwanafunzi, ukurasa wa 82. Baada ya kusoma kifungu, wazungumzie sifa za rejesta ya hotelini kwa kurejelea yaliyomo vitabuni mwao, katika ukurasa wa 83.

***Hatua ya 4***

Waongoze wanafunzi kufanya mazoezi katika sehemu hii. Hakikisha kuwa wote wameshiriki na kutoa majibu sahihi.

**Maadili na mwenendo mwema**

Kujenga urafiki pamoja na ushirikiano kwa watu wa rika zote.

**Tathmini**

Tathmini uwezo wa mwanafunzi wa kutumia lugha ya rejesta ya hotelini katika mawasiliano ya kila siku.

**Zoezi la ziada**

Wanafunzi waigize mazungumzo ya hotelini mbele ya darasa wakizingatia sifa mbalimbali za rejesta ya hotelini.

## Kipindi cha 8 na 9

**Funzo**

Rejesta ya mahakamani (Kitabu cha Mwanafunzi, ukurasa wa 83)

**Shabaha**

Kufikia mwishoni mwa vipindi hivi, mwanafunzi aweze:

i) Kutambua sajili ama rejesta ya mahakamani.
ii) Kutambua sifa za rejesta ya mahakamani.
iii) Kubaini rejesta ya mahakamani kutoka kwa rejesta nyinginezo.
iv) Kutumia vilivyo msamiati wa rejesta ya mahakamani katika mawasiliano yake ya kila siku.

**Zana na vifaa muhimu kwa vipindi hivi**

i) Michoro na picha mbalimbali kama vile hakimu, kizimba, mshukiwa, korokoro, mwendesha mashtaka, na kadhalika.

ii) Vifaa vya wanafunzi wenye mahitaji maalumu
iii) Kesi iliyorekodiwa
iv) Kitabu cha Mwanafunzi.

**Mbinu**

Kuwashirikisha wanafunzi kujadiliana katika vikundi mchoro uliomo katika Kitabu cha Mwanafunzi na kuzungumzia mambo wanayoyajua kuhusiana na mahakama.

## Utaratibu

***Hatua ya 1***

Kwa kuuliza maswali, waongoze wanafunzi kutambua maana ya korti au mahakama. Unaweza kuuliza maswali kama vile:
i) Mhalifu ni nani?
ii) Mojawapo ya kazi za polisi ni nini?
iii) Wahalifu wakishikwa hupelekwa wapi?
iv) Ni nani anayeamua kufungwa au kuwachilia huru washukiwa wa uhalifu?

***Hatua ya 2***

Baada ya kuhakikisha kuwa wanafunzi wako wameelewa maana ya mahakama au korti, waongoze kutambua msamiati unaotumika mahakamani. Unaweza kufanya hivyo kwa kuwachezea rekodi ya kesi mahakamani.

Kumbuka hapa kuwa unaweza kuwapeleka wanafunzi wako mahakamani ili waone yale uliyofunza. Hili linaweza kufanywa kwa mipango ya baadaye au kabla ya kipindi hiki.

***Hatua ya 3***

Katika hatua hii, waongoze wanafunzi kusoma yaliyomo katika Kitabu cha Mwanafunzi, ukurasa wa 83 hadi 85. Unaweza kuwashirikisha wanafunzi wote kwa kuwaelekeza kila mmoja ajisomee au wasome kwa sauti kwa kuigiza yaliyomo kifunguni. Wanafunzi wanaposoma kwa sauti hufaidika zaidi.

***Hatua ya 4***

Baada ya hayo, waelekeze wanafunzi kujibu maswali katika Kitabu cha Mwanafunzi, ukurasa wa 85 na kuyafanyia masahihisho majibu hayo.

***Hatua ya 5***

Hatimaye, unaweza kuwaongoza wanafunzi kuunda muhtasari wa yale yaliyo muhimu katika sehemu hii ili kujua endapo malengo ya kipindi hiki yameafikiwa.

**Suala mtambuka**

Kipindi hiki kinatoa nafasi nzuri ya kujadili mafunzo kuhusu amani na maadili.

**Tathmini**

Tathmini uwezo wa mwanafunzi wa kutumia lugha ya rejesta ya mahakamani katika mawasiliano ya kila siku.

**Majibu ya maswali**

1. Msamiati zaidi wa kimsingi katika rejesta ya mahakamani: mashtaka, ithibati, mshukiwa, wakili, dhamana, mdhamini.
2. Maana na matumizi
   a) mashtaka – malalamiko yaliyopelekwa mahakamani (Mashtaka yote yalisomwa mahakamani na hakimu.)
   b) ithibati – ushahidi unaotolewa mahakamani (Hakimu alitupilia mbali ithibati iliyotolewa dhidi ya mshukiwa.)
   c) mshukiwa – mtu aliyefikishwa mahakamani kwa sababu ya kushukiwa kufanya kosa au makosa fulani (Mshukiwa aliingizwa mahakamani na askari wawili.)
   d) wakili – mtaalamu wa sheria anayewawakilisha watuhumiwa mahakamani (Wakili wake alifaulu kuthibitisha kuwa mshukiwa hakuvunja sheria yoyote.)
   e) dhamana – malipo au ahadi iliyotolewa mahakamani ili kuzuia mshukiwa asipelekwe korokoroni (Nduguye alimtolea dhamana iliyohitajika.)
   f) mdhamini – mtu aliyetoa malipo au ahadi ili mshukiwa asipelekwe korokoroni (Mdhamini wake alichelewa kufika mahakamani.)

## Kipindi cha 9

**Funzo**

Sifa ya rejesta ya mahakamani na maigizo ya mahakamani mbele ya darasa

**Shabaha**

Mwanafunzi aweze kutumia lugha ya rejesta ya mahakamani katika mawasiliano ya kila siku.

**Mbinu**

Kuwashirikisha wanafunzi kuigiza darasani maelezo yaliyotolewa baada ya hatua ya 3 (hapa chini).

## Utaratibu

***Hatua ya 1***

Wanafunzi wazungumzie waliyojifunza katika kipindi kilichopita.

***Hatua ya 2***

Waongoze wanafunzi kutaja sifa mbalimbali za rejesta ya mahakamani. Waongoze kusoma kifungu cha habari katika Kitabu cha Mwanafunzi.

***Hatua ya 3***

Waongoze wanafunzi kuigiza kesi mahakamani.

**Maadili na mwenendo mwema**

Kujenga urafiki pamoja na ushirikiano kwa watu wa rika zote.

**Tathmini**

Tathmini uwezo wa mwanafunzi wa kutumia lugha ya rejesta ya mahakamani katika mawasiliano ya kila siku.

**Zoezi la ziada**

Wasomee wanafunzi maelekezo yafuatayo kisha waigize darasani baadaye.

*Ituze anamiliki shamba kubwa la mahindi. Yeye ni tajiri mkubwa katika kijiji. Kila mara, mahindi huibwa katika shamba lake ila hajui mwizi ni nani.*

*Nziza ni jirani wa Ituze. Ituze anamshuku Nziza kuwa ndiye mwizi japo hana ushahidi. Kina Nziza hawana shamba lolote la mahindi kwao ilhali wao hula mahindi mabichi kila siku. Wao ni maskini. Ituze hujiuliza, je hawa kina Nziza hutoa mahindi wapi?*

*Jioni moja, Nziza alitoka shuleni akiwa na marafiki zake: Ikirezi, Nkusi na Uwase. Walisikia mtu akivunja mahindi shambani mwa Ituze. Nziza aliingia shambani kumfukuza mwizi. Mwizi alitoroka. Alipokuwa akiondoka shambani, Ituze pamoja na Tona, Butera na Hirwa walimwona kwa umbali. Wote walimfuata Nziza hadi kwao. Walipoingia ndani ya nyumba, walipata mahindi mabichi kwenye meza.*

*Ituze aliwapigia polisi simu na wakaja kumshika Nziza. Nziza alifikishwa mahakamani siku iliyofuata kwa tuhuma ya kuiba mahindi shambani mwa Ituze.*

Kama darasa zima, wanafunzi waigize kesi hii. Wanafunzi watatu waigize kama hakimu. Wengine waigize kama mshtaki (Ituze) na mashahidi wake (Tona, Butera na Hirwa). Wengine waigize kama mshtakiwa (Nziza) na mashahidi wake (Ikirezi, Nkusi na Uwase). Pawepo kiongozi wa mashtaka, mawakili, karani wa mahakama, askari na wengineo. Wanafunzi ambao hawatapata nafasi waigize kama marafiki na familia za mshtaki na mshtakiwa. Baadaye, mahakimu wasome maamuzi yao kivyao.

**Maadili na mwenendo mwema**

Kujenga urafiki pamoja na ushirikiano kwa watu wa rika zote.

**Tathmini**

Tathmini uwezo wa mwanafunzi wa kutumia lugha ya rejesta ya mahakamani katika mawasiliano ya kila siku.

## Kipindi cha 10 na 11

**Funzo**

Rejesta ya bungeni

**Shabaha**

Kufikia mwishoni mwa vipindi hivi, mwanafunzi aweze:

i) Kuitambua rejesta au sajili ya bungeni.
ii) Kubaini rejesta ya bungeni kutoka kwa rejesta nyinginezo.
iii) Kutumia vilivyo lugha ya rejesta ya bungeni katika mawasiliano yake na watu wengine.
iv) Kubaini sifa za rejesta ya bungeni.

**Zana na vifaa muhimu kwa vipindi hivi**

i) Vifaa vya wanafunzi wenye mahitaji maalumu
ii) Michoro ama picha za matukio bungeni
iii) Video ama rekodi ya sauti za mambo yanavyoendelea bungeni
iv) Kitabu cha Mwanafunzi
v) Ziara ya wanafunzi bungeni.

**Mbinu**

Kuwashirikisha wanafunzi kusoma na kuigiza mazungumzo ya kifungu kilichomo katika Kitabu cha Mwanafunzi.

## Utaratibu

***Hatua ya 1***

Anza somo hili kwa kuuliza maswali ya kurudia yale uliyoyafunza katika kipindi kilichopita. Ni sharti wanafunzi waweze kueleza vilivyo sajili pamoja na mengi yanayoihusu.

***Hatua ya 2***

Baada ya utangulizi huo, tumia vifaa mbalimbali ulivyovitayarisha kufunza maana ya bunge. Kwa mfano, unaweza kuonyesha picha ya spika wa bunge akiendesha shughuli za bunge na kuwaongoza wanafunzi katika kuijadili.

***Hatua ya 3***

Baada ya hayo, waongoze wanafunzi kuzitambua wazi wazi sifa za rejesta hii ya bungeni. Unaweza kufanya hivyo kwa kuchezesha mjadala uliorikodiwa bungeni kisha wanafunzi wataje mambo muhimu kutokana na mjadala huo.

***Hatua ya 4***

Waongoze wanafunzi kusoma sehemu hii iliyomo vitabuni mwao. Hakikisha ya kuwa umewashirikisha wanafunzi wote.

***Hatua ya 5***

Waelekeze wanafunzi katika kujadili sifa mbalimbali za rejesta ya bungeni.

***Hatua ya 6***

Waongoze wanafunzi kujibu mazoezi ya sehemu hii pamoja na kuyafanyia masahihisho majibu yao.

***Hatua ya 7***

Waongoze wanafunzi katika kuunda muhtasari wa yale yaliyo muhimu ambayo wamejifunza katika sehemu hii.

**Maadili na mwenendo mwema**

Kujenga urafiki pamoja na ushirikiano kwa watu wa rika zote.

**Tathmini**

Tathmini uwezo wa mwanafunzi wa kutumia lugha ya rejesta ya bungeni katika mawasiliano ya kila siku.

**Majibu ya zoezi**

Msamiati maalumu wa bungeni uliotumiwa katika kifungu ni kama vile:

1. bunge – baraza la taifa lililo na wajumbe waliochaguliwa na watu na linalotunga sheria (Bunge limepitisha sheria nyingi.)
2. mbunge – mtu aliyechaguliwa na wananchi ili kuwawakilisha bungeni (Mbunge wetu huchangia sana mijadala ya bungeni.)
3. spika – kiongozi wa majadiliano bungeni (Spika alimruhusu mbunge achangie mjadala bungeni.)
4. naibu wa spika – msaidizi wa spika bungeni (Naibu wa spika alifungua kikao cha bunge kwa niaba ya spika.)
5. sheria – kanuni zilizotungwa na bunge la nchi na kuidhinishwa na rais (Wazalendo hujivunia kutii sheria za nchi yao.)
6. eneo la ubunge – eneo la uwakilishi bungeni; huwakilishwa na mbunge (Eneo la bunge lilipiga hatua za kimaendeleo chini ya mbunge huyo.)
7. piga kura – utaratibu wa kuamua jambo bungeni (Wabunge watapiga kura leo alasiri.)
8. hoja – pendekezo katika bunge (Hoja ya mbunge huyo ilipingwa na wabunge wengi.)
9. idhinisha – ruhusu jambo fulani lifanyike (Rais ameidhinisha sheria nyingine.)
10. teua – chagua (Spika hawezi kumteua naibu wa spika wake.)
11. kuwakilisha – kuenda mahali kwa niaba ya mtu au watu wengine (Kuwakilisha wananchi bungeni ni wajibu wa mbunge.)
12. kura ya kutokuwa na imani – kupiga kura ili kutokubali wazo au mtu fulani (Wabunge walitishia kuitisha kura ya kutokuwa na imani na spika wa bunge.

## Kipindi cha 11

### Funzo

Maigizo ya bungeni

### Shabaha

Mwanafunzi aweze kutumia lugha ya rejesta ya bungeni katika mawasiliano ya kila siku.

### Mbinu

Kuwashirikisha wanafunzi kuigiza mazungumzo ya bungeni.

## Utaratibu

***Hatua ya 1***

Wanafunzi wazungumzie mambo muhimu waliyojifunza katika kipindi kilichotangulia.

***Hatua ya 2***

Wanafunzi wataje sifa za rejesta ya bungeni huku wakitoa mifano.

***Hatua ya 3***

Geuza darasa liwe bunge. Wanafunzi waigize kama wabunge kutoka upande wa upinzani na upande wa serikali. Pia, pawepo wabunge maalumu na mawaziri. Pawepo spika, makarani wa bunge pamoja na maafisa wengineo wanaopatikana bungeni.

Waziri mmoja alete mswada bungeni unaopendekeza sheria mpya dhidi ya wawindaji haramu au hoja yoyote utakayopendekeza au wanafunzi wanaweza kujichagulia hoja yao. Hoja hiyo iwe hoja inayofahamika vizuri miongoni mwa wanafunzi wako.

Wajadili hoja hiyo kwa kuzingatia rejesta ya bungeni.

### Maadili na mwenendo mwema

Kujenga urafiki pamoja na ushirikiano kwa watu wa rika zote.

### Tathmini

Tathmini uwezo wa mwanafunzi wa kutumia lugha ya rejesta ya bungeni katika mawasiliano ya kila siku.

## Kipindi cha 12

### Funzo

Rejesta ya sokoni

### Shabaha

Kufikia mwishoni mwa kipindi hiki, mwanafunzi aweze:

i) Kutambua rejesta ya sokoni.
ii) Kubaini msamiati wa rejesta ya sokoni.
iii) Kutumia vilivyo msamiati huo wa sokoni katika mawasiliano yake ya kila siku.
iv) Kutambua sifa za rejesta ya sokoni.

**Zana na vifaa muhimu kwa kipindi hiki**

i) Kitabu cha Mwanafunzi
ii) Picha ama michoro ya wauzaji, wanunuzi na bidhaa sokoni
iii) Kuwapeleka wanafunzi sokoni na kuwaongoza kuufahamu msamiati utumiwao huko
iv) Vifaa vya wanafunzi wenye mahitaji maalumu.

**Mbinu**

Kuwashirikisha wanafunzi kusoma katika vikundi kifungu na kuigiza mazungumzo ya kifungu kilichomo katika Kitabu cha Mwanafunzi.

## Utaratibu

***Hatua ya 1***

Waongoze wanafunzi kuijua rejesta ya sokoni kwa kuwaonyesha picha mbalimbali za sokoni kisha wazizungumzie. Unaweza kuwauliza wanafunzi majina ya watu waliomo kwenye picha na shughuli wanazofanya. Wanafunzi nao wazungumzie wanayofahamu kuhusu sokoni.

***Hatua ya 2***

Waongoze wanafunzi wako kuisoma yaliyomo chini ya rejesta ya sokoni katika Kitabu cha Mwanafunzi.

***Hatua ya 3***

Waongoze wanafunzi kufahamu sifa za rejesta hii ya sokoni kabla ya kuwaelekeza kujibu mazoezi yote ya sehemu hii. Wanapokuwa wanajibu ama baada ya kumaliza kuyajibu, wasaidie katika kusahihisha majibu yao.

***Hatua ya 4***

Waongoze wanafunzi kusema kwa ufupi mambo muhimu waliyojifunza katika kipindi hiki. Hakikisha kuwa malengo ya kipindi yametimizwa.

**Maadili na mwenendo mwema**

Kujenga urafiki pamoja na ushirikiano kwa watu wa marika yote.

**Tathmini**

Tathmini uwezo wa mwanafunzi wa kutumia lugha ya rejesta ya kanisani katika mawasiliano ya kila siku.

**Zoezi la ziada**

Kwa kutumia vifaa vilivyopo darasani kama bidhaa, wanafunzi washiriki katika mazungumzo kati ya wauzaji na wanunuzi wakizingatia sifa za lugha ya sokoni.

**Majibu ya zoezi**

1. Maana ya maneno
   a) mia bei – bei ni faranga (au pesa zinazotumika) mia moja
   b) mteja - mnunuzi
   c) bei rahisi – bei ya chini au nafuu
   d) bidhaa – vitu vinunuliwavyo au kuuzwa
   e) bei ghali – bei ya juu
   f) faida – pato linalobaki baada ya kutoa gharama zote
2. Msamiati katika sentensi
   a) "Mia bei! Mia bei!" wanabiashara walitangaza sokoni.
   b) Mteja alimuomba mwanabiashara ampunguzie bei.
   c) Tulinunua matunda kwa bei rahisi katika soko hilo.
   d) Duka la Ingabire limejaa bidhaa kutoka viwanda mbalimbali.
   e) Uhaba wa matunda umesababisha yauzwe kwa bei ghali.
   f) Biashara ya mazao ya kilimo ina faida kubwa.

## Kipindi cha 13

### Funzo

Rejesta ya kanisani

### Shabaha

Kufikia mwishoni mwa kipindi hiki, mwanafunzi aweze:

i) Kutambua rejesta ama sajili ya kanisani.
ii) Kubaini rejesta ya kanisani.
iii) Kuzibaini sifa za rejesta ya kanisani.
iv) Kutumia vilivyo lugha ya rejesta ya kanisani katika mawasiliano yake ya kila siku.

**Zana na vifaa muhimu kwa kipindi hiki**

i) Kitabu cha Mwanafunzi.
ii) Michoro ama picha za msamiati wa kanisani kama vile: Biblia, kasisi, waumini, piano, kwaya, n.k.
iii) Kanda ya ibada iliyorekodiwa.
iv) Vifaa vya wanafunzi wenye mahitaji maalumu.

**Mbinu**

Kuwashirikisha wanafunzi kuzungumzia kuhusu rejesta ya lugha ya kanisani kwa kuujadili mchoro katika vikundi kabla ya kusoma kifungu katika Kitabu cha Mwanafunzi.

## Utaratibu

***Hatua ya 1***

Waongoze wanafunzi kutaja na kuzungumzia dini na madhehebu yao. Unaweza kuuliza:

i) Unashiriki katika dini gani?

ii) Ipo tofauti gani kati ya dini na dhehebu?

iii) Mambo gani hufanyika ibadani?

***Hatua ya 2***

Baada ya utangulizi huo, waongoze wanafunzi kutambua sajili ya sehemu hii kabla ya kuanza kufunzia msamiati wake. Nao msamiati huo ufunzwe kwa zana na vifaa ulivyotayarisha. Iwapo shule ina kanisa, basi unaweza kuwapeleka wanafunzi huko na kufunza kwa vifaa halisi.

***Hatua ya 3***

Waongoze wanafunzi kufanya kazi ya vikundi iliyomo vitabuni mwao.

***Hatua ya 4***

Baada ya hayo, waongoze wanafunzi kusoma kifungu cha sehemu hii katika Kitabu cha Mwanafunzi.

***Hatua ya 5***

Waongoze wanafunzi ili wafahamu sifa za rejesta hii ya kanisani na hatimaye wasaidie kufanya muhtasari wa yaliyo muhimu katika kipindi hiki.

***Hatua ya 6***

Waelekeze wanafunzi kulifanya zoezi la sehemu hii huku ukiwaongoza katika huko kujadiliana kwao.

**Maadili na mwenendo mwema**

Kujenga urafiki pamoja na ushirikiano kwa watu wa marika yote.

**Tathmini**

Tathmini uwezo wa mwanafunzi wa kutumia lugha ya rejesta ya kanisani katika mawasiliano ya kila siku.

**Zoezi la ziada**

1. Wanafunzi wazungumzie sifa za ibadani wanamoshiriki kama vile msikitini, kanisani na kadhalika.
2. Wanafunzi wataje umuhimu wa dini katika jamii.

**Majibu ya zoezi**

Waelekeze wanafunzi wajadili msamiati ufuatao huku wakiangalia maana yake katika kamusi ya lugha sanifu: kanisa, imani, Amri kumi za Mungu, dini ya kweli, Mwenyezi Mungu, Neno, Biblia, Mitume, malaika, misahafu, kutubu, pekee, dhambi, Mola, makasisi, mapadri, wachungaji, maaskofu, maaskofu wakuu, jukumu, Manani, wanamwabudu, sala, mwovu shetani, malaika mbinguni, jahanamu, kuangamia mtoni, kuingia mbinguni, njia pana, njia nyembamba, msalaba wa Yesu, Mwokozi Yesu, Utata wa Uungu, siku ya kiama, kuungama dhambi. Baadhi ya msamiati kama vile Mwenyezi Mungu, mitume, malaika, dhambi, sala, siku ya kiama, kutubu hutumia pia katika misikiti.

## Kipindi cha 14

### Funzo

Rejesta ya sarufi ya Kiswahili

### Shabaha

Kufikia mwishoni mwa kipindi hiki, mwanafunzi aweze:

i) Kutambua maana ya sarufi.
ii) Kutambua rejesta ya sarufi ya Kiswahili.
iii) Kutumia vilivyo lugha ya rejesta ya sarufi ya Kiswahili katika mawasiliano yao ya kila siku.
iv) Kuzibaini sifa za rejesta ya sarufi ya Kiswahili.

**Zana na vifaa muhimu kwa kipindi hiki**

i) Kitabu cha Mwanafunzi.
ii) Vitabu vinginevyo vya sarufi.
iii) Kanda za sarufi iliyorekodiwa.
iv) Vifaa vya wanafunzi wenye mahitaji maalumu.

### Mbinu

Kuwashirikisha wanafunzi kuzungumzia kuhusu rejesta ya lugha ya Kiswahili sanifu kwa kusoma kifungu katika Kitabu cha Mwanafunzi.

## Utaratibu

### *Hatua ya 1*

Unaweza kuanza hapa kwa kuwauliza wanafunzi maswali ya kurudia yale waliyojifunza katika kipindi kilichopita yakiwa pamoja na maana ya rejesta.

***Hatua ya 2***

Waulize wanafunzi kukueleza maana ya rejesta ya sarufi ya Kiswahili kwa msingi wa yale waliyoyafanya katika hatua ya kwanza hapo juu.

***Hatua ya 3***

Funza maana ya baadhi ya maneno ya sajili hii kwa kutumia vifaa ulivyonavyo.

***Hatua ya 4***

Waongoze wanafunzi kusoma sehemu hii iliyomo vitabuni mwao. Unaweza kuanza na kazi ya vikundi ambapo utawaongoza wanafunzi kuujadili mchoro uliopo kwenye sehemu hii kama utangulizi wa masomo yao.

***Hatua ya 5***

Waongoze wanafunzi kusoma kifungu katika Kitabu cha Mwanafunzi, kama njia mojawapo ya kutilia mkazo yale uliyofunza hapo awali.
Baada ya hayo, waongoze wanafunzi katika kufahamu sifa za rejesta ya sarufi ya Kiswahili.

***Hatua ya 6***

Waongoze wanafunzi katika majadiliano yao ya zoezi walilopewa.

**Suala mtambuka**

Somo hili linatoa nafasi nzuri ya kuzungumzia mafunzo kuhusu usawa wa jinsia.

**Tathmini**

Tathmini uwezo wa mwanafunzi wa kutumia lugha ya rejesta ya Kiswahili sanifu katika mawasiliano ya kila siku.

**Zoezi la ziada**

Wanafunzi wafanye utafiti zaidi kuhusu istilahi zinazotumika katika sarufi ya Kiswahili pamoja na maana ya istilahi husika. Pia, watoe mifano.

**Majibu ya zoezi**

1. Mtungo au insha – maelezo au masimulizi yaliyoandikwa kwa lugha ya mtiririko (Ndahiro ameandika insha ya kupendeza./Ndahiro ameandika mtungo wa kupendeza.)
2. Msamiati – jumla ya maneno katika lugha fulani (Mwalimu aliwashauri wanafunzi wasiutumie msamiati ikiwa hawajui maana yake.)
3. Rejesta – lugha inayotumiwa katika mazingira fulani (Tumesoma rejesta mbalimbali katika somo la Kiswahili.)
4. Vitendawili – fumbo linalotegwa ili liteguliwe (Kila lugha ina vitendawili vyake.)
5. Methali – usemi wa kimapokeo unaowasilisha ukweli fulani (Methali zina maana ya juu na maana fiche.)
6. Msemo – fungu la maneno au kauli inayowasilisha ukweli fulani katika maisha ya jamii. (Misemo ya lugha huwasilisha ukweli usiopingika.)

7. Nahau – fungu la maneno lenye maana maalumu isiyotokana na maana za kawaida za maneno hayo. Nahau zilizotumiwa zimeifanya hadithi ipendeze.
8. Mafumbo ni semi za maonyo au mawaidha ambazo maana zake za ndani zimefichika. (Wazee wengi hupenda kuongea kwa mafumbo.)
9. Barua – Maandishi yenye ujumbe ambayo huandikwa ili yasomwe na mtu aliyelengwa. (Barua aliyoniandikia mjomba niliisoma kwa furaha kubwa.)
10. Masimulizi – aina ya utanzu wa fasihi unaohusu usimuliaji wa mambo fulani.
11. Dhahania – mambo ya kufikirika (Baridi ni nomino dhahania.)
12. Istilahi – maneno maalumu yanayotumiwa katika taaluma fulani (Sarufi ya lugha ina istilahi zake.)
13. Kiimbo – kupanda na kushuka kwa sauti wakati wa kuzungumza (Kila lugha ina utaratibu wake wa kiimbo.)

**Majibu ya zoezi la ziada**

| | Kifungu | Rejesta na watu wanaozungumza | Sifa za rejesta na mfano wa msamiati wake |
|---|---|---|---|
| a) | Mtu I: Wapi menu?<br>Mtu II: Hii hapa.<br>Mtu I: Nipe chai tano, na matoke nne.<br>Mtu II: (*Kwa MTU III*) Wewe?<br>Mtu III: Mimi isombe. | Hotelini<br>Mtu I na III: Wateja<br>Mtu II: Mhudumu | 1. Matumizi ya lugha isiyokuwa rasmi. Mfano: chai moja, mimi isombe<br>2. Matumizi ya msamiati maalumu wa chakula. Mfano: matoke<br>3. Kuchanganya lugha: Mfano: wapi menu? |
| b) | Mtu I: Ulianza kuhisi maumivu ya tumbo lini?<br>Mtu II: Siku mbili zilizopita.<br>Mtu I: Ulikula nini?<br>Mtu II: Siku hiyo nilikunywa tu maji.<br>Mtu I: Maji hayo yalichemshwa?<br>Mtu II: Hapana.<br>Mtu I: Maji hayo yalitiwa dawa?<br>Mtu II: Hapana.<br>Mtu I: Umemeza dawa gani?<br>Mtu II: Asprin.<br>Mtu I: Kuna mkurupuko wa cholera. Chukua karatasi hii. Enda kwenye maabara ufanyiwe uchunguzi kisha urudi ikuandikie dawa. | Hospitalini<br>Mtu I: Daktari<br>Mtu II: Mgonjwa | 1. Kuulizwa ulizwa maswali: ulianza kuugua lini?...ulikula nini?...maji hayo yalichemshwa na kadhalika.<br>2. Msamiati wa dawa: *Asprin*<br>3. Msamiati wa magonjwa: *cholera*<br>4. Mgonjwa kupewa maagizo: enda *kwenye maabara*...<br>(Kubali majibu mengineyo sahihi) |

| | | | |
|---|---|---|---|
| c) | Mwandishi: Vijana wawili wavumbua dawa mpya ya kuwaulia wadudu wanaoharibu sukumawiki.<br>Jane Usanase, 15, na Paul Ngabo, 14, washangaza wakazi wa wilaya ya Karongi kwa kuvumbua dawa mpya ya kuulia wadudu wanaoharibu sukumawiki. Akionyesha furaha yake, mkuu wa wilaya hiyo Bwana Ndoli aliwapongeza vijana hao kwa kutumia maarifa waliyopata darasani kusaidia jamii zao.<br>“Hii ni changamoto kwa vijana waliopo shuleni. Usisome tu kwa ajili ya kupita mtihani. Tumia maarifa hayo kuleta mabadiliko katika jamii,” alisema Bwana Ndoli.<br>Vijana hao walipokea tuzo nyingi kutoka kwa wakulima. Walionyesha furaha zao na kuahidi kufanya tafiti zaidi.<br>“Sisi tunapenda sana masomo ya Kilimo na Sayansi. Tuliamua kutumia maarifa tuliyopata katika somo la Kemia kutafitia dawa hizi,” alisema Usanase.<br>Vijana hao wanatarajiwa kukutana na rais katika ikulu siku ya Jumamosi. | Habari magazetini<br>Mwandishi: mwanahabari | 1. Kutumiwa kwa wakati usiodhihirika: wavumbua... washangaza...<br>2. Maelezo ya kina kama vile umri na majina ya wahusika: Jane Usanase, 15, na Paul Ngabo, 14<br>3. Matumizi ya sentensi ndefu ndefu: Vijana wawili wavumbua dawa mpya ya kuwaulia wadudu wanaoharibu sukumawiki.<br>4. Kunukuliwa kwa msemaji<br>(Kubali majibu yoyote mengineyo sahihi) |
| d) | Mtu I: Kiranja yu wapi?<br>Mtu II: Hajakuja leo. Aliomba ruhusa!<br>Mtu I: Akija kesho, mwambie anione ofisini. Mmoja wenu afute ubao. Mwingine aniletee chaki kutoka ofisini. | Darasani<br>Mtu I: Mwalimu<br>MtuII: Mwanafunzi | 1. Lugha ya kuamuru kwa upande wa mwalimu: ...*afute ubao... harakisha*<br>2. Lugha ya heshima kwa upande wa mwanafunzi: tafadhali, *naomba*... *Asante*... |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | Mtu I: Tafadhali, naomba kuenda msalani.<br>Mtu II: Haya! Harakisha, ninaanza kipindi sasa hivi.<br>Mtu I: Asante. | | 3. Msmiati maalumu: *kiranja, ubao na kadhalika*.<br>4. Lugha ya tasfida: msalani<br>(*Kubali majibu mengineyo sahihi*) |
| e) | Mzungumzaji: Sote tunafaa kumshukuru Mola kwa kutupa uhai ili kufika hapa kumwabudu. Imeandikwa katika Kitabu Kitakatifu kuwa sisi sote ni wageni hapa duniani na tunaishi ili tumwabudu Mwenyezi Mungu na kufanya mapenzi yake. Wale ambao watakiuka mapenzi yake watachomwa na moto wa jehanamu. | Kanisani/msikitini<br>Mzungumzaji: Kasisi/mchungaji/ shehe | 1. Kutajwa kwa majina ya Mungu kwa heshima: *Mola, Mwenyezi Mungu*<br>2. Kurejelewa kwa vifungu katika vitabu takatifu: Imeandikwa *katika Kitabu Kitakatifu kuwa...*<br>(*Kubali majibu mengineyo sahihi*) |

## Kipindi cha 15,16 na 17

### Funzo

Majina ya ngeli ya KI-VI katika umoja na wingi

### Shabaha

Kufikia mwishoni mwa vipindi hivi, mwanafunzi aweze:

i) Kuyatambua majina ya ngeli ya KI-VI.
ii) Kubaini umoja na wingi wa ngeli hii.
iii) Kutumia majina ya ngeli ya KI-VI kutungia sentensi katika umoja na wingi.

**Zana na vifaa muhimu kwa vipindi hivi**

i) Picha na michoro mbalimbali ya vitu ambavyo majina yavyo yapo katika ngeli hii.
ii) Vifaa vya wanafunzi wenye mahitaji maalumu
iii) Vifaa halisi
iv) Kitabu cha Mwanafunzi
v) Kadi

**Mbinu**

Mhadhara pamoja na kuwashirikisha wanafunzi katika kuzungumzia nomino za ngeli ya KI-VI.

## Kipindi cha 15

**Funzo**

Maelezo kuhusu ngeli ya KI-VI na mifano ya majina mbalimbali katika ngeli hii

### Utaratibu

***Hatua ya 1***

Unaweza kuanza kufundisha hapa kwa kurudia mojawapo ya ngeli ulizofunza hapo awali. Katika kuirudia ngeli huko, ni sharti wataje majina yake kwa umoja na wingi.

***Hatua ya 2***

Waongoze wanafunzi kutambua majina ya ngeli hii ya KI-VI katika hali ya umoja na wingi pamoja na maana ya kila jina. Mbinu mojawapo unayoweza kutumia ni ile ya kadi na vifaa halisi. Kwa mfano, waonyeshe wanafunzi kifaa halisi kama vile kijiko, tamka jina hilo, nao wanafunzi walitamke. Waonyeshe vijiko viwili, tamka jina nao wanafunzi walitamke. Waulize maana na wakikosea uwarekebishe.

***Hatua ya 3***

Waongoze wanafunzi kusoma mifano ya majina ya vitu mbalimbali katika ngeli ya KI-VI kuanzia ukurasa wa 97 hadi 99 kwenye Kitabu cha Mwanafunzi.

Wakimaliza, waelekeze kuyafanya mazoezi yote yaliyotolewa.

Baada ya hayo, wasaidie wanafunzi kufanya masahihisho ya majibu yale yaliyoandikwa.

***Hatua ya 4***

Waongoze wanafunzi kufanya muhtasari wa yale yaliyo muhimu katika kipindi hiki na kuyaandika madaftarini mwao.

**Suala mtambuka**

Somo hili linatoa nafasi nzuri ya kuzungumzia mafunzo kuhusu usawa wa jinsia.

**Tathmini**

Tathmini uwezo wa mwanafunzi wa kubaini nomino za ngeli ya KI-VI na kuzitungia sentensi sahihi.

**Majibu ya zoezi**

Majina kumi ya ngeli ya KI-VI: kitanda – vitanda, kijiko – vijiko, kijiti – vijiti, kisa – visa, kiwiko – viwiko, kicheko – vicheko, kichana – vichana, kifungo – vifungo, kizibo – vizibo, kiti – viti.

**Majina kutokana na vitenzi**

1. apa – kiapo – viapo
2. piga – kipigo – vipigo
3. nyoa – kinyozi – vinyozi
4. levya – kileo – vileo
5. vuka – kivuko – vivuko
6. tukia – kituko – vituko
7. tiba – kitibi – vitibi
8. tua – kituo – vituo
9. kwaza – kikwazo – vikwazo

**Majina yanayoanza kwa Ki- lakini hayachukui wingi**

1. kiwi
2. kiu
3. kilo
4. Kingwana
5. Kina

**Majina ya vitu katika hali ya udogo**

1. kijiti – vijiti
2. kijinga – vijinga
3. kijisu – vijisu
4. kibahasha – vibahasha
5. kijitabu – vijitabu

## Kipindi cha 16

### Funzo

Matumizi ya majina ya ngeli ya KI-VI (Kitabu cha Mwanafunzi, ukurasa wa 100)

## Utaratibu

### *Hatua ya 1*

Unaweza kuianza sehemu hii kwa kuwaongoza wanafunzi kukumbuka yale yaliyofunzwa katika kipindi kilichopita.

Baada ya hayo, unaweza kutumia baadhi ya vifaa ulivyotumia katika kipindi kilichopita. Mathalan, chukua kikombe na kijiko na uige kukoroga ili kufunza matumizi ya vifaa hivyo. Unaweza kusema:

i) Ninakoroga kwa kijiko.
ii) Kikombe kina chai.

Kwa mtindo huu, funza kwanza matumizi ya maneno ya vifaa vya kushikika kabla ya kufunza yale ya majina kama vile kiwango, kilio na kadhalika.

***Hatua ya 2***

Waongoze wanafunzi katika kuisoma sehemu hii iliyomo vitabuni mwao kuanzia ukurasa wa 100-101 .

***Hatua ya 3***

Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la sehemu hii pamoja na kazi ya wanafunzi wawili wawili.

**Suala mtambuka**

somo hili linatoa nafasi nzuri ya kujadili mafunzo kuhusu amani na maadili.

**Majibu ya zoezi**

1. Mwanafunzi aeleze kutokana na jinsi alivyoelewa.
2. i) huchukua vy- katika wingi (vyombo)
   ii) huchukua vi- katika wingi (vioo)
   iii) huchukua vi- katika wingi (viti)
   iv) huchukua vy- katika wingi (vyeo)
3. i) Vy- vi- -vi
   ii) Ki- ki-
   iii) Ki- ki-
   iv) Vi- vi-
   v) Vy- vi-
   vi) Ch- ki
4. iii) Si sahihi Kiswahili kinazungumzwa Afrika Mashariki.
   iv) Sahihi
   v) Si sahihi Kitoto kinaruka.
   vi) Si sahihi Kijiti kimevunjika.
   vii) Sahihi
   viii) Si sahihi Vyuma vinachomwa.
   ix) Si sahihi Vigelegele vinasikika.

## Kipindi cha 18 na 19

### Funzo

Matumizi ya majina ya ngeli ya KI- VI na vivumishi (Kitabu cha Mwanafunzi,

**Shabaha**

Kufikia mwishoni mwa kipindi hiki, mwanafunzi aweze:
Kutumia vilivyo majina ya ngeli ya KI-VI pamoja na vivumishi mbalimbali.

**Zana na vifaa muhimu kwa kipindi hiki**

i) Michoro, picha na vifaa halisi vya kutungiwa sentensi
ii) Vifaa vya wanafunzi wenye mahitaji maalumu
iii) Kitabu cha Mwanafunzi
iv) Kadi.

**Mbinu**

Mhadhara pamoja na kuwashirikisha wanafunzi katika kutumia majina ya ngeli ya KI-VI pamoja na vivumishi husika katika sentensi.

## Kipindi cha 18

**Funzo**

Matumizi ya majina ya ngeli ya KI- VI na vivumishi vya sifa, vivumishi vya pekee na vivumishi vionyeshi.

## Utaratibu

***Hatua ya 1***

Unaweza kuianza sehemu hii kwa kuwaongoza wanafunzi kukumbuka yale uliyofunza katika kipindi kilichopita.

Halafu, unaweza kutumia baadhi ya vifaa ulivyotumia katika kipindi hicho kilichopita pamoja na vivumishi ambata. Mathalan, chukua kikombe safi na kingine kichafu na utunge sentensi kama vile:

i) Kikombe safi kinapendeza.
ii) Vikombe safi vinapendeza.
iii) Kikombe kichafu kinasafishwa.
iv) Vikombe vichafu vinasafishwa.

Kwa mtindo huu, funza kwanza matumizi ya maneno ya vifaa vya kushikika ndipo ufunze yale ambayo hayashikiki.

***Hatua ya 2***

Waongoze wanafunzi kusoma na kujadili yaliyomo vitabuni mwao. Waongoze kufanya mazoezi ya kila sehemu huku ukisahihisha majibu yao. Hapa, badala ya wanafunzi kusoma kwanza ndipo warudie kufanya mazoezi, itakuwa vizuri zaidi wakiifanyia kila sehemu zoezi lake kabla ya kuenda katika sehemu inayofuata.

#### *Hatua ya 3*

Waongoze wanafunzi kuandika muhtasari wa sehemu hii.

#### Tathmini

Tathmini uwezo wa mwanafunzi wa kutumia majina ya ngeli ya KI-VI pamoja na vivumishi husika katika sentensi sahihi.

## Kipindi cha 19

#### Funzo

Matumizi ya majina ya ngeli ya KI- VI na vivumishi vya idadi, vivumishi vya kuuliza na vivumishi vimilikishi.

#### Shabaha

Mwanafunzi aweze kutumia kwa usahihi majina ya ngeli ya KI-VI na vivumishi vya idadi, vivumizi viulizi na vivumishi vimilikishi.

#### Mbinu

Mhadhara pamoja na kuwashirikisha wanafunzi katika kutumia majina ya ngeli ya KI-VI pamoja na vivumishi husika katika sentensi.

### Utaratibu

#### *Hatua ya 1*

Unaweza kuianza sehemu hii kwa kuwaongoza wanafunzi kukumbuka yale uliyofunza katika kipindi kilichopita.

Halafu, unaweza kutumia baadhi ya vifaa ulivyotumia katika kipindi hicho kilichopita pamoja na vivumishi ambata. Mathalan, chukua vifutio viwili na uwaulize: Vifutio hivi ni vingapi? Na kadhalika.

Kwa mtindo huu, funza kwanza matumizi ya maneno ya vifaa vya kushikika ndipo ufunze yale ambayo hayashikiki.

#### *Hatua ya 2*

Waongoze wanafunzi kusoma na kujadili yaliyomo katika vitabuni mwao. Waongoze kufanya mazoezi ya kila sehemu huku ukisahihisha majibu yao.

#### *Hatua ya 3*

Waongoze wanafunzi kuandika muhtasari wa sehemu hii.

**Suala mtambuka**

Somo hili linatoa nafasi nzuri ya kujadili mafunzo kuhusu desturi ya usanifishaji na ujasiriamali. kutokana na mazungumzo ya wauzaji na wateja

**Tathmini**

Tathmini uwezo wa mwanafunzi wa kutumia majina ya ngeli ya KI-VI pamoja na vivumishi husika katika sentensi sahihi.

**Majibu ya Mazoezi**

**Sentensi za majina ya KI-Vi pamoja na vivumishi vya pekee**

1. Kichupa chenye dawa kimevunjika. (Vichupa vyenye dawa vimevunjika.)
2. Kizibo chenyewe kimekazwa. (Vizibo vyenyewe vimekazwa.)
3. Chumba chote kimepakwa rangi. (Vyumba vyote vimepakwa rangi.)
4. Kinywaji chochote kitanunuliwa. (Vinywaji vyovyote vitanunuliwa.)
5. Kicheko kingine kimezuka. (Vicheko vingine vimezuka.)

**Sentensi za majina ya KI-Vi pamoja na vivumishi vionyeshi**

1. Kisa hiki hakijasimuliwa. (Visa hivi havijasimuliwa.)
2. Kikwazo hicho ni kipya. (Vikwazo hivyo ni vipya.)
3. Kitambaa kile kinapendeza sana. (Vitambaa vile vinapendeza sana.)
4. Kichana hiki cha Kanyana kimeoshwa. (Vichana hivi vya Kanyana vimeoshwa.)
5. Kidimbwi hicho kimekauka. (Vidimbwi hivyo vimekauka.)

**Sentensi za majina ya KI-Vi pamoja na vivumishi vya idadi**

1. Vyumba viwili vilipakwa rangi.
2. Vitabu sita vimenunuliwa.
3. Vitanda kumi vitatayarishwa.
4. Vioo vingi vimehamishwa.
5. Visa vichache vinapendeza.

**Sentensi za majina ya KI-Vi pamoja na vivumishi viulizi**

1. Kiatu kipi kimeshonwa? (Viatu vipi vimeshonwa?)
2. (Vitambaa vingapi vinapendeza?)
3. Kitabu gani kimesomwa? (Vitabu gani vimesomwa?)
4. Kikwazo kipi kilikiukwa? (Vikwazo vipi vilikiukwa?)
5. (Visa vingapi vitaandikwa?)

**Sentensi za majina ya KI-Vi pamoja na vivumishi vimilikishi**

1. Kibeti chake kimepatikana. (Vibeti vyao vimepatikana.)
2. Choo changu kimejengwa. (Vyoo vyetu vimejengwa.)
3. Kisa chako kimesomwa. (Visa vyenu vimesomwa.)
4. Kiberiti changu kimeanguka majini. (Viberiti vyetu vimeanguka majini.)
5. Kidole chake kitapakwa dawa. (Vidole vyao vitapakwa dawa.)

## Kipindi cha 20

### Funzo

Maswali ya marudio (Kitabu cha Mwanafunzi.)

**Shabaha**

Kufikia mwishoni mwa kipindi hiki, mwanafunzi aweze:
Kujitathmini na kuona kama ameyaelewa vilivyo yote waliyofunzwa katika sura hii.

**Zana na vifaa muhimu kwa kipindi hiki**

i) Kitabu cha Mwanafunzi.

**Mbinu**

Kujibu maswali ya marudio madaftarini na baadaye kusahihisha majibu ya mwanafunzi.

## Utaratibu

***Hatua ya 1***

Baada ya kuwapongeza wanafunzi na kuwatia ari ya kutaka kujifunza mengi zaidi kuhusu lugha hii, waongoze kujibu maswali ya sehemu hii.

***Hatua ya 2***

Waongoze wanafunzi kusahihisha majibu yao ya sehemu hii. Wanaweza kubadilishana madaftari yao na kusahihishiana hizo kazi zao. Iwapo mbinu hii itatumika, basi ni sharti uyapitie madaftari hayo ili kuhakikisha kuwa tuzo hazikutolewa pale ambapo hazikustahili kutolewa.

**Tathmini**

Tathmini uwezo wa mwanafunzi wa kujibu maswali ya marudio.

**Majibu ya maswali ya marudio**

1. Rejesta au sajili ni lugha inayotumiwa mahali ama katika hali fulani na wala haiwezi kuhamishwa kutoka mazingira yale na kutumiwa katika mazingira tofauti.
2.

| Rejesta | Mifano ya msamiati |
|---|---|
| Burudani | bendi, kwaya, tarumbeta, sakata ngoma, taarabu, kata na shoka, tuliza roho, wimbo, ngoma, ruka ruka, na kadhalika. |
| Michezo | miereka, piga kona, ruka maji, piga mbizi, mpira kuwa mwingi, mbio za nyikani, mpira wa wavu na kadhalika. |
| Mahakamani | hakimu, kata rufaa, ruka kesi, simama kizimbani, wakili, kesi, achiliwa kwa dhamana, ushahidi, maamuzi ya mahakama na kadhalika. |
| Hotelini | menu, ankra, chai kwa chapati, leta sahani mbili na kadhalika. |

| | |
|---|---|
| Kanisani | bwana asifiwe, siku ya kiama, Biblia inasema..., tubu dhambi, toa fungu la kumi, roho mtakatifu, mchungaji, somo la leo linatoka katika kitabu cha... na kadhalika. |
| Bungeni | Mheshimiwa Spika, mswada, sheria za bunge, Rais amependekeza marekebisho katika mswada huu na kadhalika. |
| Hospitalini | meza tembe mbili kila asubuhi, ulianza kuhisi maumivu lini? Enda maabarani, tumia maji safi yaliyochemshwa, ninaugua malaria na kadhalika. |

3. a) Michezo
    i) Hujaa jazba hasa baada ya mchezo kuanza,
    ii) Hujaa mazungumzo ya kuhamisha ndimi ambapo baadhi ya maneno ya Kiingereza na hata kienyeji hutumiwa,
    iii) Huwa na lugha ya kuchekesha na kuburudisha wanaoisikiliza,
    iv) Hujaa maoni mbalimbali kuhusu nani atashinda, nani mchezaji bora zaidi, na kadhalika,
    v) Huwepo kurudiarudia maneno kama vile majina ya wachezaji, dakika zilizopita, mabao yaliyofungwa na kadhalika,
    vi) Huwa na lugha ya kuibua hisia na kumfanya mtu kuingiwa na mahangaiko ya moyo,
    vii) Sentensi fupi fupi huweza kutumika pamoja na taswira ya kuchora picha kamili ya yanayotendeka,

   b) Burudani
    i) Kuwa na maneno ya raha,
    ii) Huibua hali za kutuliza na kumpumbaza mshiriki
    iii) Kuwepo na uwezekano wa washirika wake kukesha hadi che huku wakijifurahisha kwa namna wapendavyo,
    iv) Kuwepo bendi ya muziki na wanasarakasi,
    v) Hali ya kusahau aghalabu kwa wakati mfupi tu shida na mahangaiko aliyonayo mshiriki.

   c) Hotelini
    i) Kuwepo kwa lugha ya vyakula mbalimbali,
    ii) Kupatikana kwa msamiati wa vinywaji vingi,
    iii) Wahudumu kuzungumza na wateja kwa unyenyekevu,
    iv) Kupatikana maneno ya huduma mbalimbali,
    v) Lugha ya mkato hutumika.

   d) Sokoni
    i) Lugha ya kurudiarudia maneno hutumika huku bidhaa zikinadiwa,
    ii) Lugha ya kuwavutia wateja huweza kutumiwa,

iii) Hutumika lugha isiyo rasmi na sarufi hukosa kufuatwa,
iv) Kiimbo cha wauza bidhaa hutumika kama vile kuzungumza kwa upole kwa wazee na kutumia lugha ya kusifu kwa wateja wanaonekana tajiri,
v) Lugha ya kununua na kuuza hutumiwa kama vile: panda bei, shuka bei,

4. Tofauti kati ya rejesta ya michezo na rejesta ya burudani

| **Rejesta ya michezo** | **Rejesta ya burudani** |
| --- | --- |
| 1. Hudhihiri jazba<br>2. Huhusisha kuhamisha ndimi<br>3. Huwa na lugha ya kuchekesha<br>4. Watangazaji hutoa maoni yao<br>5. Hudhihirisha urudiaji wa maneno na misemo<br>6. Huwa na lugha ya kuibua hisia<br>7. Sentensi fupifupi hutumiwa | 1. Huhusisha maneno ya raha<br>2. Huibua hali za kutuliza na kupumbaza mshiriki<br>3. Huhusisha shughuli za burudani kama vile muziki, ngoma na sarakasi<br>4. Hukusudia kuwafurahisha washiriki<br>5. Huwasahaulisha washiriki shida na matatizo ya maisha angalau kwa kipindi kifupi |

5. Ndiyo, rejesta ya hotelini na ya sokoni zinakaribiana. Zote ni rejesta za kibiashara na dhamira yake ni kusifia bidhaa na huduma zinazotolewa katika rejesta hizi mbili.

6. a) **Aina mbalimbali za michezo katika jamii**
   i) Riadha
   ii) Mpira wa miguu (kandanda)
   iii) Mpira wa kikapu
   iv) Mpira wa pete
   v) Mpira wa magongo

   b) **Umuhimu wa michezo**
   i) Michezo huimarisha afya.
   ii) Michezo huimarisha umoja miongoni mwa wanajamii.
   iii) Michezo huiletea nchi fahari kote ulimwenguni hasa baada ya wachezaji kushinda katika michezo mbalimbali inayohusisha nchi nyingine.
   iv) Michezo huwaletea washiriki mapato.
   v) Michezo huburudisha.

7. a) **Namna mbalimbali za burudani katika jamii**
   i) Muziki
   ii) Ngoma
   iii) Maigizo
   iv) Usomaji wa habari za burudani katika vitabu, majarida na mitandaoni

v) Sarakasi

b) **Umuhimu wa burudani**

i) Hukuza umoja na utangamano katika jamii.

ii) Hukuza ushirikiano.

iii) Huimarisha afya za washiriki.

iv) Hudumisha utamaduni.

v) Huwaletea watu walio na vipaji vya kuburudisha mapato kwa sababu ni namna ya ajira.

8. Umuhimu wa kuonyesha adabu na heshima kwa watu katika mazingira mbalimbali

i) Watu huishi kwa amani.

ii) Watu huheshimiana hata ingawa wana tamaduni mbalimbali.

iii) Nchi hupiga hatua za kimaendelea kwa sababu hakuna mizozo.

iv) Watu hutambua tamaduni za jamii nyingine zilizo tofauti na zao.

9. a) rejesta ya bungeni.

**Sifa:**

- Matumizi ya majina ya heshima: Mheshimiwa spika
- Kurejelewa kwa spika mara kwa mara: Mheshima Spika..Mheshimiwa Spika...
- Kurejelewa kwa sheria na katiba: sheria hii imekiuka katiba ya nchi yetu.

b) rejesta ya sokoni.

**Sifa:**

- Lugha ya kuwashawishi wanunuzi: Bei rahisi...bei imeshuka...njoo mteja..
- Lugha ya adabu: karibu...
- Msamiati wa bidhaa na bei zao: Bei rahisi.. nunua viatu...
- Kurudiwarudiwa kwa baadhi ya maneno: bei...bei...

c) Rejesta ya kanisani

**Sifa:**

- Kurejelewa kwa Biblia: Maandiko yanasema...
- Msamiati kuhusu dhambi: ... dhambi..
- Maneno ya vitisho kwa wale ambao wanatenda dhambi: ..wenye dhambi watachomwa motoni.

10. **Kulinganisha na kutofautisha rejesta za bungeni na mahakamani**

| Rejesta ya bungeni | Rejesta ya mahakamani |
|---|---|
| 1. Wabunge huomba spika kuwaruhusu wachangie mjadala<br>2. Lugha ya adabu hutumiwa<br>3. Ina msamiati maalumu kama vile, hoja, kura ya maoni n.k.<br>4. Huwepo utaratibu wa kuzungumza<br>5. Hoja huwasilishwa kwa namna maalumu<br>6. Katiba hurejelewa na kunukuliwa<br>7. Lugha ya utafiti hutumiwa. | 1. Lugha ya adabu hutumiwa<br>2. Huwepo na kutafsiri na kufasiri kutoka lugha moja hadi nyingine ili kufanikisha mawasiliano<br>3. Msamiati wa sheria hutumiwa hasa na mawakili<br>4. Katiba hunukuliwa<br>5. Maneno ya Kilatini hutumiwa<br>6. Huwepo kuahirishwa kwa uamuzi kuhusu kesi |

11. La. Kwa sababu rejesta ya hospitalini huhusisha msamiati kuhusu wagonjwa, madaktari, manesi, matibabu na magonjwa mbalimbali ilhali rejesta ya jikoni hujikita katika msamiati wa vyakula, vyombo vya upishi na mapishi mbalimbali.
12. Maneno ya rejesta ya utamaduni ni kama vile: mapokeo, jamii, masimulizi, vizazi, mababu, wahenga, urithi n.k.
13. Rejesta ya sarufi

    Sarufi ni kanuni za lugha zitumiwazo ili kupata ufasaha katika lugha. Rejesta ya sarufi kwa hivyo hudhihirisha istilahi zinazotumiwa katika kanuni hizo.

    Katika rejesta hiyo mna maneno kama vile sarufi, Kiswahili, sentensi, lafudhi, alfabeti, vitenzi, mnyambuliko, maandishi, majina, namna za majina, vivumishi, vielezi, viwakilishi, viunganishi, vihusishi, vihisishi, aya, kuwakifisha, matumizi na mengineyo.
14. Kutunga sentensi
    a) Mwana mpotevu alimrudia babake akiwa na huzuni.
    b) Baraka zetu hutoka kwa Mwenyezi Mungu.
    c Mpira umekuwa mwingi kwa sababu ya mchezaji kuikata pasi ya mpinzaji wake kwa nguvu.
    d) Wakati wa burudani, washiriki walicheza densi usiku kucha.
    e) Ukosefu wa matunda umesababisha matunda yauzwe bei ghali.
    f) Mhudumu alituletea ankra yetu baada ya kumaliza kula.
    g) Wakili wa mshukiwa alikata rufaa baada ya hakimu kutoa uamuzi.
15. a) vyombo
    b) viti
    c) vioo
    d) vyoo

16. - Majina yanayoanza kwa ki- katika umoja na vi- katika wingi: kiti-viti
- Majina yanayoanza kwa ch- katika umoja na vy- katika wingi: chombo-vyombo
- Majina yanayoanza kwa ki- na hayabadiliki: kiangazi
- Majina yanayoanza kwa vi- na hayabadiliki: vigelegele

17. Kutunga sentensi kwa kutumia majina ya ngeli ya KI-VI na vivumishi mbalimbali

**Sentensi za majina ya KI-Vi pamoja na vivumishi vya sifa**

a) Kichupa kikuu kimevunjika. (Vichupa vikuu vimevunjika.)
b) Kizibo kipya kimekazwa. (Vizibo vipya vimekazwa.)
c) Chumba kizuri kimepakwa rangi. (Vyumba vizuri vimepakwa rangi.)
d) Kinywaji kitamu kitanunuliwa. (Vinywaji vitamu vitanunuliwa.)
e) Kicheko kirefu kimezuka. (Vicheko virefu vimezuka.)

**Sentensi za majina ya KI-Vi pamoja na vivumishi vionyeshi**

a) Kisa hiki hakijasimuliwa. (Visa hivi havijasimuliwa.)
b) Kikwazo hicho ni kipya. (Vikwazo hivyo ni vipya.)
c) Kitambaa kile kinapendeza sana. (Vitambaa vile vinapendeza sana.)
d) Kichana hiki cha Kanyana kimeoshwa. (Vichana hivi vya Kanyana vimeoshwa.)
e) Kidimbwi hicho kimekauka. (Vidimbwi hivyo vimekauka.)

**Sentensi za majina ya KI-Vi pamoja na vivumishi viulizi**

a) Kiatu kipi kimeshonwa? (Viatu vipi vimeshonwa?)
b) (Vitambaa vingapi vinapendeza?)
c) Kitabu gani kimesomwa? (Vitabu gani vimesomwa?)
d) Kikwazo kipi kilikiukwa? (Vikwazo vipi vilikiukwa?)
e) (Visa vingapi vitaandikwa?)

**Sentensi za majina ya KI-Vi pamoja na vivumishi vimilikishi**

a) Kibeti chake kimepatikana. (Vibeti vyao vimepatikana.)
b) Choo changu kimejengwa. (Vyoo vyetu vimejengwa.)
c) Kisa chako kimesomwa. (Visa vyenu vimesomwa.)
d) Kiberiti changu kimeanguka majini. (Viberiti vyetu vimeanguka majini.)
e) Kidole chake kitapakwa dawa. (Vidole vyao vitapakwa dawa.)

18. a) Vijiko vyangu vimenunuliwa/Kijiko changu kimenunuliwa.
b) Vioo kumi vitaletwa kesho.
c) Niletee kitabu hicho/Niletee vitabu hivyo.
d) Chumba chote kimefagiliwa/Vyumba vyote vimefagiliwa.

19. **Kutunga sentensi sahihi**

a) Vichana vyetu vimeoshwa.
b) Vyungu vinane vitanunuliwa.

c) Kiatu kile kilishonwa jana.
d) Kijiko kipi kitapewa mtoto?
e) Vitanda vyenyewe havina mablanketi.

20. **Nitatumia ujuzi niliopata katika sura hii:**
a) Kutumia rejesta mbalimbali katika mazungumzo ya kila siku katika mazingira mbalimbali.
b) Kuonyesha adabu na heshima kwa watu mbalimbali katika mazingira mbalimbali.
c) Kushiriki katika michezo.
d) Kujenga urafiki pamoja na ushirikiano kwa watu wa rika zote.
e) Nitachunguza kuhusu rejesta nyingine katika jamii na jinsi zinavyotumika katika mawasiliano.
f) Kutumia majina ya ngeli ya KI-VI pamoja na vivumishi mbalimbali kwa usanifu.

Sura ya
4

# Mada kuu: Mazungumzo na mawasiliano katika shughuli mbalimbali za kijamii (vipindi 20)

## Mada ndogo: Msamiati katika kazi za jumuiya

**Ujuzi upatikanao katika mada**

Mwanafunzi aweze kusikiliza, kuzungumza, kujadili, kueleza, kusoma na kuandika matini mbalimbali kuhusu shughuli au kazi za jumuiya kulingana na mazingira tofauti nchini.

**Mbinu za kufundishia na kujifunzia**

i) Kusoma vifungu vya habari kuhusu shughuli mbalimbali za kijamii na kujibu maswali ya ufahamu na kisha kutoa muhtasari wa kifungu cha habari husika bila kuzidi aya moja.
ii) Wakishirikiane katika vikundi, wanafunzi wajadili shughuli za kijamii walizoshiriki na kisha kuwasilisha mbele ya darasa.
iii) Kila mwanafunzi kusimulia au kueleza mambo muhimu yanayojitokeza katika shughuli ya kijamii aliyoshiriki zaidi.
iv) Kupitia vifungu mbalimbali vya habari, wanafunzi washiriki katika kuainisha na kubainisha aina mbalimbali za maneno kama yanavyojitokeza katika vifungu hivyo.
v) Wanafunzi wafanye mazoezi ya kutunga sentensi kwa kutumia wakati ujao hali yakinishi na hali kanushi.

**Uhusiano wa mada na masomo mengine**

Somo la karatasi ya maarifa kuhusu mada ya kazi za ujenzi wa taifa na kujitegemea.

**Vigezo vya tathmini au upimaji**

Uwezo wa kuelewa mawasiliano yanayojitokeza katika shughuli mbalimbali za kijamii.

**Zana na vifaa**

Picha zinazoonesha matukio ya shughuli mbalimbali za kijamii kama vile *Umuganda*, mkutano, harusi, mazishi, n.k.

## Kipindi cha 1 na 2

## Funzo

Mkutano wa kijiji chetu

### Shabaha

Kufikia mwishoni mwa vipindi hivi, mwanafunzi aweze:

i) Kujua msamiati wa kazi za jumuiya kupitia kwa mikutano ya kijijini
ii) Kuutumia msamiati huo katika kusikiliza, kuzungumza, kujadili, kueleza, na kusoma
iii) Kuutumia msamiati huo katika kusoma na kuandika matini mbalimbali kuhusu shughuli au kazi za jumuiya kulingana na mazingira tofauti nchini

**Zana na vifaa muhimu kwa vipindi hivi**

i) Vifaa vya wanafunzi wenye mahitaji maalumu
ii) Michoro ya shughuli mbalimbali zinazofanyika katika mkutano wa kijijini
iii) Video ama sauti zilizorekodiwa kuhusu mambo yanavyoendeshwa katika mkutano wa kijijini
iv) Kitabu cha Mwanafunzi.

### Mbinu

Kuwashirikisha wanafunzi katika vikundi vya wanafunzi wawili wawili kuzungumzia kuhusu mikutano inayofanyika katika vijiji vyao kwa kuitazama michoro katika Kitabu cha Mwanafunzi. Baadaye, msome pamoja kifungu kuhusu mkutano wa kijijini.

## Kipindi cha 1

## Utaratibu

### *Hatua ya 1*

Unaweza kulianza somo hili kwa kuwauliza wanafunzi maswali kuhusu mikutano vijijini mwao, kama vile:

i) Kijiji chenu kinaitwaje?
ii) Je, huwepo mikutano gani kijijini mwenu?
iii) Umewahi kuhudhuria mkutano wowote kijijini mwenu?
iv) Mikutano hiyo ilihusu nini?
v) Ni kina nani wanaonuiwa kufaidika katika mikutano hiyo?
vi) Ni kina nani wanaohudhuria mikutano hiyo? n.k.

### *Hatua ya 2*

Kwa kutumia picha ama michoro ama vifaa vinginevyo ulivyotayarisha, wafundishe wanafunzi msamiati wa mkutano kama huo wa kijijini. Baadhi ya maneno ambayo unahitajika kufunza hapa ni kama vile:

- mkutano
- mzee au kiongozi wa kijiji
- hotuba
- janga
- mwaliko
- ujumbe
- adabu
- mwanakijiji
- agenda
- maombi
- mgeni wa heshima
- kuhudhuria, n.k.

***Hatua ya 3***

Waongoze wanafunzi kujadili michoro na kusoma kifungu kilichopo katika Kitabu cha Mwanafunzi, ukurasa wa 108. Kumbuka kuwashirikisha wanafunzi wote.

***Hatua ya 4***

Waongoze wanafunzi kujibu maswali ya pamoja na zoezi la sehemu hii na kuyafanyia masahihisho majibu yao.

***Hatua ya 5***

Waongoze wanafunzi kuandaa muhtasari wa yale waliyojifunza katika sehemu hii ili kuhakikisha kuwa malengo ya kipindi yametimizwa.

**Maadili na mwenendo mwema**

Kuonyesha heshima na ushirikiano wakati wowote kwenye shughuli mbalimbali za kijamii.

**Tathmini**

Tathmini uwezo wa mwanafunzi wa kuutumia msamiati wa kazi za jumuiya katika kusoma na kuandika matini mbalimbali kuhusu shughuli au kazi za jumuiya kulingana na mazingira tofauti nchini.

**Majibu ya maswali**

1. Msamiati wa kimsingi kuhusu shughuli katika mkutano wa kijijini na maana
    a) mkutano – mkusanyiko wa watu mahali pamoja
    b) adabu – tabia njema
    c) heshima – utu au hali ya kuwa na adabu
    d) mgeni wa heshima – mtu maalumu aliyealikwa katika mkutano
    e) kujikinga – kujilinda
    f) kupunguza makali – kuondoa kwa kiasi fulani athari fulani
    g) UKIMWI – hali ya ukosefu wa kinga mwilini
    h) mfunge ndoa – muoane
    i) kumkumbatia – kushikana kama njia ya kuonyeshana upendo
    j) afya nzuri – hali nzuri ya mtu
    k) waathiriwa – watu waliopata athari za jambo fulani mbaya
    l) kujiunga – kuwa pamoja

m) kuambukizwa – kupata ugonjwa
n) kiongozi wa kijiji – mtu anayeelekeza shughuli za uongozi kijijini
o) kupiga foleni – watu kusimama katika mstari au mlolongo
p) kufungua mkutano – kuanza mkutano

2. Kujadiliana kuhusu ugonjwa wa UKIMWI na kuwepo kwa upimaji wa UKIMWI.
3. Bi. Abigael Uwera
4. Mambo muhimu yanayojitokeza katika kifungu ni:
   a) Mkutano wa kijiji unafanyika.
   b) Wanakijiji wanajadiliana kuhusu ugonjwa wa UKIMWI. Mgeni wa heshima katika mkutano ni afisa wa afya kutoka Wizara ya Afya.
   c) Afisa wa afya anazungumzia maana ya UKIMWI, jinsi UKIMWI huambukizwa, jinsi ya kupunguza makali ya athari za UKIMWI.
   d) Waathirika wa UKIMWI wanaeleza jinsi ambavyo wamekuwa wakikabiliana na ugonjwa huo.
   e) Wanakijiji wanajitolea kupimwa hali zao.
5. Hakikisha kuwa aya hiyo imeandikwa kwa sentensi zenye mtiririko na zinazoleta maana kamili. Hakikisha kuwa mambo muhimu kifunguni yametajwa katika aya hiyo.

   **Mfano wa aya**

   Munyana alihudhuria mkutano wa kijiji chao. Shughuli kuu ya mkutano ilikuwa kujadiliana kuhusu ugonjwa wa UKIMWI. Mgeni wa heshima katika mkutano huo alikuwa afisa wa afya kutoka Wizara ya Afya, Bi. Abigael Uwera. Afisa wa afya alizungumzia maana ya UKIMWI, jinsi UKIMWI huambukizwa na jinsi ya kukabiliana na UKIMWI pamoja na kupunguza makali ya athari za UKIMWI. Aidha, waathirika wa UKIMWI walieleza jinsi ambavyo wamekuwa wakikabiliana na ugonjwa huo. Baadaye, wanakijiji walijitolea kupimwi ili wajue hali zao.

## Kipindi cha 2

### Funzo

Mjadala: Kazi ya kikundi

### Shabaha

Mwanafunzi aweze kuutumia msamiati wa kazi za jumuiya katika majadiliano ya vikundi.

### Mbinu

Kuwashirikisha wanafunzi katika vikundi ili kujadiliana jinsi ya kupunguza umaskini kijijini.

**Utaratibu**

***Hatua ya 1***

Wanafunzi wazungumzie waliyojifunza katika kipindi kilichotangulia.

***Hatua ya 2***

Wanafunzi wajiunge na vikundi mbalimbali.

***Hatua ya 3***

Hakikisha kuwa wanafunzi wanashiriki katika mjadala na kuwa wanatumia msamiati kuhusu mkutano wa kijiji kama walivyojifunza katika kipindi kilichotangulia.

***Hatua ya 4***

Mwanafunzi kutoka kila kikundi awasilishe hoja zao mbele ya darasa huku akirekebisha penye makosa.

**Maadili na mwenendo mwema**

Kuonyesha heshima na ushirikiano wakati wowote kwenye shughuli mbalimbali za kijamii.

**Tathmini**

Tathmini uwezo wa mwanafunzi wa kijieleza kwa kujiamini na kuutumia msamiati wa mkutano wa kijijini.

**Zoezi la ziada**

Wanafunzi wataje shughuli mbalimbali ambazo hufanyika katika mikutano ya vijiji vyao.

## Kipindi 3 na 4

**Funzo**

Sherehe ya harusi ya rafiki yangu

**Shabaha**

Kufikia mwishoni mwa vipindi hivi, mwanafunzi aweze:

i) Kujua msamiati wa kazi za jumuiya kupitia kwa sherehe za arusi.
ii) Kuutumia msamiati huo katika mawasiliano yake ya kila siku.

**Zana na vifaa muhimu kwa vipindi hivi**

i) Picha za arusi
ii) Video za arusi
iii) Vifaa vya wanafunzi wenye mahitaji maalumu
iv) Kitabu cha Mwanafunzi.

## Kipindi cha 3

Katika kipindi hiki, wanafunzi watajadiliana kuhusu mambo ambayo hufanyika katika sherehe za harusi walizohudhuria.

### Mbinu

Kuwashirikisha wanafunzi katika vikundi vya wanafunzi wawili wawili kuzungumzia kuhusu sherehe za harusi.

### Utaratibu

#### *Hatua ya 1*

Unaweza kulianza somo hili kwa kurudia baadhi ya yale uliyofunza katika kipindi kilichopita. Halafu unaweza kuwaongoza wanafunzi kutambua malengo ya kipindi hiki kwa kuwauliza maswali kama vile:

i) Je, harusi ni nini?

ii) Ni kina nani walio muhimu katika harusi?

iii) Taja mambo mawili muhimu yanayohitajika kufanywa kabla ya harusi.

#### *Hatua ya 2*

Huku ukitumia picha ama video pamoja na vifaa vinginevyo ulivyotayarisha, waongoze wanafunzi kujua msamiati wa harusi. Baadhi ya maneno unayohitajika kufunza ni pamoja na:

- kuchumbia
- mchumba
- harusi au arusi
- mshenga
- mahari
- bibi harusi
- bwana arusi
- mpambe
- siku ya arusi
- mapochopocho

#### *Hatua ya 3*

Waongoze wanafunzi kufanya kazi ya wanafunzi wawili wawili katika Kitabu cha Mwanafunzi. Hakikisha kuwa wametumia baadhi ya msamiati uliofunza hapo juu na kuwa wote wameshiriki.

#### *Hatua ya 4*

Wape fursa baadhi ya wanafunzi kusema mambo waliyojifunza katika kipindi hiki huku ukihakikisha kuwa malengo ya kipindi hiki yametimizwa.

### Maadili na mwenendo mwema

Kuonyesha heshima na ushirikiano wakati wowote kwenye shughuli mbalimbali za kijamii.

### Tathmini

Tathmini uwezo wa mwanafunzi wa kuzungumza kwa kujiamini huku akitumia msamiati wa sherehe za harusi.

## Kipindi cha 4

Katika kipindi hiki, wanafunzi watasoma kifungu cha habari katika Kitabu cha Mwanafunzi.

## Utaratibu

### *Hatua ya 1*

Waongoze wanafunzi katika kukumbuka mambo muhimu waliyofanya katika kipindi kilichotangulia. Hakikisha kuwa wanakumbuka msamiati kuhusu harusi na kuwa wanaweza kutumia msamiati huo kutungia sentensi sahihi.

### *Hatua ya 2*

Waongoze wanafunzi kusoma kifungu katika Kitabu cha mwanafunzi, na wajibu maswali chini yake.

### *Hatua ya 3*

Waongoze wanafunzi kujadiri michoro iliyo katika kitabu cha mwanafunzi.

### *Hatua ya 4*

Waongoze wanafunzi kuunda muhtasari wa yale waliyojifunza katika sehemu hii huku ukihakikisha kuwa malengo ya kipindi hiki yameafikiwa.

**Suala mtambuka**

Kipindi hiki kinatoa nafasi ya kujadili mafunzo kuhusu usawa wa jinsia kutokana na harusi.

**Majibu ya maswali**

1. Ndoa ni jambo la kufurahia kwa sababu sherehe za harusi zinazotangulia ndoa huwa za kupendeza na hufanyika katika hali ya furaha kubwa.

   2 na 3 maana ya msamiati pamoja na sentensio zilizotungwa kwa kutumia msamiati huo

   a) harusi – sherehe za mume na mke kuoana (Harusi ya Ganza na Mutesi ilipendeza sana.)
   b) ndoa – makubaliano ya mume na mke kuishi pamoja (Ndoa imara ni msingi wa familia yenye furaha.)
   c) Mpambe – mtu anayesimamia bwana au bibi harusi wakati wa harusi (Mpambe wa Ganza alitabasamu sana wakati wa harusi.)
   d) kumchumbia – kupeleka maombi kwa wazazi wa msichana ya kutaka kumuoa binti yao (Ganza alimchumbia Mutesi kabla ya kumuoa.)
   e) posa – maombi yanayopelekewa wazazi wa msichana anayedhamiriwa kuolewa (Wazazi wa Ganza waliwatuma wajumbe wakapeleke posa kwa wazazi wa Mutesi.)
   f) Mahari – mali inayotolewa na mwanamume kwa wazazi wa msichana anayedhamiria kumuoa (Mahari si malipo bali ni namna ya kuonyesha heshima kwa wazazi wa msichana anayeolewa.)

g) pete – pambo wanalivalishana vidoleni bwana na bibi harusi wakati wa sherehe za harusi (Pete walizovalishana Ganza na Mutesi zilitengenezwa kwa dhahabu.)
h) mchumba – mwanamume aliyepeleka posa au mwanamke aliyepelekewa posa na ikakubaliwa na wazazi (Mchumba wake Ganza anaitwa Mutesi.)
i) waliapishwa – walisemeshwa viapo/walitakiwa waape (Bwana na bibi harusi waliapishwa huku wakivalishana pete.)
j) kuvishana pete – kuvalishana pete (Ganza na Mutesi walivishana pete wakati wa sherehe za harusi yao.)

4. Mambo muhimu yanayofanyika harusini kwa mujibu wa kifungu ni:
   a) Watu kufika kanisani
   b) Bibi harusi kuingizwa kanisani akisindikizwa na wazazi wake
   c) Bibi harusi na bwana harusi kuapishwa na kuvishana pete
   d) Kasisi kuwatangaza rasmi bwana na bibi harusi kuwa mume na mke
   e) Sherehe za burudani baada ya ibada ya kanisani.
5. Ushirikiano katika jamii una umuhimu mkubwa. Kwa mujibu wa kifungu, mwanamke na mwanamume wanaooana hupata msaada kutoka kwa wanajamii katika kuandaa sherehe za harusi. Kila hatua hushirikisha wanajamii.
6. Muhtasari wa kifungu

   Shema anamsimulia Tona kuhusu sherehe za harusi za rafikiye alizohudhuria. Anasimulia kuhusu maandalizi ya kabla ya siku ya harusi na matukio yalivyofuatana katika siku hiyo ya harusi. Wapambe wa pande zote hushirikiana na maharusi katika maandalizi. Katika siku ya harusi, bwana harusi hufika mapema kanisani kumsubiri bibi harusi. Bibi harusi huingizwa kanisani akisindikizwa na wazazi wake. Baada ya kupokelewa na kasisi, ibada ya kanisani huanza. Maharusi huapishwa huku wakivishana pete. Baada ya hapo, kasisi huwatangaza rasmi bwana na bibi harusi kuwa mume na mke. Baada ya ibada ya kanisani, burudani.

Hakikisha ufupisho umeandikwa kwa sentensi zenye maana na mtiririko. Mwanafunzi aangazie mambo yote muhimu kwenye kifungu kwa ufupi na lugha iliyo sahihi.

### Kipindi 5 na 6

**Funzo**

Mazishi

**Shabaha**

Kufikia mwishoni mwa vipindi hivi, mwanafunzi aweze:
i) Kubaini msamiati wa msingi unaotumika katika shughuli za mazishi.
ii) Kuelezea mambo mbalimbali yafanyikayo katika shughuli za mazishi.

**Zana na vifaa muhimu kwa vipindi hivi**

i) Picha za watu katika mazishi

ii) Vifaa vya wanafunzi wenye mahitaji maalumu

iii) Kitabu cha Mwanafunzi.

**Mbinu**

Kuwashirikisha wanafunzi katika vikundi vya wanafunzi wawili wawili kuzungumzia kuhusu shughuli za mazishi kabla ya kuwaongoza kusoma kifungu na kujibu maswali.

**Kipindi cha 5**

Katika kipindi hiki, wanafunzi watasoma kifungu cha habari kuhusu mazishi na kujifunza mengi kuhusu mazishi.

**Utaratibu**

***Hatua ya 1***

Wanafunzi wazungumzie waliyojifunza katika kipindi kilichotangulia.

***Hatua ya 2***

Kwa kuwa kipindi hiki kinaweza kuibua hisia za huzuni, hakikisha kuwa umekifunza kwa makini. Waeleze wanafunzi maana ya mazishi kisha wataje wanayofahamu kuhusu mazishi.

Epuka kuwauliza wanafunzi kuzungumzia mazishi ya jamaa zao au mtu yeyote wa karibu. Zungumzia mazishi kwa ujumla bila kurejelea mazishi fulani maalumu ya watu ambao wanafunzi wanawafahamu.

***Hatua ya 3***

Wanafunzi wafanye kazi za wanafunzi wawili wawili kisha wasome kifungu cha habari katika Kitabu cha Mwanafunzi, na wajibu maswali chini yake.

**Maadili na mwenendo mwema**

Kuonyesha heshima na ushirikiano wakati wowote kwenye shughuli mbalimbali za kijamii.

**Tathmini**

Tathmini uwezo wa mwanafunzi wa kuzungumza kwa kujiamini huku akitumia msamiati wa shughuli za mazishi.

**Majibu ya maswali**

1. Mazishi ni shughuli zote zinazofanyika wakati wa kumzika mtu aliyeaga dunia.

   2 na 3 Kubainisha msamiati wa mazishi kifunguni na kuutungia sentensi

   a) aliaga dunia – alikufa (Mwafulani aliaga dunia baada ya kuugua kwa siku nyingi.)

b) ugonjwa wa saratani ya mapafu – ugonjwa wa kansa ya mapafu (Marehemu aliaga dunia baada ya kuugua ugonjwa wa saratani ya mapafu.)
c) mochari – chumba au jengo mnamohifadhiwa maiti (Marehemu alitolewa mochari asubuhi ya siku ya mazishi.)
d) kumpa mjomba heshima zake za mwisho – kuhakikisha marehemu amefanyiwa shughuli mwafaka za mazishi (Jamaa na marafiki walifika kumpa mjomba heshima zake za mwisho.)
e) mazishi – shughuli zote zinazofanyika wakati wa kumzika mtu aliyeaga dunia (Mazishi ya marehemu babu yake yalihudhuriwa na watu wengi.)
f) jeneza – sanduku la kumzikia maiti (Jeneza liliteremshwa kaburini kwa mtambo maalumu.)
g) sanda – kitambaa chepesi anachovishwa maiti na kuzikwa nacho (Watu wengi hawana ukakamavu wa kumvisha maiti sanda.)
h) kaburi – shimo anamozikwa maiti (Waombolezaji walishirikiana kuchimba kaburi.)
i) walitufariji – walituliwaza wakati wa huzuni (Jamaa na marafiki walitufariji baada ya mjomba kuaga dunia.)
j) marehemu – neno la heshima linalotanguliziwa jina la mtu aliyeaga dunia (Marehemu mjomba alipendwa sana na watu.)
k) mfu – mtu aliyekufa (Mfu alizikwa siku hiyo.)
l) amlaze mahali pema peponi – ampumzishe mahali pazuri huko kunakoaminika roho za wafu huenda (Waombolezaji walimuomba Mungu amlaze marehemu mahali pema peponi.)

4. Shughuli muhimu za mazishi zilizotajwa kifunguni ni:
   a) Mwili wa marehemu kupelekwa mochari baada ya kuaga dunia.
   b) Jamaa na marafiki kushiriki kupanga shughuli za mazishi na kuandaa jeneza, sanda na kaburi.
   c) Mwili wa marehemu kuondolewa mochari ili kufanyiwa ibada ya wafu.
   d) Mwili wa marehemu kusafirishwa nyumbani ili kufanyiwa mazishi.
   e) Ibada ya wafu kufanywa siku ya mazishi na maiti kuzikwa kaburini hapo baadaye.
   f) Wageni kupewa vyakula na vinywaji na kuondoka baadaye kwenda makwao.
5. Aya ya mambo muhimu kutokana na kifungu

   Msimulizi anasimulia jinsi mjomba wake alivyoaga dunia kutokana na uvutaji sigara uliomfanya augue sarata ya mapafu. Mwili wa marehemu ulipelekwa mochari baada ya kuaga dunia. Jamaa na marafiki walishiriki kupanga shughuli za mazishi na kuandaa jeneza, sanda na kaburi. Mwili wa marehemu uliondolewa mochari ili kufanyiwa ibada ya wafu. Mwili wa marehemu ulisafirishwa nyumbani ili kufanyiwa mazishi. Ibada ya wafu ilifanywa siku ya mazishi na maiti kuzikwa kaburini hapo baadaye. Wageni walipewa vyakula na vinywaji na kuondoka baadaye kwenda makwao.

### Kipindi cha 6

Kazi ya kikundi

**Shabaha**

Mwanafunzi aweze kuutumia msamiati unaotumika katika shughuli za mazishi.

**Mbinu**

Kuwashirikisha wanafunzi katika vikundi ili kujadiliana kuhusu shughuli za mazishi ya kienyeji katika sehemu wanafunzi watokako.

### Utaratibu

***Hatua ya 1***

Wanafunzi wazungumzie msamiati muhimu waliojifunza katika kipindi kilichotangulia. Hakikisha kuwa wanaweza kutumia msamiati huo katika mawasiliano kwa usahihi.

***Hatua ya 2***

Wanafunzi walinganishe na kutofautisha shughuli mbalimbali zinazofanyika katika harusi na mazishi.

***Hatua ya 3***

Katika vikundi, wanafunzi wafanye kazi ya kikundi. Hakikisha kuwa wanafunzi wote wameshiriki.

***Hatua ya 4***

Wanafunzi waseme muhtasari wa mambo muhimu waliyojifunza. Hakikisha kuwa malengo ya sehemu hii yametimizwa.

**Maadili na mwenendo mwema**

Kuonyesha heshima na ushirikiano wakati wowote kwenye shughuli mbalimbali za kijamii.

**Tathmini**

Tathmini uwezo wa mwanafunzi wa kuzungumza kwa kujiamini huku akitumia msamiati wa shughuli za mazishi.

### Kipindi cha 7 na 8

**Funzo**

Mjadala: Kazi ya *umuganda*

**Shabaha**

Kufikia mwishoni mwa vipindi hivi, mwanafunzi aweze:

i) Kujua msamiati wa kazi za *umuganda*

ii) Kuutumia msamiati huo katika mawasiliano yake ya kila siku katika kusikiliza, kuzungumza, kujadili, kueleza, kusoma na kuandika matini mbalimbali.

**Zana na vifaa muhimu kwa vipindi hivi**

i) Picha na michoro ya watu wakifanya kazi mbalimbali za *umuganda*
ii) Vifaa vya wanafunzi wenye mahitaji maalumu
iii) Kitabu cha Mwanafunzi.

**Mbinu**

Kuwashirikisha wanafunzi katika vikundi vya wanafunzi wawili wawili kuzungumzia kuhusu kazi za umuganda kabla ya kuwaongoza kusoma kifungu na kujibu maswali.

## Kipindi cha 7

## Utaratibu

### *Hatua ya 1*

Unaweza kulianza somo hili kwa kuuliza wanafunzi maswali kama vile:
i) Je, *umuganda* ni nini hapa kwetu?
ii) Neno hili *umuganda* lina maana gani katika Kiswahili?
iii) Umewahi kuhudhuria kazi hii?
iv) Manufaa ya kazi hii ni gani?
v) Kazi hii hufanyika mara ngapi kwa mwezi?

### *Hatua ya 2*

Baada ya wanafunzi kufahamu ni lipi linalonuiwa kufunzwa, waongoze kuufahamu msamiati wa sehemu hii. Baadhi ya maneno unayoweza kufunza hapa ni kama vile:
- umoja
- ushirikiano
- usafi
- ujima
- utengano
- ujenzi wa taifa (*umuganda* ni mojawapo ya njia za kujenga taifa)
- utu uzima
- shughuli
- jamaa
- jamii

### *Hatua ya 3*

Waongoze wanafunzi kutazama michoro na kusoma yaliyomo chini ya kazi ya *umuganda*.

Kumbuka hapa kuwa ni sharti kila zoezi lifanyiwe masahihisho ipasavyo kabla ya kuendelea na kazi ifuatayo.

### *Hatua ya 4*

Wanafunzi wataje mambo muhimu waliyojifunza katika kipindi hiki. Hakikisha kuwa malengo ya sehemu hii yametimizwa.

**Maadili na mwenendo mwema**

Kuonyesha heshima na ushirikiano wakati wowote kwenye shughuli mbalimbali za kijamii.

**Tathmini**

Tathmini uwezo wa mwanafunzi wa kuzungumza kwa kujiamini huku akitumia msamiati wa kazi za umuganda.

**Majibu ya maswali**

1. Umuhimu wa kazi ya umuganda katika jamii zetu

   Jamii zetu hushirikiana kufanya kazi za kuinua hali zetu. Ushirikiano huo huleta umoja. Kazi wanazofanya kwa pamoja ni kama vile: kuzuia mmomonyoko wa udongo, kusafisha mazingira, kupanda miti, kulima na kupalilia mashamba.
2. Masimulizi ya wanafunzi yadhihirishe uelewa wa kazi ya umuganda katika jamii zao. Shughuli muhimu kama vile utunzaji mazingira, ushirikiano katika kazi za kilimo na kazi nyinginezo zitajwe.

## Kipindi cha 8

### Funzo

Mjadala: Kazi ya kikundi.

**Shabaha**

Mwanafunzi aweze kuutumia msamiati unaotumika katika kazi za ushirikiano katika jamii.

**Mbinu**

Kuwashirikisha wanafunzi katika vikundi kuzungumzia kuhusu kazi za ushirikiano walizowahi kushiriki katika jamii zao.

***Hatua ya 1***

Wanafunzi wazungumzie msamiati muhimu waliojifunza katika kipindi kilichotangulia. Hakikisha kuwa wanaweza kutumia msamiati huo katika mawasiliano kwa usahihi.

***Hatua ya 2***

Katika vikundi, wanafunzi wafanye mjadala uliopo katika kazi ya kikundi. Hakikisha kuwa wanafunzi wote wameshiriki.

***Hatua ya 3***

Wanafunzi waseme muhtasari wa mambo muhimu waliyojifunza. Hakikisha kuwa malengo ya sehemu hii yametimizwa.

**Maadili na mwenendo mwema**

Kuonyesha heshima na ushirikiano wakati wowote kwenye shughuli mbalimbali za ushirikiano katika kijamii.

**Tathmini**

Tathmini uwezo wa mwanafunzi wa kuzungumza kwa kujiamini huku akitumia msamiati wa shughuli za ushirikiano katika jamii.

**Kazi ya ziada**

Wanafunzi wataje mambo ambayo hufanyika katika shughuli zifuatazo pamoja na umuhimu wazo katika jamii.

i) *Ubudehe*
ii) *Gacaca*
iii) *Itotero*

## Kipindi cha 9 na 10

**Funzo**

Namna sahihi ya kuuliza maswali

**Shabaha**

Kufikia mwishoni mwa vipindi hivi, mwanafunzi aweze:

i) Kujua namna sahihi ya kuuliza maswali.
ii) Kuutumia ujuzi huo katika mawasiliano yake ya kila siku.

**Zana na vifaa muhimu kwa vipindi hivi**

i) Kadi zilizoandikwa viulizi
ii) Wanafunzi darasani (kuulizana maswali)
iii) Vifaa vya wanafunzi wenye mahitaji maalumu
iv) Kitabu cha Mwanafunzi.

**Mbinu**

Kuwashirikisha wanafunzi kuuliza maswali kwa kutumia maneno ya kuulizia kabla ya kusoma kifungu kwa pamoja na kuulizana maswali kwa kutumia maneno ya viulizi.

## Kipindi cha 9

## Utaratibu

***Hatua ya 1***

Lianze funzo hili kwa kuwaongoza wanafunzi kutaja baadhi ya semi zenye maswali. Mfano:

i) Angurumapo simba mcheza ni nani?
ii) Yu wapi mtesi atesaye mfululizo/kufululiza?

iii) Wajua tamu ya ua, sumu wanipiani?
iv) Pilipili usiyoila yakuwashiani?

### *Hatua ya 2*

Huku ukiwatumia wanafunzi darasani, funza malengo ya kipindi hiki. Unaweza kuanza kwa kiulizi chochote. Mathalan, onyesha kadi iliyoandikwa 'nani'. Mchague mwanafunzi mmoja atunge swali sahihi akitumia neno hilo. Akoseapo msahihishe. Wanafunzi kadhaa watunge maswali yao. Halafu tena waongoze kujua maana ya kiulizi hicho.

Fanya vivi hivi kwa viulizi vyote ulivyovipangia kuvifunza. Hakikisha kuwa umevifunza viulizi vyote vilivyomo kwenye Kitabu cha Mwanafunzi.

### *Hatua ya 3*

Waongoze wanafunzi kusoma kifungu kilichomo vitabuni mwao na wafanye kazi ya wanafunzi wawili wawili chini yake. Katika huko kusoma, washirikishe wanafunzi wote.

### Maadili na mwenendo mwema

Kuonyesha heshima na ushirikiano wakati wowote kwenye shughuli mbalimbali za ushirikiano katika kijamii.

### Tathmini

Tathmini ujuzi wa mwanafunzi wa kuuliza maswali kwa lugha ifaayo. Wanafunzi watunge maswali sahihi kwa kutumia maneno yaliyotolewa. Kwa mfano:

a) Wanyarwanda hushiriki vipi katika kazi za umuganda?
b) Mkutano wa wanakijiji ulifanyika lini?
c) Ulishiriki wapi kazi za umuganda za mwezi uliopita?
d) Nani hajui umuhimu wa kazi za umuganda?
e) Nini kinaweza kumzuia mzalendo kushiriki shughuli za kijamii?
f) Watu wangapi walifanya utunzaji wa mazingira?
g) Ni kwa njia gani wananchi wanaweza kudumisha umoja?

## Kipindi cha 10

### Funzo

Mjadala: Kazi ya kikundi

### Shabaha

Mwanafunzi awe na ujuzi wa kuuliza maswali.

### Mbinu

Kuwashirikisha wanafunzi kuuliza maswali kwa kutumia maneno ya kuulizia.

## Utaratibu

***Hatua ya 1***

Waongoze wanafunzi kutunga sentensi wakitumia viulizi mbalimbali walivyojifunza katika kipindi kilichotangulia.

***Hatua ya 2***

Waongoze wanafunzi kufanya kazi ya kikundi katika Kitabu cha Mwanafunzi. Unaweza kuwapa vifungu zaidi vya habari kuhusu shughuli mbalimbali za kijamii, wavisome na waulizane maswali kuhusu yaliyomo kwenye vifungu hivyo.

***Hatua ya 3***

Hatimaye, waongoze wanafunzi kufanya muhtasari wa yale waliyojifunza katika sehemu hii.

**Maadili na mwenendo mwema**

Kuonyesha heshima na ushirikiano wakati wowote kwenye shughuli mbalimbali za ushirikiano katika kijamii.

**Tathmini**

Tathmini ujuzi wa mwanafunzi wa kuuliza maswali kwa lugha ifaayo. Wanafunzi watunge maswali sahihi kwa kutumia maneno ya kuulizia waliyojifunza katika Kipindi cha 9.

## Kipindi cha 11

**Funzo**

Aina saba za maneno ya Kiswahili (Nomino) (Kitabu cha Mwanafunzi,

**Shabaha**

Kufikia mwishoni mwa kipindi hiki, mwanafunzi aweze:

i) Kuzitambua aina saba za maneno ya Kiswahili.
ii) Kutambua maana ya nomino.
iii) Kutambua maneno yaliyomo katika kundi la nomino.
vi) Kuyatumia vilivyo mambo haya yote katika mawasiliano yake ya kila siku.

**Zana na vifaa muhimu kwa kipindi hiki**

i) Michoro ya maneno haya saba kila neno likiwa na picha za kusimamia aina hiyo ya maneno kama vile neno 'nomino' pamoja na michoro ya vifaa vinavyotumika katika shughuli mbalimbali za kijamii kama vile jembe, fyekeo na kadhalika.
ii) Vifaa halisi

iii) Vitendo vya wanafunzi darasani
iv) Vifaa vya wanafunzi wenye mahitaji maalumu
v) Kitabu cha Mwanafunzi.

**Mbinu**

Kuwashirikisha wanafunzi kuzungumzia mambo wanayoyajua kuhusiana na nomino na kutoa mifano kabla ya kusoma kwa pamoja maelezo katika Kitabu cha Mwanafunzi.

## Utaratibu

***Hatua ya 1***

Anza kwa kuwaongoza wanafunzi kukumbuka maana ya 'nomino'. Hakikisha kuwa wanafunzi wanafahamu maana ya neno hili.

***Hatua ya 2***

Kwa kutumia michoro uliyoitayarisha na vifaa vinginevyo, funza namna za nomino ukizioanisha na shughuli mbalimbali za kijamii.

***Hatua ya 3***

Waongoze wanafunzi kusoma yaliyomo chini ya nomino katika vitabu vyao, ukurasa wa 117. Katika kusoma huko, unaweza kuongezea yaliyomo katika mifano ya jedwali kwa kuwashirikisha wanafunzi kutunga sentensi zaidi.

***Hatua ya 4***

Waongoze wanafunzi kufanya mazoezi ya sehemu hii ya kubainisha nomino pamoja na kutunga sentensi.

***Hatua ya 5***

Maliza sehemu hii kwa kuwaongoza wanafunzi kuunda muhtasari wa yale waliyojifunza.

**Suala mtambuka**

Kipindi hiki kinatoa nafasi nzuri ya kujadili kuhusu usawa wa jinsia.

**Tathmini**

Tathmini uwezo wa mwanafunzi wa kusoma kifungu na kubainisha aina za nomino mbalimbali zilizotumiwa pamoja na kuzitumia nomino kwa usahihi katika mawasiliano.

**Majibu ya mazoezi**

**Zoezi A**

Ama kwa kweli, <u>ndoa</u> **(kawaida)** ni jambo linalowafurahisha <u>watu</u> **(kawaida)** wengi. Kutajwa tu kwa neno hili hufanya roho za watu wengi kusisimka. Takriban watu wote husikia neno hili kwa <u>upendo</u> **(dhahania)**. Kwa nini upendo? Unapotajiwa neno hili,

fikira **(dhahania)** ya kwanza kukujia ni raha **(dhahania)**. Watu husikia raha kwa sababu huwepo maakuli **(wingi)** na vyakula **(kawaida)** vingi vya bwerere. Pia, harusi **(kawaida)** huleta heshima na umaarufu **(dhahania)**.

Kabla ya kufanya harusi, yapo mambo **(kawaida)** mengi ambayo hufanyika. Kwanza kabisa, ni sharti mchumba **(kawaida)** apatikane. Halafu ni sharti ujumbe **(dhahania)** wa posa **(kawaida)** upelekwe na mshenga **(kawaida)** kwa kina mchumba. Ukikubalika, mahari **(wingi)** huzungumziwa na kulipwa. Ni baada ya haya yote tu ambapo siku ya harusi huwekwa.

Nayo matayarisho **(dhahania)** ya harusi huwa mengi. Bi harusi **(kawaida)** pamoja na wapambe **(kawaida)** wake sharti wanunuliwe mavazi **(kawaida)** mbalimbali ya harusi. Mavazi haya huwa pamoja na nguo **(kawaida)** maalumu za Bi harusi na wapambe wake. Pia ni sharti pawepo jozi **(jamii**) mpya za viatu (**kawaida**), pete (**kawaida**) ya harusi, mashada **(jamii)** ya maua **(kawaida)** na kadhalika. Matayarisho mengine ni usafiri **(dhahania)**, waendesha harusi **(kawaida)**, kwaya **(jamii)**, na matayarisho mengine mbalimbali.

Hatimaye huja siku yenyewe ya harusi. Mfano mzuri wa siku hii ni harusi ya rafiki **(kawaida)** yangu Iliza **(pekee)** iliyofanyika Ijumaa **(pekee)** jijini Kigali **(pekee)**. Umati **(jamii)** wa watu ulihudhuria harusi hiyo. Baada ya ibada (**kawaida**), tulienda katika Hoteli ya Serena (pekee) ambapo sherehe **(dhahania)** kamili iliandaliwa.

**Zoezi B**

Mifano ya sentensi

1. **Ndoa** hiyo iliwafurahisha watu sana. (*nomino ya kawaida*)
2. Ndoa hudumu ikiwa mume na mke wana **upendo**. (*nomino dhahania*)
3. **Kwaya ya waimbaji** wa nyimbo za ijili iliimba kwa sauti ya juu. (*nomino ya jamii*)
4. Daima **Iliza** alitamani harusi ya kupendeza. (*nomino ya pekee/maalumu*)
5. **Maakuli** katika sherehe hizo za harusi yalifurahiwa sana. *(nomino ya wingi)*

## Kipindi 12

### Funzo

Vitenzi

### Shabaha

Kufikia mwishoni mwa kipindi hiki, mwanafunzi aweze:

i) Kujua maana ya kitenzi.

ii) Kuvitumia vilivyo vitenzi katika mawasiliano yake akiwa katika mazingira mbalimbali.

**Zana na vifaa muhimu kwa kipindi hiki**

i) Kadi zilizoandikwa vitenzi tofauti tofauti.

ii) Vitendo vya wanafunzi
iii) Vifaa vya wanafunzi wenye mahitaji maalumu
iv) Kitabu cha Mwanafunzi.

**Mbinu**

Kuwashirikisha wanafunzi kuzungumzia mambo wanayoyajua kuhusiana na vitenzi na kutoa mifano kabla ya kusoma kwa pamoja maelezo katika Kitabu cha Mwanafunzi.

## Utaratibu

***Hatua ya 1***

Baada ya kuwaongoza wanafunzi kukumbuka maana na matumizi ya neno 'kitenzi', waulize wanafunzi kukutajia vitenzi vyovyote wavijuavyo. Kwa namna hii utajua moja kwa moja ikiwa wameelewa maana ya vitenzi.

***Hatua ya 2***

Huku ukivitumia vitendo vya wanafunzi darasani, anza kufunza namna za vitenzi. Hakikisha ya kwamba huendelei kufunza namna nyingine ya kitenzi kabla ya wanafunzi wote kuelewa namna hiyo unayofunza. Mifano inayotolewa iwe katika muktadha wa shughuli mbalimbali za kijamii walizosoma wanafunzi.

***Hatua ya 3***

Waongoze wanafunzi kusoma sehemu hii ambayo imo katika vitabu vyao.
Washirikishe wanafunzi wote katika kusoma huko.

***Hatua ya 4***

Waelekeze wanafunzi kufanya mazoezi yote mawili ya sehemu hii pamoja na kuhakikisha ya kuwa majibu yao yamefanyiwa masahihisho.

Hatimaye, waongoze wanafunzi kufanya muhtasari wa yale waliyojifunza katika sehemu hii.

## Suala mtambuka.

Kipindi hiki kinatoa nafasi nzuri ya kujadili uhifadhi wa mazingira na usafi wake.

**Tathmini**

Tathmini uwezo wa mwanafunzi wa kusoma kifungu na kubainisha aina za vitenzi mbalimbali zilizotumiwa pamoja na kuvitumia vitenzi kwa usahihi katika mawasiliano.

**Majibu ya mazoezi**
**Zoezi A**
"Tuharakishe **(kitenzi halisi)**. Ujenzi wa choo umeanza **(kitenzi halisi)**," Ikirezi aliniambia **(kitenzi halisi)**. Alikuwa **(kitenzi kisaidizi)** akihema **(kitenzi kikuu)**.

"Mimi ni **(kitenzi kishirikishi)** mgonjwa. Ningali **(kitenzi kisaidizi)** ninaumwa **(kitenzi kikuu)** na tumbo lakini nitajikaza **(kitenzi halisi)**," nilimjibu **(kitenzi halisi)**. Hatimaye tuliwasili **(kitenzi halisi)** penye mkutano. Watu walikuwa **(kitenzi kisaidizi)** wamejigawa **(kitenzi kikuu)** katika vikundi tayari kwa kazi mbalimbali.

"Tazama **(kitenzi halisi)**. Kila mtu ameanza **(kitenzi kisaidizi)** kujenga **(kitenzi kikuu)** choo isipokuwa sisi," nilimwambia Ikirezi. Kiongozi wa kijiji alinisikia.

"Msiwe **(kitenzi halisi)** na shaka. Nyinyi mtaokota **(kitenzi halisi)** taka zote zilizopo pale uwanjani. Baada ya hapo, mtafagia **(kitenzi halisi)** kando ya barabara. Kazi hiyo si **(kitenzi kishirikishi)** ngumu," kiongozi wa kijiji alisema **(kitenzi halisi)**.

Mimi na Abatoni tulitafuta **(kitenzi halisi)** vifagio. Tuliongezewa **(kitenzi halisi)** vijana watatu ili watusaidie **(kitenzi halisi)** kufanya **(kitenzi halisi)** kazi hiyo. Tulifurahia **(kitenzi halisi)** sana kushirikiana **(kitenzi halisi)** na wanakijiji.

**Zoezi B**

**Mifano ya sentensi**

1. Rais **aliwahimiza** wananchi washiriki kikamilifu katika shughuli mbalimbali za kijamii. (kitenzi halisi)
2. Wanakijiji **wangali** wanafanya kazi ya *umuganda*. (kitenzi kisaidizi)
3. Harusi hiyo haitawahi **sahaulika** kwa namna ilivyopendeza. (kitenzi kikuu)
4. Kazi ya ushirika si ngumu. (kitenzi kishirikishi)

## Kipindi 13

### Funzo

Vielezi

### Shabaha

Kufikia mwishoni mwa kipindi hiki, mwanafunzi aweze:

i) Kutambua maana ya kielezi.
ii) Kuvitumia vilivyo vielezi katika mawasiliano yao ya kila siku.

**Zana na vifaa muhimu kwa kipindi hiki**

i) Kadi zilizoandikwa vielezi vya vitendo mbalimbali.
ii) Vitendo vya wanafunzi.
iii) Vifaa vya wanafunzi wenye mahitaji maalumu.
iv) Kitabu cha Mwanafunzi.

### Mbinu

Kuwashirikisha wanafunzi kuzungumzia mambo wanayoyajua kuhusiana na vielezi na kutoa mifano kabla ya kusoma kwa pamoja maelezo katika Kitabu cha Mwanafunzi.

## Utaratibu

### *Hatua ya 1*

Unaweza kulianza somo hili kwa kurudia baadhi ya yale muhimu uliyofunza katika kipindi kilichopita. Baada ya hayo, unaweza kuwauliza wanafunzi kueleza maana na matumizi ya kielezi.

### *Hatua ya 2*

Funza aina mbalimbali za vielezi. Ni sharti usisitize matumizi ya jumla ya kielezi kuwa huongezea maana kitenzi, kivumishi ama huweza kujiongezea maana pia. Kumbuka kuwa matumizi ya kila namna ya neno unalofunza ni muhimu zaidi. Mifano yote unayotoa sharti yawepo katika muktadha wa shughuli mbalimbali za jumuiya.

### *Hatua ya 3*

Waongoze wanafunzi kusoma sehemu ya vielezi ambayo imo vitabuni mwao kama njia mojawapo ya kutilia mkazo yote uliyofunza.

### *Hatua ya 4*

Waongoze wanafunzi katika mazoezi mbalimbali katika sehemu hii. Kwanza wasome na kubainisha vielezi na halafu wavitungie vielezi hivyo tungo zilizo sahihi.

### *Hatua ya 5*

Waongoze wanafunzi kuandika muhtasari wa yale yaliyo muhimu na ambayo wamejifunza hapa.

## Suala mtambuka.

Kipindi hiki kinatoa nafasi nzuri ya kujadili uhifadhi wa mazingira na usafi wake.

### Tathmini

Tathmini uwezo wa mwanafunzi wa kusoma kifungu na kubainisha aina za vielezi mbalimbali zilizotumiwa pamoja na kuvitumia vielezi kwa usahihi katika mawasiliano.

**Majibu ya zoezi A**

Ilikuwa siku ya Jumamosi **(wakati)**. Ilikuwa siku ya kuwasaidia wazee kuandaa mashamba yao na kupanda mbegu. Wanakiji wote waliamka alfajiri **(wakati)**. Mimi pia nilijiunga nao kwa hiari **(namna)**. Wa kwanza kusaidiwa aliitwa Abera. Tulitembea upesi **(namna)** kuelekea shambani mwake ili tufike mapema **(wakati)**. Tulipofika ndani ya shamba **(mahali)**, kila mtu alipewa jukumu. Wengine walifyeka majani marefu yaliyomea pembeni mwa shamba **(mahali)**. Waliyafyeka majani kwa panga **(namna)**. Wengine walilima kwa jembe la mkono **(namna)**. Wengine waliondoa magugu hatari kutoka shambani na kuyachoma kwa moto **(namna)**. Sisi tulipanda mbegu. Kila mtu alipewa

kazi ya kufanya mara kwa mara **(wakati)**. Hakuna aliyekaa bure **(namna)**. Sote tulifanya kazi kijeshi **(namna)**.

**Majibu ya zoezi B (Kitabu cha Mwanafunzi, ukurasa wa 122)**

1. Rais aliwahimiza wananchi wafanye **bidii** katika shughuli mbalimbali za kijamii. (kielezi cha namna)
2. Wanakijiji wangali watafanya kazi ya *umuganda* **Jumamosi**. (kielezi cha wakati)
3. Harusi hiyo ilifanyiwa **hotelini**. (kielezi cha mahali)
4. Kazi ya ushirika si ngumu **sana**. (kielezi cha kiasi)

## Kipindi 14

### Funzo

Vivumishi

### Shabaha

Kufikia mwishoni mwa kipindi hiki, mwanafunzi aweze:

i) Kujua kivumishi ni nini

ii) Kuvitumia vilivyo vivumishi katika mazingira yoyote anayokuwemo.

**Zana na vifaa muhimu kwa kipindi hiki**

i) Kadi zilizoandikwa vivumishi mbalimbali.

ii) Vifaa halisi vya kufunzia vivumishi.

iii) Vifaa vya wanafunzi wenye mahitaji maalumu.

iv) Kitabu cha Mwanafunzi.

### Mbinu

Kuwashirikisha wanafunzi kuzungumzia mambo wanayoyajua kuhusiana na vivumishi na kutoa mifano kabla ya kusoma kwa pamoja maelezo katika Kitabu cha Mwanafunzi.

## Utaratibu

### *Hatua ya 1*

Unaweza kulianza somo hili kwa kuwaongoza wanafunzi kurudia yale mambo muhimu waliyofunzwa na kujifunza kuhusu nomino mbalimbali. (Haya ni maneno yanayoongezea maneno mengine maana – vivumishi huongezea majina maana na vielezi huongezea vitenzi maana n.k.)

### *Hatua ya 2*

Kwa kutumia vifaa ulivyotayarisha, anza kufunza namna za vivumishi. Njia mojawapo yakutumia vifaa vyako ni kuwa na vifaa vinavyolinganisha vitu mbalimbali. Unaweza kuwa na maji safi na maji machafu, unaweza kuwa na mwanafunzi mfupi na mrefu na kadhalika. Hakikisha kuwa mifano unayotoa ipo katika muktadha wa shughuli mbalimbali za jumuiya.

***Hatua ya 3***
Waongoze wanafunzi kusoma sehemu hii katika Kitabu cha Mwanafunzi.

***Hatua ya 4***
Waelekeze wanafunzi kufanya mazoezi yote mawili ya sehemu hii pamoja na kuhakikisha ya kuwa majibu yao yamefanyiwa masahihisho vilivyo.

***Hatua ya 5***
Hatimaye, waongoze wanafunzi kuunda na kuandika muhtasari wa yale waliyojifunza katika sehemu hii.

**Tathmini**

Tathmini uwezo wa mwanafunzi wa kusoma kifungu na kubainisha aina za vivumishi mbalimbali zilizotumiwa pamoja na kuvitumia vivumishi kwa usahihi katika mawasiliano.

**Majibu ya zoezi A**

Ni taifa gani **(kiulizi)** ambalo halipendi maendeleo? Ama ni watu wepi **(kiulizi)** ambao hawapendi kuendelea? Sisi Wanyarwanda tunapenda maendeleo ili taifa letu **(kimilikishi)** likue hata zaidi. Nchi yenye **(pekee)** watu wanaopenda maendeleo hukua haraka. Ili jambo hili **(kionyeshi)** liwezekane, ni sharti tufanye mambo kadhaa **(idadi)**.

Kwanza kabisa, nchi yetu haiwezi kukua bila masomo. Lazima watoto wote **(pekee)** waliofika umri wa kuenda shule waende shuleni. Nasi wanafunzi wenyewe **(pekee)** tulenge kufikia elimu ya chuo kikuu. Ili kufaulu masomoni, ni sharti tushirikiane na jamii. Ujuzi huu **(kionyeshi)** tunaopata shuleni ni sharti tuutumie kusaidia jamii. Tusingoje hadi tumalize chuo kikuu ndipo tuanze kujenga taifa hili **(kionyeshi)** letu (kimilikishi).

Pili, usafi ni jambo muhimu **(sifa)** sana. Jamii haiwezi kujenga taifa lake **(kimilikishi)** kama haina afya nzuri **(sifa)**. Je, kina nani wanafaa kudumisha usafi huu? **(kionyeshi)** Watu hao **(kionyeshi)** si watu wengine (**pekee**) bali ni mimi na wewe. Kila mmoja wetu (**kimilikishi**) ahakikishe kuwa anaishi katika mazingira safi **(sifa)** kila siku.

Tatu, kuna shughuli ya mikutano tofauti tofauti **(sifa)** ya kutangaza na kuhimiza maendeleo. Jamii inapokutana na kuelezwa maendeleo yaliyopatikana, hupata motisha ya kufanya mengi zaidi. Hali hii **(kionyeshi)** basi huwa ni msukumo muhimu **(sifa)** katika kazi zao **(kionyeshi)**. Vilevile, vijiji hushindana katika maendeleo. Mashindano ya dhati kati ya vijiji huwa ni motisha nzuri **(sifa)** ya ujenzi wa taifa. Kumbuka kuwa vijiji vikipiga hatua mbele nalo taifa hufanya vivyo hivyo.

Jambo jingine **(pekee)** linalohitajika katika huu ujenzi wa taifa ni kuwa na mikakati kabambe **(sifa)** ya kushughulikia mikasa. Mathalan, tumejitayarisha vipi kukabiliana na mkurupuko wa magonjwa hatari **(sifa)** na njaa? Ni sharti tushirikiane ili kuibuka na mikakati kabambe ya kukabiliana na mikasa kama hii.

Ili haya yote na mengine mengi **(idadi)** yafaulu, umoja na ushirikiano wetu lazima uwepo. Kumbuka kuwa kidole kimoja **(idadi)** hakivunji chawa nalo jiwe moja **(idadi)** haliinjiki chungu.

**Majibu ya zoezi B**

1. Rais aliwahimiza wananchi **wazuri** wafanye bidii katika shughuli mbalimbali za kijamii. (kivumishi cha sifa)
2. Wanakijiji **wenye** uzalendo watafanya kazi ya *umuganda* Jumamosi. (kivumishi cha pekee)
3. Harusi **hiyo** ilifanyiwa hotelini. (kivumishi kionyeshi)
4. Tutahitaji fyekeo **kumi** za kufyekea nyasi. (kivumishi cha idadi kamili)
5. Je, ni wanafunzi **wangapi** walioshiriki shughuli za kijamii wakati wa likizo? (kivumishi kiulizi)
6. Uzalendo **wetu** utadhihirika katika huduma kwa jamii **zetu**. (vivumishi vimilikishi).

## Kipindi 15

### Funzo

Viwakilishi

### Shabaha

Kufikia mwishoni mwa kipindi hiki, mwanafunzi aweze:

i) Kuitambua maana ya viwakilishi.
ii) Kuvitumia vilivyo viwakilishi katika mawasiliano yao ya kila siku.

**Zana na vifaa muhimu kwa kipindi hiki**

i) Vifaa halisi
ii) Wanafunzi darasani
iii) Vifaa vya wanafunzi wenye mahitaji maalumu
iv) Kitabu cha Mwanafunzi.

### Mbinu

Kuwashirikisha wanafunzi kuzungumzia mambo wanayoyajua kuhusiana na vimilikishi na kutoa mifano kabla ya kusoma kwa pamoja maelezo katika Kitabu cha Mwanafunzi

## Utaratibu

### Hatua ya 1

Unaweza kuanza kufunza hapa kwa kuwatumia wanafunzi wako ili kufunza viwakilishi nafsi vya A-WA. Kwa mfano, baada ya kujitumia kama mfano kufunza neno 'mimi', unaweza kumchagua mwanafunzi kutunga sentensi: *Mimi ninasoma Kiswahili*. Fanya vivi hivi mpaka uwe umevifundisha viwakilishi hivi vyote sita.

### *Hatua ya 2*

Kwa njia hiyo hiyo ya hatua 1, funza viwakilishi viambata ama virejeleo. Hapa itakuwa rahisi ukitumia vifaa halisi. Mathalan, ukiwa pamoja na wanafunzi unaweza kuwaongoza kutunga sentensi kama: *Tutakisafisha kijiji*. Njia mojawapo rahisi ya kuvifunza hivi viwakilishi ni kuwaongoza wanafunzi kutambua kuwa ni virejeleo.

Kama ilivyo kawaida hapa, unapolitumia jedwali lililomo vitabuni mwa wanafunzi unaweza kuliongezea hata zaidi sana sana matumizi ya viwakilishi ulivyofunza. Jinsi matumizi yanavyokuwa mengi ndivyo wanafunzi wanavyoelewa hata zaidi.

### *Hatua ya 3*

Waongoze wanafunzi katika kuisoma sehemu hii iliyomo vitabuni mwao (ukurasa wa 124-125).

### *Hatua ya 4*

Waongoze wanafunzi kufanya zoezi la sehemu hii ya viwakilishi pamoja na kusahihisha majibu yao.

### *Hatua ya 5*

Hitimisha sehemu hii kwa kuwaongoza wanafunzi kuunda na kuuandika muhtasari wa yale yaliyo muhimu katika kipindi hiki.

### Suala mtambuka

Kipindi hiki kinatoa nafasi nzuri ya kujadili amani na maadili na kuhimiza wanajamii kushirikiana katika shughuli mbalimbali.

### Tathmini

Tathmini uwezo wa mwanafunzi wa kusoma kifungu na kubainisha aina za vimilikishi mbalimbali zilizotumiwa pamoja na kuvitumia vimilikishi kwa usahihi katika mawasiliano.

### Majibu ya zoezi

<u>Waliosema</u> **(vya nafsi ambata)** kuwa umoja ni nguvu hawakukosea bali walipiga ndipo. <u>Mimi</u> **(vya nafsi huru)** ninaamini sana katika msemo huu. <u>Ninaamini</u> **(vya nafsi ambata)** kwa sababu ya mambo niliyoshuhudia nilipompoteza mama mzazi. Mama alikuwa mtu wa watu. <u>Aliwapenda</u> **(vya nafsi ambata)** wanakajiji nao wanakijiji wa mbali na wa karibu wakampenda. Kifo chake kiliwashtua wengi. <u>Kilifanya</u> **(vya ngeli)**

kijiji kizima kiomboleze. Watu walifurika nyumbani kwetu kutupa pole. Kuwepo kwao **(vya virejeshi)** kulituliwaza. Licha ya machungu, tulihisi kuwa hatupo peke yetu. Nani **(vya viulizi)** angekosa kupata nguvu katika hali kama hii? Msiba huleta unyonge. Wetu **(vya vivumishi vimilikishi)** ulileta nguvu kutokana na ushirikiano huo.

Mbali na kutupa moyo, wanakijiji waligharamia mazishi. Wao **(vya vivumishi vionyeshi)** walisimamia kila kitu. Sisi **(vya nafsi huru)** tulishuhudia tu mambo yakitendeka. Hawakutaka **(vya nafsi ambata)** tushiriki katika shughuli zozote kutokana na huzuni. Waliopika **(vya nafsi ambata)** walipika. Waliotengeneza jeneza walifanya hivyo tena kwa ustadi. Waliochimba kaburi hawakusita kumaliza mapema. Kila kitu kilifanywa kwa haraka na ustadi. Mama akalazwa na kupewa heshima zake za mwisho kwa ushirikiano wa wanakijiji. Wao hao **(vya vionyeshi visisitizi)** wakatuchangia pesa za matumizi ya baadaye. Tulikosa maneno ya kuelezea furaha na shukrani zetu kwao. Kweli, umoja ni nguvu.

## Kipindi cha 16

### Funzo

Viunganishi

### Shabaha

Kufikia mwishoni mwa kipindi hiki, mwanafunzi aweze:
i) Kujua maana ya kiunganishi.
ii) Kuvitumia viunganishi kwa njia iliyo sahihi na katika mawasiliano yake ya kila siku.

**Zana na vifaa muhimu kwa kipindi hiki**

i) Kadi zenye viunganishi tofauti tofauti
ii) Vitendo vya wanafunzi
iii) Vifaa vya wanafunzi wenye mahitaji maalumu
iv) Kitabu cha Mwanafunzi.

### Mbinu

Kuwashirikisha wanafunzi kuzungumzia mambo wanayoyajua kuhusiana na viunganishi na kutoa mifano kabla ya kusoma kwa pamoja maelezo katika Kitabu cha Mwanafunzi.

## Utaratibu

### *Hatua ya 1*

Unaweza kuanza kufunza hapa kwa kuwaongoza wanafunzi kujua maana ya viunganishi. Nalo hili unaweza kulitekeleza kwa kutumia vitendo darasani. Kwa mfano, tia kalamu katika mfuko na ufunze: *Nimetia kalamu ndani ya mfuko*, na kadhalika.

***Hatua ya 2***

Kwa kutumia mbinu kama ile ya hatua 1 hapo juu, funza aina zote za viunganishi. Kulingana na wepesi wa kufahamu wa wanafunzi wako, unaweza kutaja hapa kuwa maneno yanayounganisha huweza kugawika mara mbili: Vipo viunganishi na vipo vihusishi. Viunganishi huunganisha neno na neno ama kundi la maneno lakini vihusishi huunganisha kitu na pahali. Kwa hiyo *na* ni kiunganishi na *kando ya* ni kihusishi.

Kumbuka kuwa ni sharti ufunze vihusishi vya *-a unganifu* kama vile *wa, cha, za, pa, la*, ambavyo huweza kuunganika na majina ya pahali na kuwa vihusishi kama vile *katikati mwa, upande wa, nje ya, na* kadhalika.

***Hatua ya 3***

Waongoze wanafunzi kusoma sehemu hii iliyomo katika vitabu vyao

***Hatua ya 4***

Waelekeze wanafunzi wako kufanya kazi ya utafiti ya kikundi iliyomo vitabuni mwao pamoja na zoezi lifuatalo. Hakikisha ya kuwa pale panapohitaji kufanyiwa masahihisho unawaongoza kufanya hivyo.

**Suala mtambuka**

Kipindi hiki

**Tathmini**

Tathmini uwezo wa mwanafunzi wa kusoma kifungu na kubainisha aina za viunganishi mbalimbali zilizotumiwa pamoja na kuvitumia viunganishi kwa usahihi katika mawasiliano.

**Majibu ya zoezi**

Kila jamii huwa na ngoma yao waipendayo. <u>Aghalabu</u> wao huipenda <u>kwa sababu</u> wameirithi kutoka kwa mababu zao. <u>Mathalan</u>, Waswahili hupenda sana msondo. Je, nyinyi mnapenda ngoma gani <u>katika</u> jamii yenu?

<u>Kwa kawaida</u>, ngoma kama hiyo huchezwa na wale waliopo sasa. <u>Baadaye</u> hupitishwa kwa vizazi vijavyo. <u>Kwa namna hiyo,</u> ngoma husika huja ikawa sehemu kuu ya utamaduni wao <u>japo</u> baadhi ya mambo ya kisasa huongezwa. Mambo hayo ya kisasa huongezwa pasipo kubadilisha asilia ya ngoma hizo.

Sisi Wanyarwanda <u>pia</u> tunapenda ngoma zetu za kiasili. Itokeapo shughuli muhimu, sisi hushiriki <u>katika</u> kuimba <u>na</u> kucheza ngoma zetu za kitamaduni.

<u>Hivyo basi</u>, ngoma huchezwa kama njia mojawapo ya kujiburudisha. Shughuli hii huambatana sana sana <u>na</u> sherehe fulani <u>kama vile</u> siku za kitaifa, harusi, kusherehekea mavuno, siku ya kutoka jandoni <u>au</u> kuvunja ungo na kadhalika. <u>Mbali na hayo</u>, ngoma ni njia moja kuu ya kutuleta pamoja <u>ili</u> kufanya shughuli mbalimbali za kimaendeleo.

Aidha, tunapocheza ngoma fulani siku ya taifa, tunapata kumbukumbu muhimu katika historia yetu. Kwa mfano, tunakumbuka jinsi tulivyokuja pamoja kujikomboa kutoka kwa minyororo ya wakoloni. Ikiwa umoja wetu ulifukuza wakoloni sembuse umaskini?

Ngoma vile vile hutukumbusha umuhimu wa kuwepo kwa amani. Pia, ngoma hutuonya dhidi ya kuchukiana. Hutukumbusha kuwa amani, upendo na umoja ni mambo muhimu katika ujenzi wa nchi yetu.

Iwapo tutapenda ngoma zetu za kienyeji na kutunga nyimbo za kisasa zenye kukuza ushirikiano, basi tutapiga hatua kubwa katika maendeleo yetu.

## Kipindi 17

### Funzo

Vihisishi

### Shabaha

Kufikia mwishoni mwa kipindi hiki, mwanafunzi aweze:

i) Kujua maana ya kihisishi.

ii) Kuvitumia kwa njia sahihi vihisishi katika mawasiliano yao wakiwa katika mazingira tofauti tofauti.

### Mbinu

Kuwashirikisha wanafunzi kuzungumzia mambo wanayoyajua kuhusiana na vihisishi na kutoa mifano kabla ya kusoma kwa pamoja maelezo katika Kitabu cha Mwanafunzi.

**Zana na vifaa muhimu kwa kipindi hiki**

i) Vitendo vya wanafunzi darasani

ii) Vifaa vya wanafunzi wenye mahitaji maalumu

iii) Kitabu cha Mwanafunzi.

## Utaratibu

### *Hatua ya 1*

Waelekeze wanafunzi kufahamu maana ya kihisishi. Kwa mfano, unaweza kuonyesha hisia za mshangao au huzuni kupitia matendo mbalimbali kati yako na wanafunzi.

### *Hatua ya 2*

Kwa mbinu hiyo hiyo na nyinginezo, toa mifano ya vihisishi ukijikita katika muktadha wa mawasiliano katika shughuli mbalimbali za jumuiya. Utapata hapa kuwa baadhi ya maneno hayo yanaweza kufunzwa kwa kuigizwa darasani.

### *Hatua ya 3*

Waongoze wanafunzi kusoma sehemu ya kihisishi katika Kitabu cha Mwanafunzi,

Katika kusoma huko, hakikisha ya kuwa umewaongoza wanafunzi kutunga sentensi mbalimbali zenye vihisishi katika muktadha wa shughuli za jumuiya.

***Hatua ya 4***

Baada ya hayo, waelekeze wanafunzi kufanya mazoezi yote mawili ya sehemu hii pamoja na kuhakikisha ya kuwa panapohitaji masahihisho pamefanyiwa hivyo.

***Hatua ya 5***

Waongoze wanafunzi katika kuandaa muhtasari wa yale muhimu uliyofunza hapa na kuuandika madaftarini mwao.

### Suala mtambuka.

Somo hili linatoa nafasi ya kujadili mafunzo kuhusu mazingira na maendeleo endelevu kutokana na kifungu cha habari.

**Tathmini**

Tathmini uwezo wa mwanafunzi wa kusoma kifungu na kubainisha aina za vihisishi mbalimbali zilizotumiwa pamoja na kuvitumia vihisishi kwa usahihi katika mawasiliano.

**Majibu ya zoezi**

Sote tulifunga safari ya kumtembelea Gatete kijijini mwao. Lo! Hatukuamini macho yetu tulipofika huko. Kumbe kijiji hicho kilikuwa safi na tulivu mno!

Gatete alipokuja kutulaki, tulimpa pongezi.

"Hongera! Mnafanya kazi nzuri kweli," Ndoli alisema.

Gatete alimtazama Ndoli kwa mshangao. Hakuelewa sababu za hongera zake.

"Jamani! Mbona kijiji hiki chenu ni safi namna hii?" nilimwuliza Gatete.

"Ahaa! Sisi hutupa taka zote katika majaa. Pia tunachimba mitaro ili tusiwe na vidimbwi vya maji. Yeyote, awe mdogo au mkubwa, huokota majani makavu au taka zozote popote," Gatete alisema akitabasamu.

"Maskini sisi! Hatufanyi hivyo hata!" Ndoli alisema.

"Alaa! Mnafaa mwanze kufanya hivyo moja kwa moja. Usafi ni jambo muhimu sana katika maisha yetu."

"Naam! Kuanzia leo, nitahimiza wanakijiji wenzangu ili kwa pamoja tudumishe usafi."

### Kipindi 18

**Funzo**

Utambuzi wa aina saba za maneno ya Kiswahili katika kifungu

**Shabaha**

Kufikia mwishoni mwa kipindi hiki, mwanafunzi aweze:

i) Kubainisha na kuainisha kwa urahisi aina saba za maneno ya Kiswahili.
ii) Kuyatumia kwa urahisi aina hizo saba za maneno ya Kiswahili katika kuwasiliana na watu wengine.

**Zana na vifaa muhimu kwa kipindi hiki**

i) Kitabu cha Mwanafunzi

**Mbinu**

Kuwashirikisha wanafunzi kuzungumzia mambo wanayoyajua kuhusiana na aina saba za maneno ya Kiswahili na kutoa mifano kabla ya kusoma kwa pamoja maelezo katika Kitabu cha Mwanafunzi.

## Utaratibu

### *Hatua ya 1*

Hatua kwa hatua, kutoka nomino hadi vihisishi, waongoze wanafunzi kutaja mambo muhimu waliyojifunza katika kila sehemu.

### *Hatua ya 2*

Waongoze wanafunzi kulifanya zoezi la ziada na kazi ya kikundi katika Kitabu cha Mwanafunzi.

Hapa, itakuwa vizuri zaidi wanafunzi wakisoma kifungu cha habari kwa mara ya kwanza kwa minajili ya kukielewa. Halafu tena wakisome kwa mara ya pili wakitambua aina mbalimbali za maneno.

### *Hatua ya 3*

Wape wanafunzi vifungu zaidi vya habari vilivyoandikwa katika Kiswahili ili wavisome na watambue aina mbalimbali za maneno jinsi ilivyopendekezwa katika kazi ya kikundi.

**Suala mtambuka**

Kipindi hiki kinatoa nafasi nzuri ya kujadili usawa wa jinsia kutokana na kifungu cha habari.

**Tathmini**

Tathmini uwezo wa mwanafunzi wa kusoma kifungu na kubainisha aina saba za maneno ya Kiswahili pamoja na kuyatumia maneno hayo kwa usahihi katika mawasiliano.

**Majibu ya zoezi la ziada**

**Aina za maneno katika kifungu 'Kukoga mwaka'**

Hapo zamani (*kielezi cha wakati*), watu (*nomino ya kawaida*) tofauti (*kivumishi cha sifa*) walikuwa (kitenzi kishirikishi) na (*kiunganishi*) itikadi (*nomino ya kawaida*) mbalimbali (*kivumishi cha idadi*) kuhusu kuanza kwa mwaka (*kielezi cha wakati*). Baadhi yao walisherehekea (*kitenzi halisi*) siku hiyo kwa kuchinja (*kitenzi halisi*) na (*kiunganishi*) kuandaa (*kitenzi halisi*) karamu (*kielezi*) murua! (*kivumishi cha sifa*) Nao (*kiwakilishi*) wengine (kivumishi cha pekee) waliwatambikia (*kitenzi halisi*) wazee (*nomino ya kawaida*) wao (*kivumishi kimilikishi*) waliofuata (*kitenzi halisi*) njia ya marahaba (*kielezi cha mahali*). Zaidi ya haya (*kivumishi kionyeshi*), baadhi ya watu waliamini kuwa ni (*kitenzi kishirikishi*) lazima mwaka mpya (*kivumishi cha sifa*) uanze (*kitenzi halisi*) kwa usafi (*kielezi cha namna*). Hii (*kiwakilishi kionyeshi*) ndiyo ilikuwa sababu ya kukoga mwaka.

Kukoga mwaka kulikuwa na utaratibu (*nomino halisi*) wake (*kivumishi kishirikishi*). Kazi (*nomino ya kawaida*) hizo (*kivumishi kionyeshi*) zote (*kivumishi cha idadi*) zilitegemea (*kitenzi halisi*) mwanzo wa mwaka (*kielezi cha wakati*) wa (*kiunganishi cha a-unganifu*) kiasili (*kielezi cha namna*) bali (*kiunganishi*) si (*kitenzi kishirikishi*) ule (*kiwakilishi kionyeshi*) wa kizungu (*kielezi cha namna*). Mwaka huo wa kiasili ulikuwa (*kitenzi kisaidizi*) ukianza (*kitenzi kikuu*) saa thenashara (*kielezi cha wakati*) hivi za asubuhi (*kielezi cha wakati*). Hivyo basi, kabla ya wakati (*kielezi cha wakati*) huo, wenyeji walirauka saa kumi (*kielezi cha wakati*). Madhumuni ya kuamka wakati huo yalikuwa kusafisha kila kitu kabla ya mapambazuko (*kielezi cha wakati*). Basi wanawake (*nomino ya kawaida*) waliamka na kukusanya vitu (*nomino ya kawaida*) vyote (*kivumishi cha pekee*) ambavyo viliweza kuoshwa na kuvipeleka mtoni (*kielezi cha mahali*). Wengine (*kiwakilishi cha pekee*) walibaki (*kitenzi halisi*) nyumbani (*kielezi cha mahali*) ili (*kiunganishi cha kutegemeza*) kusafisha vile vitu ambavyo havikuweza kuchukuliwa mtoni lakini ambavyo vilihitaji kuoshwa au kusafishwa.

Baadhi ya vitu vilivyooshwa mtoni (*kielezi cha mahali*) vilikuwa nguo zilizomea koga, vyungu, sahani, sufuria na vyombo vinginevyo. Baadhi ya watu walisafisha vyombo (*nomino ya kawaida*) hivyo kwa sabuni lakini wengine walivisafisha kwa majani maalum.

Jambo (*nomino dhahania*) lililokuwa la (*kivumishi cha a-unganifu*) mwisho kufanywa huko mtoni (*kielezi cha mahali*) ni kuwaosha watoto. Baadaye watu wazima wangeoga wao wenyewe. Wakati mwingine, watu wangeosheana miguu (*nomino ya kawaida*) kama ishara ya upendo (*nomino dhahania*).

Nao wanawake (*nomino ya kawaida*) wale (*kivumishi kionyeshi*) waliobaki (*kitenzi halisi*) nyumbani (*kielezi cha mahali*) walikuwa na kazi kubwa ya kusafisha nyumba (*nomino ya kawaida*) mbalimbali za msonge. Baadhi yao walipaka sakafu kwa samadi mbichi iliyochanganywa na udongo na maji. Nao wanawake wengine waliondoa

masizi (*nomino ya kawaida*) yaliyokuwa yakining'inia kwenye mapaa (*kielezi cha mahali*).

Vijana (*nomino ya kawaida*) nao walisomba maji kutoka mtoni. Maji hayo yangetumiwa na wanaume (*nomino ya kawaida*) kuogea. Wao pia wangeoga baadaye.

Wanaume (*nomino ya kawaida*) nao hawakukaa bure. Ilikuwa kazi yao kufyeka na kusafisha uani (*kielezi cha mahali*), mbele na pande zote za nyumba (*kielezi cha mahali*). Pia ilikuwa kazi yao kufyeka (*kitenzi halisi*) nyasi zozote (*kielezi*) zilizokuwepo pale kiamboni (*kielezi cha mahali*) pamoja na kukata matagaa (*nomino ya kawaida*) yasiyohitajika ili kwamba jua la mwaka mpya lichomozapo liangaze boma (*nomino ya kawaida*) zima (*kivumishi cha sifa*).

Je, ni kwa nini (*kivumishi kiulizi*) kazi hizo zote zilifanyika? Hata wakati huo, wenyeji (*nomino ya kawaida*) waliamini kuwa Mungu (*nomino ya pekee/Maalumu*) hakupenda uchafu. Isitoshe, waliamini kuwa mtu akianza jambo fulani kwa nuksi basi hatafanikiwa katika mambo mengi. Hivyo basi, imani (*nomino dhahania)* yao (*kivumishi kionyeshi*) ilikuwa kwamba mwaka ukianza kwa uchafu basi shughuli zao zote mnamo mwaka huo zingekumbwa na nuksi. Hapana hata mmoja aliyetaka kutofanikiwa. Naam! Mwaka (*nomino ya kawaida*) mpya (*kivumishi cha sifa*) ungeanza (*kitenzi halisi*) kwa usafi kweli (*kielezi cha namna*).

**Kumbuka**: Wasisitizie wanafunzi kuwa aina ya neno haibainiki kwa kulikumbuka neno lenyewe bali lilivyotumiwa katika sentensi.

## Kipindi 19

### Funzo

Matumizi ya wakati ujao -ta- na wakati uliopita -li- hali yakinishi na hali kanushi

### Shabaha

Kufikia mwishoni mwa kipindi hiki, mwanafunzi aweze:
i) Kutambua wakati uliopita -li- na wakati ujao -ta-.
ii) Kubainisha hali yakinishi na hali kanushi.
iii) Kutumia vilivyo wakati uliopita -li- na wakati ujao -ta- katika hali yakinishi na hali kanushi.

**Zana na vifaa muhimu kwa kipindi hiki**

i) Vifaa halisi.
ii) Wanafunzi darasani.
iii) Vifaa vya wanafunzi wenye mahitaji maalumu.
iv) Kitabu cha Mwanafunzi.

**Mbinu**

Mhadhara pamoja na kuwashirikisha wanafunzi kueleza uelewa wao wa dhana za wakati uliopita na ujao pamoja na hali yakinishi na kanushi kabla ya kusoma maelezo katika Kitabu cha Mwanafunzi.

## Utaratibu

***Hatua ya 1***

Unaweza kuanza kufundisha kwa kuwauliza wanafunzi wataje mambo watakayofanya baada ya kipindi hiki. Kwa mfano: *Mtafunzwa somo gani baada ya somo hili*? Andika majibu yao katika ubao.

Baada ya hapo, waulize wanafunzi kutaja shughuli yoyote iliyofanyika darasani au shuleni siku moja au siku kadhaa zilizopita. Mfano: *Tulisoma nini katika kipindi kilichopita*? Andika jibu hilo katika ubao.

***Hatua ya 2***

Waambie wanafunzi kutambua tofauti zilizopo baina ya sentensi hizo mbili. Hapo, waambie kuhusu wakati uliopita na wakati ujao.

***Hatua ya 3***

Waambie wanafunzi kukataa au kukanusha sentensi hizo kisha waeleze tofauti zilizopo kabla na baada ya kukanushwa kwa sentensi hizo.

***Hatua ya 4***

Waongoze wanafunzi kukumbuka maana ya hali yakinishi na kanushi. Sasa, funza matumizi ya wakati huu uliopita na wakati ujao. Lipitishe hili kwa kutumia hali yakinishi ikiambatana na hali kanushi kwa kurejelea mifano waliyotoa wanafunzi.

***Hatua ya 5***

Waongoze wanafunzi katika kusoma vifungu vya habari chini ya wakati uliopita na wakati ujao katika vitabu vyao. Unapokuwa unafanya hivyo, ukumbuke ya kwamba ile sehemu ya jedwali inaweza kupanuliwa na ikawa na mifano mingi zaidi pande zote mbili.

Hakikisha kuwa mifano inayotolewa inaangazia shughuli mbalimbali za jumuiya (shughuli zilizofanywa na zitakazofanywa).

***Hatua ya 6***

Unaweza baada ya hapo, kuwaongoza wanafunzi kujua ni mabadiliko gani yatokeapo kwa -li- na -ta- kutoka hali yakinishi hadi kanushi.

## Suala mtambuka.

Kipindi hiki kinatoa nafasi nzuri ya kujadili usawa wa jinsia kutokana na kifungu cha habari.

**Tathmini**

Tathmini uwezo wa mwanafunzi wa kutumia kwa usahihi wakati uliopita -li- na wakati ujao -ta- katika hali yakinishi na kanushi.

**Mifano ya sentensi**

Waelekeze wanafunzi warejelee mifano ya sentensi iliyotolewa katika Kitabu cha Mwanafunzi. Ifuatayo ni mifano ya sentensi watakazotunga.

**Sentensi za wakati uliopita**

| Hali yakinishi | Hali kanushi |
|---|---|
| 1. Wanakijiji walihudhuria mkutano. | Wanakijiji hawakuhudhuria mkutano. |
| 2. Bibi harusi alichelewa kufika kanisani. | Bibi harusi hakuchelewa kufika kanisani. |
| 3. Mazishi yalifanywa saa za alasiri. | Mazishi hayakufanywa saa za alasiri. |
| 4. Maharusi walipewa zawadi nyingi. | Maharusi hawakupewa zawadi nyingi. |
| 5. Watu wengi walizoa taka mitaani. | Watu wengi hawakuzoa taka mitaani. |

**Sentensi za wakati ujao**

| Hali yakinishi | Hali kanushi |
|---|---|
| 1. Wanakijiji watahudhuria mkutano. | Wanakijiji hawatahudhuria mkutano. |
| 2. Bibi harusi atachelewa kufika kanisani. | Bibi harusi hatachelewa kufika kanisani. |
| 3. Mazishi yatafanywa saa za alasiri. | Mazishi hayatafanywa saa za alasiri. |
| 4. Maharusi watapewa zawadi nyingi. | Maharusi hawatapewa zawadi nyingi. |
| 5. Watu wengi watazoa taka mitaani. | Watu wengi hawatazoa taka mitaani. |

## Zoezi la ziada

Wape wanafunzi zoezi la kuandika ratiba ya shughuli mbalimbali za kusafisha shule na maelekezo katika kila shughuli itakayofanywa.

## Kipindi cha 20

**Funzo**

Maswali ya marudio

**Shabaha**

Kufikia mwishoni mwa kipindi hiki, mwanafunzi aweze:

Kujitathmini na kuona kama ameyaelewa vilivyo yote waliyofunzwa katika sura hii.

**Zana na kifaa muhimu kwa kipindi hiki**

i) Kitabu cha Mwanafunzi

**Mbinu**

Kujibu maswali ya marudio madaftarini na baadaye kusahihisha majibu ya mwanafunzi.

## Utaratibu

***Hatua ya 1***

Baada ya kuwapongeza wanafunzi na kuwatia ari ya kutaka kujifunza mengi zaidi kuhusu lugha hii, waongoze kujibu maswali ya sehemu hii.

***Hatua ya 2***

Waongoze wanafunzi kusahihisha majibu yao ya sehemu hii. Wanaweza kubadilishana madaftari yao na kusahihishiana hizo kazi zao. Iwapo mbinu hii itatumika, basi ni sharti uyapitie madaftari hayo ili kuhakikisha kuwa tuzo hazikutolewa pale ambapo hazikustahili kutolewa.

**Tathmini**

Tathmini uwezo wa mwanafunzi wa kujibu maswali ya marudio kwa usahihi.

**Majibu ya maswali ya marudio**

1. *Ubudehe* ni utaratibu wa kijamii ambapo wa wanaoishi katika maeneo jirani hufanya kazi pamoja kama vile kupalilia mashambani, kujengeana nyumba pamoja na shughuli nyinginezo za kuinua hali za maisha yao.
2. Kulinganisha na kutofautisha mazishi na harusi

| Mazishi | Harusi |
|---|---|
| 1. Huhusisha shughuli za kumzika mtu aliyeaga dunia. | Huhusisha kuwaunganisha mwanamume na mwanamke ili waishi mume na mke |
| 2. Shughuli za mazishi hufanywa katika hali ya huzuni. | Shughuli za harusi hufanywa katika hali ya furaha. |
| 3. Watu humkumbuka mtu aliyeaga dunia wakati wa uhai wake. | Watu huwatakia maharusi maisha ya upendo na furaha. |
| 4. Huhusisha jamii. | Huhusisha jamii. |
| 5. Roho ya aliyeaga dunia huombewa ili ipate amani ya milele. | Maharusi huombewa ili waishi kwa upendo na wajaliwe watoto. |
| 6. Aliyeaga dunia huvalishwa sanda na kutiwa katika jeneza. | Maharusi huvaa mavazi ya kupendeza; aghalabu bibi harusi huvaa gauni nyeupe. |
| 7. Ibada ya wafu hufanywa. | Ibada ya kuwaunganisha rasmi maharusi hufanywa. |

| | |
|---|---|
| 8. Kiongozi wa kidini huhusishwa. | Kiongozi wa kidini huhusishwa. |
| 9. Hakuna burudani katika shughuli za mazishi. | Burudani hushirikishwa katika sherehe. |
| 10. Huwepo vinywaji na vyakula kwa waliohudhuria. | Huwepo vinywaji na vyakula kwa waliohudhuria. |

3. a) Wahusika wakuu
    i) Mazishi – wahusika wakuu ni jamaa za marehemu (wafiwa), kiongozi wa kidini, marafiki za marehemu (waombolezaji).
    ii) Harusi – wahusika wakuu ni bibi na bwana harusi, wapambe wao, wazazi wa maharusi, kiongozi wa kidini, waumini, jamaa na marafiki za maharusi
    iii) Ibada msikitini au kanisani – imamu msikitini, na kasisi kanisani, waumini

   b) Tofauti za kimawasiliano
    i) Mazishi – Lugha ya majonzi na upole hutumiwa.
    ii) Harusi – Lugha ya furaha na shangwe hutumiwa.
    iii) Ibada msikitini na kanisani – rejesta ya kidini hutumiwa

4. Kutunga sentensi
   a) Shughuli za kuzuia mmomonyoko wa udongo huhusisha **kuchimba mitaro**.
   b) Ni muhimu kusomba maji wakati wa misimu ya mvua.
   c) Bibi na bwana harusi hutakiwa kula kiapo cha kudumisha ndoa yao.
   d) Mwanamume hutakiwa kupeleka mahali kwa wazazi wa msichana kabla ya siku ya harusi.

5. Mwanafunzi aeleze angalau sherehe nne ambazo hufanyika katika jamii yake. Sherehe hizo ziwe, kwa mfano,
   a) Harusi – Huhusisha kuwaunganisha mwanamume na mwanamke ili waishi mume na mke.
   b) Mazishi – Huhusisha shughuli za kumzika mtu aliyeaga dunia pamoja na kusherehekea maisha yake.

6. Mwanafunzi achague shughuli fulani ya kijamii na achukulie kwamba yeye ni kiongozi wa kikundi kinachofanya shughuli hiyo. Kikundi hicho kinaweza kuwa cha vijana wanaoshiriki mradi wa kilimo. Katika mfano kama huu, mwanafunzi aeleze shughuli zinazofanywa na kikundi hicho kama vile kilimo cha mimea, ufugaji na shughuli nyinginezo. Jambo muhimu ni mwanafunzi aonyeshe kuthamini ushirikiano katika jamii.

7. Manufaa ya kazi za *umuganda*

   Jamii hushirikiana kufanya kazi za kuinua hali zao. Ushirikiano huo huleta umoja. Kazi zinazofanywa kwa pamoja ni kama vile: kuzuia mmomonyoko wa udongo,

kusafisha mazingira, kupanda miti, kulima na kupalilia mashamba.

8. i) kuwepo kwa alama ya kiulizi (?)

   ii) matumizi ya viulizi kama vile: nani, gani, yupi, lini, ngapi na kadhalika.

9. Mifano ya sentensi

   a) Kiatu kipi kimeshonwa? (Viatu vipi vimeshonwa?)

   b) (Vitambaa vingapi vinapendeza?)

   c) Kitabu gani kimesomwa? (Vitabu gani vimesomwa?)

   d) Kikwazo kipi kilikiukwa? (Vikwazo vipi vilikiukwa?)

   e) (Visa vingapi vitaandikwa?)

10. Saba: nomino, vitenzi, vielezi, vivumishi, viunganishi, vihisishi, viwakilishi

11. Mwanafunzi aonyeshe uwezo wa kubainisha vihisishi katika lugha ya Kinyarwanda. Hakikisha kwamba wametaja vihisishi hivyo darasani huku ukiviorodhesha darasani. Waongoze kutafuta visawe vyake katika Kiswahili na kuvitumia katika sentensi sahihi.

12. a) Nomino ni neno litajalo jina la kitu, mtu ama jambo na huweza pia kuitwa jina.

    b) Mifano ya sentensi zenye nomino mbalimbali

       i) **Ndoa** hiyo iliwafurahisha watu sana. (*nomino ya kawaida*)

       ii) Ndoa hudumu ikiwa mume na mke wana **upendo**. (*nomino dhahania*)

       iii) **Kwaya ya waimbaji** wa nyimbo za injili iliimba kwa sauti ya juu. (*nomino ya jamii*)

       iv) Daima **Iliza** alitamani harusi ya kupendeza. (*nomino ya pekee/ maalumu*)

       v) **Maakuli** katika sherehe hizo za harusi yalifurahiwa sana. (*nomino ya wingi*)

       vi) **Kuimba** kwake kulipendeza. (*nomino ya kitenzi-jina*)14.

       samehe hisi kurehemu rehemu fikiri lia

13. samehe, hisi, kurehemu, rehemu, fikiri, lia,

14. Vivumishi vya sifa: Haya ni maneno yatajayo tabia au sifa za kitu.

    Vivumishi vya pekee: Hutoa habari kuhusu nomino kwa njia ya kipekee.

    Vivumishi vionyeshi: Hutumiwa kuonyesha alipo mtu au kitu, yaani kuonyesha ujirani.

    Vivumishi vya idadi: Haya ni maneno yanayoonyesha idadi ya watu ama vitu.

    Vivumishi viulizi: Hili ni kundi la vivumishi ambavyo hutumia viulizi kuulizia swali.

    Vivumishi vimilikishi: Vivumishi katika kundi hili hujibu swali Mtu, kitu au jambo ni la nani?

    *Hakikisha kuwa sentensi au mifano iliyotolewa na mwanafunzi ni sahihi.*

15. Viunganishi huunganisha maneno lakini vihisishi huonyesha mahangaiko ya moyo.
16. Aya kuhusu shughuli ya kijamii huku aina saba za maneno ya Kiswahili zikitumika

    Kiongozi wa kijiji (*nomino*) alifika (*kitenzi*) mapema (*kielezi*). Aliwakuta wanakijiji wakingoja mkutano uanze. Wanaume na (*kiunganishi*) wanawake walikuwapo. Lo! (*kihisishi*) Hata walikuwapo watoto wadogo (*kivumishi*). Wao (*kiwakilishi*) labda walifika kujionea watu tu.
17. i) Sitaenda Kigali. (hali kanushi)
    ii) Wataenda harusini.
    iii) Nitashiriki katika kazi zote kijijini. (hali yakinishi)
    iv) Ataniita siku ile.
    v) Hawatachelewa leo. (hali kanushi)
18. Umuhimu wa ushirikiano
    a) Jamii huishi kwa amani bila mizozo.
    b) Nchi hupiga hatua za kimaendeleo.
    c) Shughuli za kijamii huwa rahisi kwa sababu watu wote hushiriki.
    d) Umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu. (methali hii inaeleza ukweli kuhusu umuhimu wa ushirikiano)
19. Mambo muhimu yalisomwa katika Sura ya 4
    a) Matumizi ya msamiati mwafaka unaotumiwa katika shughuli mbalimbali za kijamii, kwa mfano kazi za umuganda, mikutano ya hadhara, kanisani na msikitini na katika sherehe mbalimbali kama vile harusi na mazishi..
    b) Kubaini tofauti za kimawasiliano kutoka shughuli moja ya kijamii hadi nyingine na kubainisha wahusika wakuu katika mawasiliano hayo.
    c) Kuainisha na kubainisha aina za maneno ya Kiswahili kama yalivyotumiwa katika matini mbalimbali.
    d) Kubaini matumizi sahihi ya viambishi vya wakati katika hali yakinishi na kanushi.
    e) Jinsi ya kueleza mambo mbalimbali yafanyikayo katika shughuli mbalimbali za kijamii.

# Faharasa

| | | |
|---|---|---|
| **adimika** | – | kosa kupatikana kwa urahisi |
| **ambukiza** | – | enezea ugonjwa |
| **andaa** | - | tayarisha |
| **ankra** | – | orodha ya vitu vilivyouzwa pamoja na bei ya kila bidhaa |
| **anuani** | – | maelezo ya mahali mtu anapoishi ambayo huandikwa katika barua |
| **asali** | – | namna ya kitu kioevu na kitamu sana kitengenezwacho na nyuki |
| **azma** | – | lengo au shabaha |
| **bainisha** | – | tambua jambo |
| **bao** | – | mpira kuingia katika lango katika mchezo wa kandanda (goli) |
| **baridi kali** | – | hali isiyokuwa na joto na isisimuayo sana mwili |
| **bei** | – | kiasi cha pesa kinachotumiwa kununulia ama kuuzia bidhaa fulani |
| **burudani** | - | starehe |
| **burudisha** | – | sababishia raha |
| **chai** | – | zao la mchai |
| **dumisha** | – | endeleza |
| **faranga** | – | pesa, fedha, dirhamu, senti, fulusi |
| **filisika** | – | ishiwa na mali |
| **fyeka** | – | kata nyasi |
| **gharamia** | – | lipia gharama |
| **harage/haragwe** | – | nafaka ya jamii ya kunde |
| **haramu** | – | -siyoruhusiwa, -siyokuwa halali |
| **Hisabati** | – | sayansi ya tarakimu ijumuishayo aljebra |
| **hitaji** | – | kuwa na haja ya kitu |
| **huzuni** | – | hisia za majonzi |
| **ibuka** | – | tokeza |
| **idadi** | – | hesabu au jumla ya vitu |
| **ilani** | – | tangazo la kuonya watu wasifanye jambo fulani hasa lenye kuleta madhara |
| **ingawa** | – | hata ikiwa |
| **jadhba/jazba** | – | hisia isababishayo kujisahau |

**jamii** – watu wanaoishi pamoja
**jangili** – mwindaji haramu
**jedwali** – orodha ya maelezo kuhusu mambo fulani kwa namna yatakavyofuatana
**jibini** – chakula kinachotengezwa kwa kuyagandisha maziwa na kuyatoa
maji
**jukumu** – wajibu
**jumuiya** – mkusanyiko wa watu
**kabuti** – koti zito la kuzuia baridi
**kagua** – chunguza kwa makini
**kahawa** – zao la mkahawa ama mbuni
**kandanda** – mchezo wa miguu
**kauli** – usemi
**kiasili** – kienyeji
**kifaa** – chombo
**kikao** – mkutano
**kipindi** – muda
**kipusa** – pembe ndogo ya kifalu
**kivuna nafaka** – mashine kama trekta ambayo huvuna ngano huku
ikiitoa wishwa
**kiwanda** – mahali panapotengenezwa bidhaa
**kodi ya mapato** – fedha zinazolipwa serikali kama ushuru wa mapato ya mtu
**kupanda** – tia mbegu mchangani ili ziote
**limbikiza** – weka vitu kidogo kidogo ili viwe vingi
**lishe bora** – chakula kinachohitajika kwa afya nzuri ya mwili
**maabara** – mahali mnamofanyiwa majaribio ya kisayansi
**maalumu** – -enye sifa ya kipekee
**mada** – kiini cha jambo linalozungumziwa
**majira** – wakati au kipindi
**majira ya kiangazi** – kipindi cha kiangazi
**majira ya kipupwe** – kipindi cha baridi
**majira ya mvua** – kipindi cha mvua
**majira ya vuli** – kipindi cha mvua chache
**majivuno** – hali ya kujiona
**manufaa** – faida

**mapato** – kitu kinachopatikana kama vile baada ya kufanya kilimo ama kufanya biashara.

**masuala mtambuka** – mambo muhimu yanayoiathiri jamii katika kipindi cha sasa

**matini** – kifungu cha habari iliyoandikwa

**mazingira** – mambo yanayotuzunguka mahali tunapoishi

**maziwa** – kitu kioevu kitokacho ndani ya titi la mnyama

**mbatata** – namna ya viazi vilivyo mviringo na visivyo na ladha

**mbinu** – njia au namna ya kufanyia jambo

**mbuga** – eneo lililotengewa wanyama wa porini

**mchele** – mpunga uliokobolewa,yaani kuondolewa mashuke

**mfawidhi** – mtu aliyepewa wajibu wa kuendesha shughuli fulani, kama vile mkutano au sherehe fulani

**mfugaji tajiri** – mfugaji ambaye ana mali nyingi

**mifugo** – wanyama wanaotunzwa nyumbani

**mikahawa** – mimea izaayo kahawa

**mkulima tajiri** – mkulima ambaye ana mali nyingi

**mmomonyoko** – kuchukuliwa kwa udongo wenye rutuba

**mori** – hasira kali

**mshinde** – aliyeshindwa

**mshindi** – aliyeshinda

**msimu** – majira

**mtama** – zao la mtama

**muhogo** – mzizi wa muhogo unapokuwa umekomaa tayari kwa kuliwa

**ndama** – mtoto wa ng’ombe

**ndizi** – tunda la mgomba linalomea kwenye mkungu.

**ngeli** – kikundi cha majina au nomino zinazofuata kanuni sawa za kisarufi

**njugu** – mbegu zitengenezewazo mafuta ya karanga

**nyama** – sehemu laini ya mwili ambayo ikikatwa hutoka damu

**pandwa** – ingiwa na

**pekee** – pweke; bila ya -ingine

**pesa** – noti na sarafu zinazotolewa na kuidhinishwa na serikali kuwa ni fedha rasmi za kubadilishana na bidhaa.

**pori** – mahali palipo na miti mingi, nyasi na vichaka

**ratiba** – mpango wa mfululizo wa shughuli fulani

| | | |
|---|---|---|
| **refa** | – | mwamuzi katika mchezo wa mpira |
| **rejesta** | – | lugha inayotumiwa katika mahali maalum, kama vile hospitalini, hotelini, msikitini na kwingineko |
| **rutuba** | – | mbolea ya kukuzia mimea ardhini |
| **sajili** | – | rejesta |
| **shabiki** | – | apendaye sana timu |
| **sheria** | – | kanuni za kuongoza watu |
| **shime** | – | neno la kuhimizia mtu |
| **shiriki** | – | husika au kuungana na watu katika kufanya shughuli fulani |
| **soseji** | – | namna ya chakula kinachotengenezwa kutoka kwa nyama ya nguruwe au ya ng'ombe |
| **suala** | – | jambo au hoja |
| **sufu** | – | manyoya ya kondoo |
| **takwimu** | – | nambari zinazoeleza ukweli kuhusu matukio ya mambo, kwa mfano idadi ya watu katika eneo fulani |
| **tambua** | – | fahamu au maizi |
| **tanbihi** | – | maelezo yanayotoa habari muhimu |
| **tathmini** | – | pima |
| **tegemea** | – | weka matumaini kupata kitu |
| **tia mdomoni** | – | kumsema ama kumsengenya mtu |
| **ulinzi** | – | ulindaji, hali ya kulinda |
| **upanzi** | – | upandaji (uwekaji mbegu ardhini) |
| **utafiti** | – | uchunguzi wa kisayansi |
| **vanila** | – | kiungo kiyafanyayo maziwa yaliyoganda kuwa na ladha ya kupendeza |
| **viazi vitamu** | – | namna ya viazi vikubwa na vilivyo vitamu |
| **wadau** | – | mtu mwenye maslahi katika shughuli fulani |
| **wadhifa** | – | madaraka au cheo fulani |
| **waligonga ndipo** | – | walisema ukweli |
| **wasifukazi** | – | maadishi yanayoeleza kuhitimu kwa mtu katika kutekeleza kazi fulani, aghalabu, kimasomo, tajiriba ya kazi na ujuzi wake |
| **wishwa** | – | takataka za nafaka kama vile mtama au ngano |
| **yakinishi** | – | hali ya kukubali |
| **zao** | – | kile kinachozaliwa na mmea |
| **zaraa** | – | kilimo |

**Vitabu vya rejea**


Kagwa, F.M. na Waihiga, G. (2007) *Kamusi Changanuzi ya Methali.* Nairobi: Moran (E.A.) Publishers.

Kipande, M. (2013) *Sarufi*. Nairobi: Moran (E.A.) Publishers.

Massamba D.P.B. (2004) *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha.* Dar es Salaam. TUKI.

Mogambi Hezron (2007) *Premier Golden Tips; Kiswahili kwa Shule za Upili.* Nairobi: Moran (E.A.) Publishers.

Mutali Chesebe (2010) Premier Golden Tips; *Stadi za Uandishi wa Insha.* Nairobi: Moran (E.A.) Publishers.

Oxford University Press (2013). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu.* Toleo la tatu.
Oxford University Press.

Rwanda Education Board. (2015) *Kiswahili Sylabus for Ordinary Level. S1-S3.* Kigali: Rwanda Education Board.

TUKI (1990) *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha.* Dar es Salaam. TUKI.